

UCHANGANUZI WA KIMTINDO WA ZINGUO LA MZUKA NA MBAYA WETU

NA

HUDSON NYANDIWA

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili
katika Chuo Kikuu cha Nairobi**

2015

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote kile kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Sahihi.....Tarehe.....

Nyandiwa Hudson

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi.....Tarehe.....

Prof. Mwenda Mbatiah

(Msimamizi)

Sahihi.....Tarehe.....

Dkt. Nyachae Michira

(Msimamizi)

TABARUKU

Kazi hii nawatabarukia wafuatao: marehemu babangu Charles Jombo Nyandiwa aliyenifaa sana kwa kunilea na kunielimisha. Bila shaka wosia wake *'Nyathi e maumo dug janyuol'* hunikumbusha nyakati muhimu nilizopiga gumzo naye hasa nyakati za mwishomwisho wa maisha yake. Mungu amrehemu. Vilevile kwa marehemu nyanyangu Ludia Ang'ailwa Isiaho, ulinifaa zaidi ya wote katika umri wangu mdogo kwa kujitwika mzigo wa malezi; bila wewe sijui ningekuwa wapi. Mamangu Jenipher Mwangale Nyandiwa kwa juhudi zake za kunilea na kunielimisha na hata kuvumilia nyakati ngumu nilipoamua kuzamia. Mchumba wangu Beatrice Achieng Owana kwa kustahimili upweke na ukiwa wakati wa masomo yangu, shukrani za dhati kwa kunipa moyo wakati wote.

SHUKRANI

Natanguliza kwa kumrudishia Maulana shukrani za dhata kwa kunipa uhai, nguvu, afya na uwezo wa kuikamilisha kazi hii. Vilevile, natoa shukrani zangu za dhata kwa wote ambao kwa njia moja au nyingine wamenifaa katika shughuli zangu za kiusomi.

Kukamilika kwa tasnifuu hii kumekuwa mchango wangu, wasimamizi wangu Prof. Mwenda Mbatiah kwa mawaidha yake yenye kina pamoja na maswali yenye uchochezi ya kiuchanganuzi aliyonirushia haswa nilipomtembelea afisini na mkahawa wa Ronalo Mjini Nairobi na mijadala mingi ambayo ilinifaa na itakayonifaa maishani. Dkt. Nyachae Michira kwa kuniongoza, kunipa mawaidha na kunitia shime niliposhughulikia kazi hii.

Shukrani pia nazitoa kwa wahadhiri wa Kiswahili katika Idara ya Kiswahili wakiwemo Prof. Kineene wa Mutiso kwa mawaidha yake ya kina ambayo hata yalikiuka mipaka ya tasnifu lakini yatanifaa maishani, Prof John Habwe, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Amir Swaleh, Bw. B. Mungania na Bi. Mary Ndung'u. Mlitufundisha kwa umahiri wa kuigwa na kutufaa pakubwa.

Katika safari hii siwezi kuwasahau wahadhiri Dkt. Ayub Mukhwana wa Chuo Kikuu cha Nairobi na Dkt. Maurice Odhiambo wa Chuo Kikuu cha Bondo kwa kunitia shime ya kuendelea na masomo. Mungu awajazie baraka zake. Kamwe siwezi kuwasahau wenzangu niliokuwa nao katika darasa la uzamili nikianza na Lidya Shaviya (Shemeji); ulinifaa kwa hali na mali haswa wakati wa jua na kiangazi, Dina Osango, Paul Sito, Queen Ndoni, Damaris Otuoma, Peter Kilonzo, Edward Zani, Flora Omosa, Rose Nyamemba, Magdalin Yegon, Gladys, Evelin, Julita Wanjala, Rose Mutunga, Mutahi Miricho, Phanice Marisya na Judith Kemnto.

Kwa pamoja tulikwea na kushuka milima mingi. Mijadala tuliyokuwa nayo ilitufaa. Ahsanteni sana walionitangulia; Vincent Oiro na Benard Ogolla pia nawashukuru, mlinifaa sana kwa mawaidha na makala mbalimbali.

Shukrani za dhata pia kwa kakangu Padre Benard Isiaho Omondi SJ kwa kunivisha wakati huu wote, ndugu zangu Otieno, Ochieng na Odongo. Dada Atieno, Akumu, Achieng na Adhiambo. Marehemu nyanyangu Ludia Isiaho kwa kunipa elimu ya shule ya

msingi, mamangu Jenipher Mwangale Nyandiwa kwa kunizaa na kunilea, babangu Charles Jombo Nyandiwa kwa kunielimisha na kunipa wosia, mke wangu Beatrice Achieng Owana kwa kuvumilia wakati mgumu haswa nilipotaka kuachwa pekee ili nitafakari kuhusiana na kazi hii; ulielewa hali hii.

Shukrani za pekee pia ni kwa mwanangu Glen Isaack Nyandiwa kwa kukubali kuchukua nafasi yangu kama mzazi na kuwatunza wenzake nilipokuwa safarini Nairobi katika shughuli za kimasomo; Glen ufaafu wako ni wa kipekee Mungu akujalie maishani, ulinielewa nilipoadimika nyumbani. Nana Velma Adhiambo (Nyasango) aliyenihurumia na kuniomba anisaidie kuikamilisha kazi hii, Samuel Okoth (Jasango) aliyenirai kuifungua tarakilishi ili niendeleo na kazi pamoja na mwanangu mpendwa Charles Nyandiwa kwa kunipa moyo wa kuendelea kutia bidii tulipokutana mjini Nairobi.

Shukrani zingine ni kwa marafiki zangu ndugu Caleb Otieno Nyakiti na kakake Samuel Okoth Nyakiti na rafiki Austine Odhiambo Bitwa kwa kunifaa kwa hali na mali. Mungu awatunukie baraka tumbitumbi. Mwisho ni kwa mwalimu wangu mkuu Bw. Owino Amollo kwa kunielewa nilipohitaji wakati wa kuishughulikia kazi hii.

Sitakiacha nyuma Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunipa nafasi ya kusomea shahada hii ya uzamili. Shukrani nyingi vilevile kwa kakangu Fred Odongo Nyandiwa kwa kujitolea kupiga chapa ya kazi hii ambayo wengi huiogopa. Ilikuwa si rahisi lakini uliifanya kwa tabasamu. Moyo wangu wanambia niwashukuru nyote.

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu uchanganuzi wa kimtindo katika *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu*. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza matumizi ya sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora katika tamthilia zinazohusika. Tulichochea na ufahamu kwamba mtindo na dhana ya maudhui ni vitengo muhimu vya fasihi ambavyo huandamana na kuegemeana ili kufanikisha dhamira ya mwandishi kwa wasomaji wa kazi yake. Uchochezi huu ulikuwa na ukweli kwamba matumizi ya tamathali za usemi huondoa uchapwa katika kazi za sanaa pamoja na kuwa matumizi ya tamathali za usemi si ya kiajali ila hutumika kimakusudi. Matumizi ya tamathali hizi huwa ni kuwasilisha ujumbe kimuktadha ili kuwezesha uelewa wa matini kwa kina. Utafiti uliongozwa na nadharia ya elimumitindo inayohusu uchanganuzi wa mbinu zote za lugha ambazo hutumika katika mawasiliano ambayo hujumuisha mawasiliano ya fasihi na mawasiliano yasiyokuwa ya fasihi. Ni wazi kuwa tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora husheheni maana zinapotumika katika muktadha na bila muktadha ni vigumu kuchanganua tamathali yoyote kisemantiki. Kwa hivyo matini huzipa muktadha wa uchanganuzi. Baada ya kuzisoma tamthilia hizi tulitambua kuwa tamathali za usemi tulizotaja hapo juu zilitumika katika tamthilia za *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*. Tulizichanganua kwa kurejelea muktadha wa matumizi yazo kwenye matini hizi. Iligundulika kuwa matumizi ya vipengele vya tamathali za usemi vya sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora vimechangia katika kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui katika tamthilia zinazohusika. Kwa hivyo iligunduliwa kwamba msanii hutawala lugha kiufundi ili kuonyesha tofauti kati ya lugha ya fasihi na lugha ya kawaida. Aidha, tamathali za usemi hutumiwa na msanii kimakusudi. Kwa hivyo ujumbe ulioko kwenye tamathali hizi huwasilishwa kwa kuzingatia muktadha na vilevile, ni vigumu kuchanganua usemi wenye ukiushi ambao hutokea katika hali isiyokuwa na muktadha. Isitoshe, iligunduliwa kwamba ukiushi katika tamathali za usemi huwezesha uelewa wa kina wa matini. Muktadha wa kiisimu huchangia kutoa maana ambayo mwishowe huibua na kuwasilisha maudhui na kwa hivyo kuifanya kazi ya sanaa kuwa na maudhui ya pekee kutokana na ukiushi kwenye usemi huo na mwisho lugha huwa na uwili usioepukika, yaani uwakilishi wa maana ya kisanii na maana ya kimawasiliano. Napendekeza na kutilia mkazo kwamba vipengele vya fani

kama vile muundo, wahusika na mandhari vichunguzwe katika tamthilia hizi mbili. Vilevile ukiushi wa kisintaksia, kileksika na wa kisarufi waweza kuchunguzwa. Aidha, nadharia tofauti na tuliyotumia yaweza kutumiwa.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
YALIYOMO.....	viii
SURA YA KWANZA	1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti	3
1.3 Madhumuni ya utafiti huu ni:	4
1.4 Nadharia Tete.....	4
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	4
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	5
1.7 Msingi wa Kinadharia.....	6
1.7.1 Kipindi cha Wagiriki na Warumi wa Kale	6
1.7.2 Uhindi wa Kale	6
1.7.3 Karne ya Katikati	6
1.7.4 Karne ya Ishirini	7
1.7.5 Dhana ya Ukiushi.....	8
1.7.6 Ukiushi na Fasihi	9
1.7.7 Umuhimu wa Ukiushi	10
1.7.8 Mihimili ya Nadharia Hii.....	15
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusiana na Mada	15
1.9 Mbinu za Utafiti.....	19
SURA YA PILI	20
UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA ZINGUO LA MZUKA.	20
2.0 Utangulizi.....	20
2.1 Sitiari.....	21

2.2 Chuku.....	45
2.3 Tashbihi.....	59
2.4 Tashihisi.....	61
2.5 Kejeli.....	65
2.6 Tanakuzi.....	69
2.7 Oksimora.....	73
2.8 Hitimisho.....	74
SURA YA TATU.....	75
UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA MBAYA WETU.....	75
3.0 Utangulizi.....	75
3.1 Sitiari.....	75
3.2 Chuku.....	82
3.3 Tashbihi.....	88
3.4 Tashihisi.....	95
3.5 Oksimora.....	100
3.6 Tanakuzi.....	105
3.7 Kejeli.....	107
3.7 Hitimisho.....	108
SURA YA NNE: HITIMISHO.....	109
4.0 Utangulizi.....	109
4.1 Kuhusu Madhumuni ya Utafiti.....	109
4.2 Kuhusu Nadharia Tete.....	111
4.3 Changamoto za utafiti.....	112
4.4 Mapendekezo.....	113
Marejeleo.....	114

SURA YA KWANZA

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Mtindo katika fasihi hurejelea matumizi ya lugha. Lugha ya fasihi ni ya kihisia na hubeba dhamira ya mwandishi. Mbali na kuwasilisha ujumbe fulani, lugha ya fasihi humshawishi msomaji ili kujaribu kuathiri au hata kubadilisha msimamo wake. Ili kumwathiri msomaji kihisia na kimawazo, mwandishi hufinyanga lugha yake kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia tamathali za usemi; ambacho ni kipengele cha mtindo.

Mohamed (1995:9) anasema kuwa fani ni kunga au mbinu azitumiazo mwandishi kuwasilishia maudhui yake. Anasisitiza kuwa fani ni kipengele muhimu ambacho kazi yoyote ya sanaa yapaswa kuwa nacho. Anasema kazi yoyote ya fasihi lazima iwe na fani na maudhui. Katika uhusiano wa fani na maudhui anafafanua kuwa maudhui ni jumla ya mambo yanayohusiana na yale mwandishi anayokusudia kuyaeleza na fani ni mbinu ambazo zinatumiwa katika lugha ili kuyaeleza hayo mwandishi aliyokusudia kuyaeleza. Maelezo haya ni muhimu kwani fani ni mbinu pana na iliyobeba mtindo.

Mbatiah (2001:13) ana maelezo kuwa fani ni jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya fasihi vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahususi. Kwa hivyo dhana ya fani ni mjumuiko mbalimbali wa vipengele vya kisanaa ambavyo huchangia katika ukamilifu wa kazi fulani. Maelezo haya yanaifanya dhana ya fani kuwa pana sana na ikiwa itashughulikiwa katika matini moja basi uchunguzi huo utakuwa na data kubwa.

Wamitila (2003:190) anakubaliana na Mbatiah (2001) kwamba fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuiwasilisha dhamira na maudhui yake. Wamitila anaendelea kusema kuwa mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kutumia lugha. Lugha anayotaka kuitumia mwandishi pia lazima iwe na vikolezo au vitia ladha fulani. Kwa hivyo mwandishi lazima ategemee fani.

Leech na Short (1981:10) wanasema neno mtindo hutumiwa kurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani na mtu fulani na kwa lengo fulani.

Vilevile tunaweza kusema kuwa ni ile hali ya kuangalia maelezo yalivyotolewa kueleza dhana fulani.

Senkoro (1982:24) anasema kuwa mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi. Dhana ya mtindo hata hivyo ina fasiri na maelezo mengi tofauti tofauti. Hali hii imetokana na sababu kuwa dhana hii imetambulika kuwa na utelezi mwingi na kuwa si rahisi kuitolea fasiri moja inayokubalika na kila mtu.

Wamitila (2003:19) akizungumzia mtindo anasema mtindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuuwasilisha ujumbe wake. Anaendelea kusema kuwa mtindo huelezea jinsi mwandishi anavyounda kazi yake. Dhana ya mtindo hurejelea sifa maalum za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha kwenye fani yake. Mfano wa mazoea hayo ni: uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, taswira, uakifishi, sentensi na kadhalika. Mazoea haya humpambanua mwandishi mmoja na mwingine.

Wamitila (khj) ana maoni kuwa mtindo huweza kujitokeza kwenye fani na maudhui ya mwandishi fulani. Anapendekeza kuwa tunapochunguza vipengele vya mtindo tunaangalia;

- a. Matumizi ya lugha
- b. Mpangilio wa matukio
- c. Taswira au jazanda
- d. Tamathali za usemi
- e. Ujenzi au usawiri wa wahusika
- f. Mandhari

Kwa hivyo swala la mtindo huhusishwa kwa kiasi kikubwa na sifa na upekee wa mtunzi. Vilevile mtindo huchukuliwa kuwa sifa inayofungamanishwa na muktadha wa kihistoria, kijamii, kiisimu na kadhalika.

Mtindo ni elementi muhimu sana katika kazi ya kifasihi. Ili kuweza kubainisha sifa za kimtindo za kazi ya kifasihi, mchanganuzi wa matini au kazi ya kifasihi anapaswa kuchunguza:

- a. Uteuzi wa msamiati wa mtunzi
- b. Miundo na mipangilio ya sentensi
- c. Uteuzi na matumizi ya tamathali za usemi na jazanda
- d. Motifu na dhamira zinazokaririwa katika kazi za watunzi
- e. Usimulizi na mbinu za usimulizi wenyewe.
- f. Sifa za uakifishaji hasa zinazoelekea kukiuka njia za kawaida za kuakifisha.

Kwa muhtasari, Mbatiah (2003:580) anasema mtindo ni jinsi mtunzi wa kazi ya kisanaa anavyotumia lugha kujieleza. Bila shaka katika kujieleza huku, maudhui hukuzwa na kuwasilishwa kwa wasomaji wa kazi yake. Maoni ya Mbatiah (khj) yanaoana na ya Wamitila (2003:145). Bennet (1979:34) na Senkoro (1982:24) wana maoni kuwa vipengele vyote vya fani vinastahili kuangaliwa katika mshikamano wake ili kazi nzima ikamilike na kueleweka.

1.2 Tatizo la Utafiti

Katika utafiti wetu tumechunguza jinsi vipengele vya kimtindo vya tamathali za usemi vya sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora huchangia na kufanikisha uibuaji, uendelezaji na uwasilishaji wa maudhui na mwishowe kufanikisha dhamira za tamthilia za *Mbaya Wetu* (2014) ya Ken Walibora na *Zinguo la Mzuka* (2011) ya Leonard Sanja Leo. Ili kufanikisha utafiti wa mada hii tumeteua nadharia ya elimumitindo.

Uhakiki tunaoshughulikia umechochewa na ufahamu kuwa mtindo na dhana ya maudhui ni vitengo muhimu vya fasihi ambavyo huandamana na kuegemeana ili kufanikisha dhamira ya mwandishi kwa wasomaji wa kazi yake. Kwa hivyo katika kazi yetu tumeshughulikia uchanganuzi wa tamathali za usemi tulizotaja hapo juu na jinsi tamathali hizo zimefanikisha uwasilishaji wa maudhui katika kazi mbili zilizotajwa hapo juu.

Tunaafikiana na maoni ya wataalam kuwa mtindo na maudhui havitengani kwani katika fani kuna mtindo kama kipengele miongoni mwa vipengele vingine. Katika mtindo kuna

kipengele cha matumizi ya lugha. Katika kipengele hiki cha matumizi ya lugha tumeteua na kuchanganua sitiari, chuku, tashihisi, tashbihi, kejeli, tanakuzi na oksimora. Vipengele hivi vikiwa chini ya mtindo ni muhimu katika kufanikisha ujenzi wa maudhui na hata kuwasilishwa kwayo katika tamthilia tulizoteua.

1.3 Madhumuni ya utafiti huu ni:

- a. Kutambua na kuchanganua tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashihisi, tashbihi, kejeli, tanakuzi na oksimora zilizotumika katika tamthilia za *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*.
- b. Kuchanganua namna vipengele vya kimtindo vya tamathali za usemi vya sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora vinachangia katika kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui katika tamthilia za *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*.
- c. Kudhihirisha kuwa ukiushi katika sitiari, chuku, tashihisi, tashbihi, kejeli na oksimora umechangia katika upekee wa maudhui katika tamthilia za *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu*.

1.4 Nadharia Tete

- a. Tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashihisi, tashbihi, kejeli tanakuzi na oksimora zimetumika katika tamthilia za *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*.
- b. Vipengele vya kimtindo vya tamathali za usemi vya sitiari, chuku, tashihisi, tashbihi, kejeli tanakuzi na oksimora vimechangia katika ujenzi na uwasilishaji wa maudhui katika *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*.
- c. Tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashihisi, tashbihi tanakuzi na oksimora zina ukiushi na kwa hivyo kuibua maudhui ya kipekee katika *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Katika utafiti wetu tumelenga kushughulikia kipengele cha mtindo cha tamathali za usemi tukijikita katika sitiari, chuku, tashihisi, tashbihi, kejeli tanakuzi na oksimora na jinsi tamathali hizi za usemi zimeibua, kuyaendeleza na kuyawasilisha maudhui katika

tamthilia za *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*. Tumejishughulisha na tamthilia hizi kwa kuwa baada ya kuzisoma tuligundua kuwa zina matumizi ya tamathali za usemi tunazolenga na ambazo zimetumika katika hali kiushi. Vilevile tuligundua kuwa kuwepo kwa vipengele vya tamathali za usemi vimetuwezesha kuitumia nadharia tuliyoiteua ya elimumitindo.

Tumechagua tamthilia mbili kutoka kwa waandishi tofauti ili tuweze kuona mwonoulimwengu wa kila mmoja kuihusu jamii licha ya wao kutoka katika jamii moja. Waandishi hawa wawili wameandika katika wakati mmoja, wana mtazamo sawa kuihusu jamii wanamoishi kwani mbali na kuifahamisha jamii matatizo yanayoikumba, kazi zao zinaitahadharisha jamii na kujaribu kuipa mwelekeo kutokana na uozo uliokithiri kuhusiana na maswala ya kiuchumi, utamaduni, maridhiano na siasa na hata uhusiano katika jamii. Aidha, mojawapo ya tamathali za usemi tulizolenga kuchanganua kwa mfano oksimora, hazikujitokeza kwa wingi katika *Zinguo la Mzuka*.

Mbali na hayo sababu nyingine ni kuwa tamthilia hizi ni za hivi karibuni na hazijawahi kushughulikuwa. Vilevile hatuwezi kushughulikia kazi zote za fasihi. Tumeteua mbili tu kutoka kwa waandishi tofauti kwani tamthilia hizi zinalenga maswala ya siasa na uongozi, ambayo ni maswala nyeti katika jamii ya sasa pamoja na changamoto zinazoikumba jamii hususan malezi.

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Katika kazi yetu tumechanganua vipengele vya kimtindo vya tamathali za usemi. Tumetumia nadharia ya elimumitindo kwa kujikita katika kipengele chake cha ukiushi wa kisemantiki tukirejelea vipengele vya kimtindo vya tamathali za usemi tulivyotaja hapo juu na mchango wa maana inayojitokeza kimuktadha kutokana na tamathali hizo na mchango wa maana hizo katika kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui katika tamthilia tulizoteua. Aidha tumejifunga katika nadharia ya elimumitindo katika kuhakiki tamthilia tulizoteua.

1.7 Msingi wa Kinadharia

Katika utafiti wetu tumeongozwa na nadharia ya elimumitindo.

Mbatiah (1999) anasema kwa miaka mingi nadharia mbalimbali za kuchanganulia matini za kifasihi zimetumika kuchanganua kazi hizi. Mbatiah anapendekeza kwamba ni jukumu la mhakiki kuchagua nadharia bora ya kifasihi ya kuchanganulia matini kiwakati. Mbatiah (khj) akimrejelea Raman Selden (1989:12) anasema mhakiki lazima achague nadharia ifaayo. Leech (1969:2) ana maoni kwamba matini za fasihi zaweza kufasiriwa katika mtazamo wa kiisimu. Taaluma ya elimumitindo inafungamanisha uhakiki wa fasihi na isimu. Kwa hivyo, taaluma hii iko katikati ya isimu na fasihi na huzifungamanisha. Msamiati mpana wa uhakiki wa kifasihi hasa sitiari, taswira, kinaya, jazanda, usambamba na kadhalika haviwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu.

1.7.1 Kipindi cha Wagiriki na Warumi wa Kale

Katika kipindi hiki dhana hii ilitumiwa kama balagha. Hii ilikuwa jinsi ya usemaji au mbinu za uwasilishaji usemi kwa njia ya kushawishi au kuathiri msikilizaji. Kulingana nao, mtindo ulikuwa njia ya kuwasilisha usemi kwa nia ya kuwavutia wasikilizaji ili waamini na kukubali yasemwayo. Hivyo mtindo ulikuwa ni uhodari wa kusema. Kasoro iliyokuwako ni kuwa, waliona mtindo katika mazungumzo bali si katika maandishi. Kwa hivyo walihusisha mtindo na mazungumzo tu. Na kwa hivyo mzungumzaji akapewa uhuru wa kuzungumza atakavyo.

1.7.2 Uhindi wa Kale

Katika jamii hii mtindo ulitazamwa kama jinsi ya kurembesha mazungumzo na kuyafanya yavutie na kuwa mazuri. Jamii hii vilevile haikuzingatia maandishi na vilevile walichukulia mtindo kama kurembesha mazungumzo tu.

1.7.3 Karne ya Katikati

Kufikia wakati huu, mtindo ulianza kuhusishwa na fasihi andishi. Kulikuwa na majaribio ya kuigawa mitindo mbalimbali katika lugha na tanzu za fasihi andishi zilizokuwepo. Hivyo, mtindo ukaanza kuhusishwa na sifa za lugha zilizokuwepo katika tanzu za fasihi andishi. Lemonosur M.V. aliyeshi miaka ya 1711 – 1765 alikuwa mfuasi wa mtazamo

huu. Alikuwa mwanataaluma wa kale wa Kirusi. Alijitokeza na mitindo mitatu na tanzu zilizoambatana na mitindo hiyo. Alikuwa na orodha ya: mtindo wa juu, mtindo wa kati na mtindo wa chini. Barua za kirafiki ziliainishwa katika mtindo wa chini, nazo tenzi zikawekwa katika mtindo wa juu. Tanzania vilevile ziliwekwa katika mtindo wa juu. Kasoro iliyokuwako ni kuwa dhana ya mitindo ilianza kuhusishwa na maandishi na kuacha kuhusishwa na mazungumzo.

1.7.4 Karne ya Ishirini

Kufikia mwanzoni mwa kipindi hiki, dhana ya elimumitindo ilianza kuhusishwa na fafanuzi mbalimbali. Kwa mfano mtindo ulihusishwa na tabia za uzungumzaji wa kila binadamu. Hivyo, kufuatana na mtazamo huu ilionekana kuwa kila mtu ana mtindo wake wa kutumia lugha. Kwa hivyo kadri kila binadamu anajifunza lugha na kuitumia ndivyo mitindo inavyoongezeka. Kwa hivyo idadi ya mitindo ya lugha ikawa sawa na idadi ya wazungumzaji wa lugha hiyo.

Katika kipindi hiki mtindo vilevile ulichukuliwa kumaanisha namna ya kuwasiliana. Ilitambulika kuwa binadamu wanaweza kuwasiliana kwa njia nyingi ijapokuwa kuna njia kuu mbili: Mazungumzo na maandishi. Hivyo kukaonekana kuwa kuna mitindo miwili mikuu ya kuzungumza na kuandika. Mtindo katika karne hii ulichukuliwa kuwa namna ya kuwasilisha miguso na maono (hisia) kwa mfano huzuni, hasira, mapenzi, furaha na kadhalika. Kila hisia ilikuwa na mtindo wake. Vilevile mtindo ulichukuliwa kuwa tabia ya mtu binafsi, tabia za kimakundi, tabia ya uteuzi, kama njia ya kujieleza, ukiushi, vazi juu ya wazo na mwisho mtindo ulichukuliwa kiutathmini au kiupimaji. Leech na Short (1981).

Leech (1969:42) amezungumzia viwango katika uchanganuzi wa nadharia ya elimumitindo. Anasema viwango hivi ni muhimu kuzingatwa na mhakiki ili kutekeleza uhakiki kwa njia ifaayo. Leech kwa hivyo anaorodhesha aina za ukiushi wa kaida za matumizi ya lugha ambao hutokea katika mtindo wa kazi za kifasihi.

- a. Ukiushi wa kimsamiati au kileksika
- b. Ukiushi wa kisarufi

- c. Ukiushi wa kilahaja
- d. Ukiushi wa kifonolojia
- e. Ukiushi wa kimaandishi au kigrafolojia
- f. Ukiushi wa rejesta
- g. Ukiushi wa kimapisi au kihistoria
- h. Ukiushi wa kisemantiki.

1.7.5 Dhana ya Ukiushi.

Dhana ya ukiushi ni sharti la kuzingatiwa wakati matini ya kifasihi yanapochunguzwa. Ukiushi kwa hivyo huwa hali ya kimsingi katika kuelewa matini hasa katika mashairi na kazi nyinginezo za fasihi. Ukiushi kwa jumla humaanisha kuondoka katika hali yakini itumikayo katika kuandika na kuzungumza.

Uchunguzi wa maelezo mbalimbali wa dhana ya ukiushi umeonyesha kuwa ukiushi kimsingi ni dhana ya kiisimu. Kwamba ukiushi hutumika mara nyingi katika sarufi na semantiki. Katika hali hii, sarufi imetumika kwa kuzingatia mofolojia, sintaksia na fonolojia. Hata hivyo, yawezekana kuwa ukiushi waweza kushughulikia muktadha mpana kuliko dhana hii inavyoelekezwa katika isimu tu. Hartman na Stork (1973) wana maelezo kuwa ukiushi ni istilahi inayoeleza usemi wowote ambao hauzingatii sheria za kisarufi au kisemantiki kwa kuzingatia lugha ya kipimo.

Leech (1969:5) na Levin: Word vol. XXI (1968:225) wana maoni kuwa ukiushi ni uvunjaji wa sheria zizingatiwazo kwa jumla katika lugha. Ukiushi waweza kuwa na muktadha. Yaani waweza kutokana na matumizi ya lugha kwa hali fulani au lugha hiyo waweza kuonekana isiyokubalika katika muktadha fulani.

Naye Cluysenaar (1976:31) anafafanua dhana ya ukiushi kuwa kuondoka katika maana inayotarajiwa kwa kuzingatia viwango tofauti vya lugha kwa mfano semantiki, leksika, sarufi na fonolojia. Viwango hivyo mbalimbali vyaweza kuwa katika sarufi na fonolojia au katika viwango vya sentensi na kirai.

1.7.6 Ukiushi na Fasihi

Ukiushi huhusishwa na fasihi. Wasomi wengi huwa na mtazamo kuwa ukiushi ni sifa inayobainisha lugha ya kifasihi na lugha isiyokuwa ya kifasihi. Jennipher Schiffer Levine kwa mfano (P.M.L.A. – Volume (94 No. 1:107) ameipigia dhana hii debe kwa kusema kuwa tofauti iliyoko baina ya lugha ya kifasihi na lugha ya kawaida ni kuwa ukiushi ulioko katika lugha ya fasihi huwa ni wa hiari. Wataalam wengine wana maoni kuwa lugha ya kifasihi huwa ni lugha ambayo hukiuka au huonyesha viwango mbalimbali vya ukiushi kwa kutozingatia lugha ya kawaida.

Maoni haya yanadhihirisha ya kwamba tofauti baina ya lugha ya kifasihi na lugha isiyokuwa ya kifasihi imewekewa misingi yake na ukiushi. Vilevile ni muhimu kuzingatia mtazamo wa wengi kuhusu fasihi kuwa dhana ya kisanaa na kwa hivyo wasomi wanaiona dhana ya ukiushi kuwa kigezo cha kazi ya kisanaa yenye thamani.

Wanaisimu wanakubaliana katika viwango tofauti tofauti kuwa lugha huwa na mpangilio ambao huzingatia sheria na ni kwa kupitia sheria hizi ndipo lugha huweza kutumika kwa manufaa ya watumizilugha hiyo. Kinyume na haya ni kuwa lugha ya kifasihi hujumuisha matumizi ambayo huwa tofauti na matumizi ya kawaida au matumizi yasiyokuwa ya kifasihi. Kwa kiwango fulani lugha ya fasihi huwa na vigezo ambavyo vinapolinganishwa na vigezo vya lugha ya kawaida au lugha inayozingatia sheria, huonekana kuwa isiyo ya kawaida au yenye kutokufuata kaida. Kimsingi kazi ya lugha ni kufanikisha mawasiliano. Kwa hivyo ni sawa kusema kuwa waandishi wote huwa na lengo la kuwasiliana kwani waandishi wote hutumia lugha kama malighafi. Waandishi wa fasihi hawazingatii tu kilichosemwa kuwa cha muhimu katika mawasiliano ila wao huambatisha umuhimu wa jinsi kinavyosemwa.

Tunachojaribu kuelewa ni kile kinachochukuliwa kuwa na ubunifu wa kisanii. Kazi iliyo na ubunifu wa kisanii ni ile kazi ambayo huwa na uwezo wa kutawala lugha kiufundi katika hali iliyo tofauti na lugha ya kawaida ambayo siyo ya kifasihi.

Leech (1969:24) ana maoni kuwa mwandishi wa kifasihi akilinganishwa na waandishi wengine, huwa na uhuru na hafungiwi na sheria au kaida za lugha.

1.7.7 Umuhimu wa Ukiushi

Katika kuchunguza ukiushi, kuna mambo mawili muhimu. Kwanza kuna swala la nia, yaani lililomsukuma mwandishi kusema analolisema na pili ni swala la itiko ambalo kwa kiwango fulani hutegemea tafsili za vigezo na mtazamo wa msomaji.

Huddleston (1976:13) ana maoni kuwa usemi wenye ukiushi huwa si wa kiajali au ulio na makosa ila usemi huu hutumika kwa kusudi fulani na mara nyingi hutumiwa na msanii kimakusudi. Sababu ya kutumia lugha kiukiushi kwa kuirejelea matini huwa ni kufanikisha mawasiliano na wakati wowote mwandishi achaguapo kutumia ukiushi huwa ni kwa nia ya kuwasiliana. Kibedi V. (1976:23) anasema kuwa wakati mtu fulani huamua kutumia lugha yenye kuchekesha huwa ana nia ya kuwasilisha ujumbe ambao hauwezi kuwasilishwa kwa kutumia lugha ya kawaida. Kwa mfano ili kigezo chenye ukiushi kuchukuliwa kuwa muhimu na kuhalalishwa kuwepo kwake katika matini, lazima kiwe na uwezo wa kuwasilisha ujumbe. Ukiushi kwa hivyo huwezesha uelewa wa kina wa matini inayoshughulikiwa. Uchanganuzi kimsingi huwa na lengo la kuchimbua nia na sababu ya mwandishi katika muktadha wa jumla ya kazi ya kifasihi.

Wasomi wengi wanakubaliana kuwa vigezo vyenye ukiushi mwishowe huweza kuchanganuliwa. Vilevile wanakubaliana kuwa hakuna mpangilio uliokubalika unaowawezesha wachanganuzi kufikia uchanganuzi ulioibuka. Hii ina maana kuwa mchanganuzi ashughulikiapo usemi wenye ukiushi, yeye huifikia maana aipatayo kwa kuzingatia uwezo wake wa kuelewa, kipaji cha ubunifu wake, uvumbuzi na ubunifu. Kwa hivyo uchanganuzi huu hutegemea wepesi wa kuhisi na kuitikia na uchanganuzi wa kina wa msomaji akizingatia muktadha. Huwa ni vugumu kuchanganua usemi wenye ukiushi ambao hutokea katika hali isiyokuwa na muktadha. Ikiwa usemi unaoshughulikiwa unachunguzwa kimuktadha, fasili yake hujitokeza kwa haraka.

Cluysenaar (1976:19) anasema: hata kwa kutegemea uwezo wetu wa kuelewa, pengine tuwe na uwezo wa kuonyesha au kudhihirisha maana hizo zinavyoibuka kutoka kwenye matini, tutakuwa tunaichosha hadhira na hata kuiogofya hadhira ikiwa hapana muktadha.

Hii ina maana kuwa uchanganuzi lazima uwe na uwezo wa kushawishi na wenye vipimo dhidi ya makubaliano na wachanganuzi wengine. Kuna uwezekano wa kufanya uchanganuzi kuwa wenye kukubalika ikiwa mchanganuzi ataanza kwa muktadha wa kiisimu. Kwanza usemi wenye ukiushi hutambuliwa. Kisha kwa kutumia mtindo wa kiisimu, usemi huo huchanganuliwa jinsi ulivyo kiushi. Hatua inayofuata huwa ni kujaribu kugundua umuhimu wa usemi huo kiushi unaoshughulikiwa. Hali hii yaweza kuhusisha kufasiri au kutathmini au yote mawili kwa lengo la kuyahusisha malengo ya uchanganuzi wa kiisimu na udhahania wa uchanganuzi wa kina. Kwa jumla mwelekeo huu ndio utakaotufaa katika kuchanganua tamthilia tulizoteua hapo juu.

Lugha huwa na uwili usioepukika. Lugha katika ukawaida wake haiwezi kuepuka kuwa yenye uwakilishi na yenye maana. Kauli hii vilevile inaunga mkono hoja kuwa lugha haiwezi kuepuka kuangaliwa katika mtazamo wa kisanii na mtazamo wa mawasiliano. Ili ukiushi uwe na umuhimu ni lazima uangaliwe kimawasiliano. Hali hii humfanya msomaji kumakinika na kila wakati apatapo kigezo chenye ukiushi, hupunga na kujaribu kutathmini sababu ya mwandishi kutumia kigezo hicho kwenye matini kwa kuegemea muktadha uliotumika.

Leech na Short (1981) wana maelezo kuwa elimumitindo ni uchanganuzi wa mtindo. Wanasema nadharia ya elimumitindo huonekana kugawika kuwili. Kwa upande mmoja inaitwa elimumitindo ya kifasihi na kwa upande mwingine inaitwa elimumitindo ya kiisimu. Fasiri kuwa ni elimumitindo ya kifasihi huja kwa kuwa nadharia hii inaangazia matini katika fasihi. Katika upande wa kiisimu nadharia hii huonekana katika kuchanganua maswala ya isimu. Kwa muhtasari elimumitindo ya fasihi na elimumitindo ya isimu hutegemeana na kukamilishana. Leech na Short (khj) katika uchunguzi wao wa kina wanasema uchunguzi wa kina wa matini za kifasihi kwa kuzingatia nadharia ya elimumitindo ni njia moja ya kuelewa na kuyaweka katika matumizi. Wanasema; kwa mhakiki kueleza jinsi athari fulani ilivyojitokeza, maana fulani hujitokeza kiisimu na kutufanya sio tu kuelewa vyema kilichoandikwa na msanii ila kukifurahia.

Ngara (1982:12) ametoa maelezo juu ya tofauti baina ya uhakiki wa elimumitindo na wa kawaida. Ngara anasema kuwa tofauti ya kwanza ni kuwa uhakiki wa kielimunitindo hutumia mbinu na maarifa ya kiisimu. Kwamba uchanganuzi huu huhusu jinsi lugha ilivyotumika, ambao ni uchanganuzi wa kiisimu. Kwa mfano dhana ya ukiukaji humaanisha uvunjaji wa kanuni za matumizi ya lugha katika viwango mbalimbali vya fonetiki, fonolojia na kadhalika. Pili, Ngara anasema, kuwa uhakiki wa kielimunitindo ni wa kitaratibu na una usahihi zaidi kuliko wa kikaida.

Kutokana na vipengele hivi viwili, dhana ya elimumitindo inahitaji uelewa wa jinsi fasihi inavyotumia lugha. Elimumitindo humtarajia mhakiki aelewe jinsi fasihi inavyotumia lugha kwa sababu lugha ya fasihi huchukuliwa kuwa ni tofauti na rejesta nyingine. Huwa ni jukumu la mhakiki kuifahamu vizuri rejesta hiyo. Kwa hivyo upekee unaojitokeza ni kuwa lugha ya fasihi, tofauti na matumizi ya lugha katika rejesta nyingine hutumika sio tu kuwasilisha mawazo bali pia kubuni sanaa. Hali hii ndiyo huifanya lugha ya fasihi kuwa na ukiukaji au ukiushi wa sheria za lugha mbali na lugha zingine. Katika mwelekeo huu lugha ya fasihi huangaliwa kama jaribio la kimakusudi la mtunzi kujiepusha na ukawaida kwani mwandishi hujaribu kutumia lugha kivyake.

Gray (1984:200) ana maoni kuwa elimumitindo ni uchanganuzi wa mitindo katika maandishi na mazungumzo kwa kutumia istilahi za kiisimu. Kwa jumla tunaweza kusema kuwa elimumitindo ni uchanganuzi wa mbinu zote za lugha ambazo zinatumiwa katika mawasiliano. Kwa hivyo elimumitindo inajumlisha mawasiliano ya kifasihi na mawasiliano yasiyokuwa ya kifasihi.

Indangasi (1988:10) ana maoni kuwa elimumitindo kama nadharia imesaidia kuelewa matumizi ya lugha katika kazi za kifasihi. Anaendelea kusema kuwa nadharia hii imeondoa utata uliokuwepo kati ya fani na maudhui.

Kwa mujibu wa maelezo ya Mbatiah (2001:77) tamathali za usemi ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika kiwango cha maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Ili kufafanua kauli hii ya

Mbatiah tunaweza kusema kuwa tamathali ya usemi ni fungu la maneno lililogeuzwa maana yake asili na kuwa na maana nyingine tofauti. Mifano ya tamathali za usemi ni: sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, oksimora, paradoksi jazanda na kadhalika. Kwa mfano katika matumizi ya sitiari; sifa ya kitu kimoja hupewa sifa za kitu kingine au kitu fulani husemwa kuwa kitu kingine. Kwa mfano: “Mwalimu mkuu wetu ni ngiri.”

Hapa sifa za ngiri zinapewa mwalimu mkuu. Tunajua ngiri ni mzoefu wa kusahau. Tafakari tunayopata ni kuwa hata umwambie jambo kwa wakati ufaao ili akufae kwa kukushughulikia haitawezekana na kwa hivyo huenda majukumu uliyotarajia kutimizwa yakacheleweshwa. Tamathali hii jinsi ilivyotumika inaleta taswira ya ngiri na taswira ya mwalimu mkuu kwa kuwa wamehusishwa kimuktadha.

Tuchukulie kwa mfano tukilinganisha mwewe na mwalimu mkuu. Mwewe mara nyingi humdhulumu kuku kwa kumpokonya vifaranga wake. Tukisema ‘mwalimu mkuu nimwewe’ basi tunaona taswira ya mwewe amnyakuavyo kifaranga licha ya kelele za kuku. Katika hali hii maudhui yanajitokeza kwani tabia za mwewe zinaonekana kwa mwalimu mkuu. Kwa hivyo lengo hasa la elimumitindo ni kueleza uhusiano uliopo baina ya lugha na majukumu ya kisanaa. Kwa hivyo mwandishi hutumia sheria za kiisimu ili kutimiza dhamira yake ingawa katika hali kiushi.

Wamitila (2003:39) ana maoni kuwa elimumitindo ni dhana inayotumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi na uchanganuzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi za kifasihi. Anasema ni taaluma iliyoko kati ya uchunguzi wa lugha na uchunguzi wa fasihi. Maelezo yake yanaoana na ya Leech na Short (1981) katika mchoro. Elimumitindo huhusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi fulani na zinazomtambulisha mwandishi anayehusika.

Wataalam mbalimbali wamezungumzia viwango mbalimbali vya uchanganuzi wa mtindo kwa kutumia nadharia ya elimumitindo. Wametaja vitengo mbalimbali kwa mfano kitengo cha lugha ambacho hushughulikia matumizi ya sentensi katika matini. Hiki ni kitengo cha sintaksia.

Habwe na Karanja (2003:125) wanasema sintaksia ni utanzu unaoshughulikia muundo wa sentensi na elementi nyingine zinazounda sentensi. Muundo wa sentensi hurejelea jinsi vipashio vyake huungana na kuhusiana ili kuunda sentensi zenye maana. Sentensi kwa hivyo ni kipashio kikubwa zaidi cha kimuundo chenye kuleta maana kamili. Miongoni mwa vipengele vinavyoshughulikiwa hapa ni: ukiushi katika mpangilio wa vipashio katika sentensi ambapo nomino, vitenzi, vielezi, viunganishi, vihusishi, uakifishi, sentensi fupi na sentensi ndefu hushughulikiwa kimaana.

Wamitila (2008:421) anasema kuwa msingi wa sitiari ni uhamishi wa maana. Ili uchunguzi wa sitiari ukamilike, sharti dhana tatu muhimu zichunguzwe. **Kilinganishi:** kile kinachotumiwa kama msingi wa kufananishwa; **kilinganishwa:** kile kinachofananishwa na msingi: **sifa** yenyewe ya ulinganishi. Anatoa mfano: '*Bakari ni fisi karamuni.*' Kilinganishi ni fisi, kilinganishwa ni Bakari na msingi ni sifa aliyonayo fisi – ulafi.

Katika kiwango cha kisemantiki lugha ya kitamathali ni miundo ya lugha ambayo ina sifa muhimu ya kuchunguza matini ya kifasihi kwa kutumia nadharia ya elimumitindo. Katika kutumia lugha maana huathirika. Ukiushi wa kiwango cha kisemantiki huhusu matumizi ya maneno kwa njia ambayo si ya kawaida maana za maneno hayo zinaporejelewa. Kwa mfano mbinu ya oksimora au tanakuzi katika vichwa vya kazi za sanaa. Riwaya ya K.W. Wamitila *Kiza Katika Nuru, Mbaya Wetu* ya Ken Walibora na kadhalika.

Elimumitindo haihusu tu uchanganuzi wa kimaandishi bali huhusu mazungumzo ya kifasihi au yasiyokuwa ya kifasihi. Pamoja na hayo, elimumitindo inaweza kuchukuliwa kama mojawapo au njia ya uchanganuzi wa kifasihi. Kwa hivyo dhana hii inapotumiwa, lengo kuu la uchanganuzi kama huu ni kubainisha uamilifu wa mbinu mbalimbali za lugha katika kufasiri matini za kifasihi. Matini ya kifasihi yanaweza kuchanganuliwa kwa kutumia utaratibu wa kielimunitindo ili kubainisha jinsi mbinu mbalimbali zilizotumiwa zinaleta athari ya kisanaa.

Baada ya kuiangalia historia ya elimumitindo, hebu sasa tudadisi jinsi tumeitumia nadharia hii. Kazi yetu imelenga ukiushi wa kisemantiki. Hiki ni kitengo mojawapo Leech na Short (1981) wameorodhesha kama mfano wa viwango vya uhakiki katika nadharia ya elimumitindo. Semantiki ni tawi la isimu ambalo hujishughulisha na uchambuzi wa lugha katika kiwango cha maana. Mwandishi anapoandika hukiuka matumizi ya lugha ya kawaida ili kuleta maana mbalimbali katika kazi yake. Katika kazi yetu tumelenga tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashihisi, tashbihi, kejeli, tanakuzi na oksimora katika ukiushi wao ili kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui.

1.7.8 Mihimili ya Nadharia Hii.

Nadharia hii ina mapendeleo ya mhakiki kutoa maelezo kwa kina kuhusiana na jinsi maneno mahususi yalivyotumika kimuktadha katika matini za kifasihi na wala haina mipaka ya kufungia kwa kijikita katika mielekeo fulani. Aidha, nadharia hii haingiliani na nadharia zingine kwani inasimama kivyake kiuchanganuzi bila kuathiri nadharia zingine kwa mfano umarksi, ufeministi na umiundo. Kwa upande mwingine, nadharia hii inashikilia kuwa uchunguzi wa matini kwa kuangalia vipengele mbalimbali hukuza mawanda mbalimbali ya kielimu haswa yale ambayo huwa yamepuuzwa. Vilevile, ina mawanda mapana ya kushughulikiwa kwani ina viwango mbalimbali kwa mfano: kiwango cha semantiki, kiwango cha grafolojia, kiwango cha sintaksia, na vinginevyo. Viwango hivi hutoa mtazamo mpana wa kushughulikia matini. Nadharia hii hailengi matini za kifasihi tu, bali hotuba za kisiasa na matangazo ya biashara. Haijifungii kwenye matini ya fasihi tuu.

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusiana na Mada

Kitsao (1975) katika kazi yake “A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts”, amefafanua dhana ya elimumitindo na mtindo. Katika tasnifu hii ya uzamili, Kitsao amefafanua viwango vya kuchanganulia dhana za mtindo katika matini kwa kulenga riwaya. Ametaja viwango vya msamiati, grafolojia, sintaksia, semantiki na vingenevyo vingi. Vilevile ameonyesha jinsi mtindo hujitokeza katika matini za kifasihi. Ingawa Kitsao alishughulikia riwaya, maelezo yake yametufaa kwani miongoni mwa vipengele alivyoshughulikia ni tamathali za usemi mbalimbali.

Vilevile kuna maelezo kuhusu ukiushi katika kiwango cha kisemantiki ambacho tumekishugulikia katika ukiushi wake tukilenga tamathali za usemi.

Leech na Short (1981) katika kitabu chao *Style in Fiction*, wameshughulikia mtindo. Wamejadili nadharia ya elimumitindo kwa kina. Katika kazi yao wana maoni kuwa mtindo na maudhui huhusiana. Kazi yao pia imeanisha viwango vya kuchanganua mtindo ambavyo ni kiwango cha msamiati, grafolojia, semantiki, sintaksia na fonolojia. Katika utafiti wetu tumelenga kiwango cha kisemantiki kwani tunaangalia maana zinazojitokeza katika tamathali za usemi na jinsi maana hizo zinachangia katika kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui katika tamthilia tulizoteua hapo juu. Maelezo ya Leech na Short haswa katika kipengele cha ukiushi katika kiwango cha semantiki yametufaa kwani swala letu la utafiti limelenga hapo kwa kuzingatia tamathali za usemi za chuku, sitiari, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora.

Indangasi (1988) katika kitabu chake *Stylistics*, alizungumzia nadharia ya elimumitindo. Amezungumzia historia ya nadharia hii na viwango mbalimbali vya kuchunguza mtindo. Amezungumzia viwango vya fonolojia, sintaksia, msamiati, semantiki, na tamathali za usemi. Mada yetu inalenga tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, tanakuzi na oksimora katika matini tulizotaja hapo juu. Kazi ya Indangasi imetufaa kwa kuwa amefafanua kipengele cha ukiushi wa kisemantiki kwa kulenga tamathali za usemi kwa kina ingawa alilenga kazi tofauti; riwaya. Kazi yetu italenga tamthilia za *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*.

Mohamed (1995) katika kitabu chake '*Kunga za Nathari: Riwaya, Tamthilia na HadithiFupi*', amefafanua maana ya mtindo na kuangalia dhana mbalimbali za mtindo. Anasema mtindo ni nyenzo ambayo hufumbata wazo kuu. Bila shaka wazo kuu ni dhamira ya mwandisi ambayo huwa ujumbe. Vilevile anasema mtindo waweza kuangaliwa kama mtu mwenyewe, jumla ya tabia za lugha za kikundi cha waandishi au wakati fulani na vilevile anasema mtindo waweza kuchukuliwa kama kuukimbia ukawaida. Maoni yake Mohamed kuhusu mtindo ni muhimu kwetu kwani yametufaa katika kuchanganua dhana ya mtindo hasa tukijikita katika matumizi ya kipengele cha

tamathali za usemi tukizungumzia sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora katika tamthilia za *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*. Maelezo ya Mohamed yamefafanua kiasi cha haja mtindo kama kuukimbia ukawaida haswa kipengele cha kisemantiki kwani katika hali hii maana tofauti hujitokeza na kwa hivyo kuibua maana kimuktadha.

Mbatiah (2000) amegusia swala la mtindo katika hadithi fupi. Mbatiah alihariri diwani ya *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*. Katika uhariri wake amegusia mtindo katika hadithi fupi. Amefafanua dhana ya mtindo. Katika kazi hii ameonyesha kuwa mtindo na maudhui huhusiana. Kazi ya Mbatiah ilijikita katika hadithi fupi. Ingawa mada yetu inachunguza tamthilia, maelezo yake yametufaa kwani yana ufafanuzi mzuri ambao umetuelekeza kuelewa dhana ya mtindo hasa vipengele vya tamathali za usemi.

Wales (2001) katika kitabu chake *A Dictionary of Stylistics* ana maelezo kuhusu mtindo na elimumitindo. Kazi yake ina ufafanuzi wa tamathali nyingi za usemi. Kamusi hii imetufaa kwani imetwezesha kurejelea dhana mbalimbali kuhusiana na mtindo. Katika kazi yetu tumejifunga katika matumizi ya lugha, kipengele cha tamathali za usemi hususan sitiari, chuku, tashihisi, tashbihi, kejeli, tanakuzi na oksimora katika tamthilia tulizotaja.

Barry (2002) katika kitabu chake *An Introduction to Literary and Cultural Theory* ametoa ufafanuzi wa kina kuhusu elimumitindo. Katika ufafanuzi wake, Barry anazungumzia mihimili ya elimumitindo. Amejadili kuhusu umuhimu wa nadharia hii katika kuhakiki matini za kifasihi. Ametoa hoja tatu kuhusiana na nadharia hii zikiwa ni: elimumitindo husisitiza mwingiliano kati ya lugha ya kifasihi na lugha ya kawaida ya matumizi ya kila siku, jingine ni kuwa nadharia ya elimumitindo huhakiki matini kwa kuzingatia utaratibu wa kisayansi wa isimu na mwisho ni kuwa elimumitindo hufuata mikakati ya kisayansi katika kujaribu kufafanua usemi. Kazi hii imetufaa kwani kutokana nayo tumepata mihimili ya nadharia hii na jinsi wanaelimumitindo hushughulikia matini za kifasihi kwa kuzingatia nadharia hii.

Ongarora (2007) alihakiki mtindo katika *Harusi ya Buldoza* kwa kutumia nadharia ya elimumitindo. Katika kazi yake Ongarora alishughulikia ukiushi mbalimbali kwa mfano ukiushi wa kisintaksia, ukiushi wa kisemantiki, ukiushi wa kimsamiati na kadhalika. Utafiti huu utatufaa kwa kuwa kipengele cha matumizi ya lugha hususan tamathali za usemi kiukiushi alichoshughulikia kimetupa mwongozo. Vilevile alitumia nadharia ya elimumitindo katika kuthibitisha kuwa kuna ukiushi wa viwango mbalimbali katika matini alizochanganua. Hata hivyo kazi yetu na yake ni tofauti kwani sisi tumepiga hatua ya kujaribu kujaza pengo kwa kushughulikia kazi za tamthilia tofauti na yeye na kuona jinsi maudhui yamewasilishwa kutokana na ukiushi huu.

Lugwiri (2011) alitumia uhakiki wa elimumitindo katika tasnifu yake. Lugwiri alichanganua sitiari, tashbihi na taashira katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*. Amebainisha wazi wazi jinsi vipengele vya tamathali za usemi vinabainika katika utenzi husika. Katika maelezo yake, Lugwiri ameonyesha kuwa tamathali za usemi husaidia katika kuibua maudhui, kuyaendeleza na kuyawasilisha. Utafiti wetu ni tofauti na wake kwani tumelenga mtindo vilevile ila tumejikita katika tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora. Kazi hii itatufaa kwani ina maelezo ya kutufaa kuhusu nadharia ya elimumitindo na ufafanuzi kuhusu dhana ya mtindo kwa jumla.

Murumba (2013) alitafiti mtindo katika *Watu wa Gehenna* (1997). Katika utafiti wake alitumia nadharia ya elimumitindo na kubainisha jinsi vipengele vya mtindo vimetumika katika matini hiyo na jinsi vimeathiri muundo. Katika utafiti wake alionyesha jinsi maana tofauti hujitokeza katika ukiushi wa kisemantiki. Vilevile alitafiti kipengele cha uhusika na wahusika na jinsi wanavyochangia katika ukuzaji wa maudhui. Utafiti wetu unahusu mtindo tukilenga kipengele cha tamathali za usemi katika tamthilia za *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka*. Tunalenga kutumia nadharia ya elimumitindo. Kwa hivyo utafiti wake Murumba umetufaa sana kwani ameifafanua dhana ya viwango vya elimumitindo na kwa hivyo kutupa mwelekeo haswa katika kipengele cha ukiushi wa kisemantiki.

Katutu (2013) alishughulikia mtindo katika Diwani ya *Mfuko na Hadithi Nyingine*. Ameshughulikia mtindo unavyoendeleza maudhui katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* (2005). Katutu ametumia nadharia ya elimumitindo na kwa hali hiyo tumefaidi katika kuelewa vipengele muhimu vya nadharia hii na jinsi vimetumika katika kutafitia mada yake.

1.9 Mbinu za Utafiti

Katika utafiti huwa kuna mbinu nyingi ambazo hutegemea aina na malengo ya utafiti. Ili kufanikisha utafiti wetu, tumezisoma tamthilia tulizoziteua na kuvipa vipengele vya kimtindo uchanganuzi wa kina kwa kujikita katika tamathali za usemi. Kusoma huku kumetufaa kwa kuwa tumepata maelezo na mifano ya tamathali za usemi tulizoteua kuzishughulikia. Tumedurusu vitabu, makala na hata tasnifu zilizoandikwa kuhusu mada na nyingine zitufaa maktabani kwa lengo la kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada tuliyoiteua. Maoni ya wasomi wa kutajika pia yametufaa kwani tumehojiana nao ana kwa ana haswa kuhusu nadharia ya elimumitindo na maswala kuhusu dhana ya mtindo na jinsi dhana hizi hujengana ili kuibua na kuwasilisha maudhui. Hata hivyo utafiti huu ni wa maktabani. Mwisho mtandao utatufaa katika kupata makala mbalimbli kuhusu mada hasa nadharia tunayoitumia.

SURA YA PILI
UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA ZINGUO LA MZUKA.

2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumechunguza ukiushi wa kisemantiki katika tamthilia ya *Zinguo la Mzuka*. Tamathali za kiwango hiki ambazo tumechanganua ni: sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, oksimora na tanakuzi. Tamthilia ya *Zinguo la Mzuka* inaangazia uongozi katika nchi ya Kusinyika pamoja na athari za mkoloni kwa viongozi waliochukua hatamu za uongozi punde tu baada ya uhuru na hata miaka mingi baadaye. Ujumbe tunaoupata katika kazi hii ni kwamba Mwafrika ambaye alikubali kutawaliwa kwa muda mrefu na mkoloni, kamwe hawezi kutupilia mbali amana ambayo alikabidhiwa na hao waliomtawala. Ukoloni mamboleo bado umeendelea kutawala maisha ya mtu yeyote aliyewahi kutawaliwa na mkoloni. Zinguo; ambaye alichukua hatamu za uongozi kutoka kwa mkoloni(Mzuka), anashindwa na changamoto za kuiongoza Kusinyika. Hali hii inaitumbukiza Kusinyika katika njaa, umasikini na ufisadi. Hali inayopingwa na Mtu 1 na Mtu 2. Wanaharakati hawa wanawafungua Wakusinyika macho na kuwafanya kuanza kupigania haki zao. Kupitia maridhiano yanayoongozwa na Mzee, Kusinyika inapata mwelekeo na kuwa nchi inayozalisha mali na iliyostawi. Vitendo katika tamthilia hii vinadhihirisha ukweli kwamba ingawa nchi za Afrika ziko huru, hazina uwezo wa kujinasua kutoka kwapa za utamaduni wa mkoloni. Tamthilia hii imetumia tamathali za usemi kama vile sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, oksimora na tanakuzi kuibua na kuendeleza maudhui.

Katika sura hii tumechanganua jinsi tamathali za usemi tulizotaja hapo juu zilivyochangia kiukiushi katika kuibua na kuendeleza maudhui katika tamthilia ya *Zinguo la Mzuka*. Kwa hivyo tumezitambua tamathali hizi na kuchanganua maana ya maneno inayojitokeza katika ulimwengu halisi na maana kiushi katika ulimwengu dhahania ambao unategemea muktadha katika matini. Miongoni mwa maudhui yaliyojitokeza ni ukoloni mambo leo, utegemezi, maridhiano, uongozi mbaya, ufisadi, ubinafsi, swala la malezi ya mtoto, taasubi ya kiume, upotovu wa vijana, nafasi ya mwanamke katika jamii ukabila na umoja. Tumeonyesha jinsi tamathali tulizoteua zilivyochangia katika kuibuka, kuendeleza na kisha kuwasilisha maudhui tuliyoorodhesha hapo juu.

Tamthilia tunayochanganua inaonyesha hali halisi ya maisha ya bara la Afrika linalojidai kuwa huru kwa miaka arubaini na zaidi na jinsi viongozi wake wanavyohusiana na watawaliwa pamoja na mkoloni au mataifa yenye nguvu. Tamthilia hii kwa hivyo inamsuta Zinguo ambaye ni mnafiki, dhalimu, mwenye tamaa na mbinafsi. Hata hivyo jamii hii ya Kusinyika inao watetezi wa kweli ambao wanaipa Kusinyika mwelekeo. Haya yote tumeyafasiri kutokana na ukiushi wa kisemantiki ulioko katika tamathali za usemi tulizoteua na kuzichanganua.


2.1 Sitiari

Wamitila (2008:420) ana maoni kuwa sitiari hueleweka inapoelezwa kwa mtazamo wa kilinganishi, kilinganishwa na msingi. Kilinganishi ni kile kinachotumiwa kama msingi wa kufananisha, kilinganishwa ni kile kinachofananishwa na msingi ni ile sifa yenyewe ya ulinganishi.

Kuhenga (1977) na Wamitila (2008) wana maoni kuwa sitiari haitumii maneno ya mlinganisho kama: kama, mfano wa, tamthili ya, ja na kama vile. Wamitila na Kuhenga wanatoa maoni yao kwa mtaalamu Leech (1969) anayesema kuwa sitiari huhusishwa na sheria mahususi ya uhamisho inayosema **A** ni **B** ikiwa na maana kuwa **A** ina tabia au sifa za **B** ingawa **A** na **B** ni vitu viwili tofauti, huwa kuna uhusiano fulani kati yavyo unaovifanya vihusishwe. Uhamishaji wa maana unatokana na uwezo wa msemaji wa kulinganisha mambo tofautitofauti maishani. Sitiari kwa hivyo huwa na nyuso mbili, uso mmoja ni ule wenye maana iliyo wazi na mwingine ni wa maana fiche. Maoni haya yanalingana na ya Mohamed (1995), Kuhenga (1977) na Mutiso (2005).

Maoni ya Walpole (1941) yanatufaa. Anasema sitiari ni kuazima jina la kitu kingine. Walpole anasema: katika usemi wenye sitiari, ishara hurushwa kutoka muktadha mmoja kwenda mwingine ulio tofauti kabisa lakini katika msingi wa kumithilisha vipengele vilivyomo katika miktadha miwili.

Walpole alitoa mchoro ufuatao kufafanua wazo hili.



- T ----- muktadha
- P ----- msemaji au mwandishi
- L ----- sitiari
- C ----- wasikilizaji au wasomaji

Kielelezo 1: mchoro wa nadharia ya Walpole ya uhamishaji maana.

Mchoro huu unaonyesha namna matumizi ya sitiari yanavyomithilisha miktadha miwili iliyotofauti katika usemi ambao ni sitiari. Mchoro unathibitisha kwamba wahusika upande wa **A** wanalingana na wahusika upande wa **B** kwa kutegemea nguvu za mfanano. Kwa hivyo, msemaji **P** katika **A** anatumia ishara ya lugha **L** katika muktadha **T** kupokelewa katika **B(C)**. Mishale katika pembetatu inathibitisha kwamba kuna mawasiliano kamili baina ya **(C)** na **(P)**. Kwa mfano katika usemi ‘Zinguo ni mwokozi wa watu wake!’ Kuna maana iliyo wazi na maana ya kimapumbo. Maana iliyo wazi ni kwamba Zinguo ana uwezo wa kuwatoa watu katika shida au hatari. Kwa hivyo ili uwe salama lazima uwe karibu na mwokozi ambaye ni Zinguo. Lakini tukifuata maana iliyotolewa kisitiari, mfasiri anaweza kupata mifano ya falsafa ya maisha chungu nzima; ambayo haioani na muktadha wa matini. Zinguo ana hekima na busara ya kuwaongoza Wanakusinyika kujiendeshea, kujiendeleza na kujinasua katika dhiki za umasikini kwa kuwajengea miundomsingi ya kuifanya nchi kuwa na pato na kupiga teke hali ya utegemezi.

Hebu tujaribu kutathmini sitiari kwenye usemi ufuatao:

Mweusi: Nenda! Nitakuzingua ujue mimi ni bingwa wa kuzingua mizuka wazugao watu. (uk 7)

Mweusi ametumia sitiari katika usemi wake. Sitiari hii tumeitambulisha kwa mkolezo kama ilivyo hapo juu. Kwa kufuata mtazamo wa Walpole (khj) tunamwona Zinguo akijiondoa katika hali ya kuwa Mkusinyika wa kawaida na kuvaa vazi la bingwa ili kujaribu kuitetea Kusinyika kutokana na dhiki ya ukandamizwaji waliyomo.

Matumizi ya kauli ‘mimi ni bingwa’ katika ulimwengu halisi, ‘mimi’ ni kiwakilishi cha nafsi ya kwanza katika umoja. Anayerejelewa na kiwakilishi hiki ni Zinguo (Mweusi). Maana yake haijitokezi sawasawa kwa kuyasoma maneno haya tu kwani haya ni matumizi katika ulimwengu halisi. Katika hali hii maana iliyosimbwa katika maneno imekiukwa. Hatuelewi ni bingwa wa nini. Tunaweza kukata kauli kuwa Mweusi anaposema kuwa yeye ni bingwa anajipa sifa za mtu aliyebobea katika ujuzi au taaluma fulani, hodari, stadi, fundi au galacha. Kawaida bingwa huwa ni mshindi, mwenye ujasiri na mwenye kujiamini na juu ya yote huwa na lengo fulani ambalo mara nyingi huleta ushindi. Tunaposoma matini, tunahamisha sifa za bingwa na kumpa Mweusi kulingana na muktadha wa matumizi ya kauli hii. Mweusi anajitaja kuwa yeye ni bingwa. Kauli hii inatumiwa na Mweusi baada ya Mweupe kumtishia kumwekea vikwazo vya kutoenda ng’ambo. Mweupe ana orodha ya vikwazo atakavyotimiza. Anataja kukatiza utoaji wa lawalawa na sharubati na biskuti, akili na maarifa pamoja na kuwazuia Wakusinyika wenzake kutoenda ng’ambo ambao vilevile anatishia kufungia bidhaa zinazotoka Kusinyika zisiuzwe nchi za nje. Bila shaka lawalawa, biskuti na sharubati ni maneno ambayo hayasimamii bidhaa zilizotajwa moja kwa moja. Maneno haya yanawakilisha misaada anayotoa Mzuka kwa nchi ya Kusinyika. Pamoja na hayo, Mzuka anaendelea kuitawala Kusinyika hata akiwa Umizukani. Zinguo haipendi hali hii na kwa hivyo anataka kumwondoa kabisa. Hali hii ndiyo inayomfanya Mweusi kujitia ujasiri kiwango cha kujipumbaza kuwa anaweza hata bila usaidizi wa Mweupe. Mweusi anakasirishwa na tabia hii ya Mzuka ya kupenda kuingilia maswala ya ndani ya Wakusinyika. Katika hali kiushi tunaona kuwa baada ya Mwafrika kupewa uhuru, haikuchukua muda mrefu kwa raia na viongozi Waafrika kugundua kuwa walipewa uhuru bandia. Walipogundua haya

walilalamika ingawa hawakujua la kufanya katika madaraka hayo mapya. Mkoloni kwa hivyo alikuwa amewarubuni na ni kweli kuwa hakuondoka. Elimu yake ilizidi kudhihirika katika mifumo ya uongozi wa Waafrika. Hali hii iliwaudhi viongozi Waafrika na hawakuwa na la kufanya ila kuendelea kujitahidi kuimarisha uhuru waliokuwa nao. Zinguo anapotumia kauli hii anajiona kuwa yumo katika nafasi ya uongozi na kwa hivyo ana nyenzo za kuweza kumzuia Mzuka kuingilia maswala ya Kusinyika. Ili kutimiza haya, anahitaji ujuzi maalum wa kutumia na ujuzi huu anaupata tu kwa kujihusisha na bingwa katika ulimwengu halisi. Hata hivyo, Mweusi anapotamka kauli hii inastaajabisha kwani hata yeye mwenyewe hajiamini. Mweusi anamwona Mweupe kama bwana wake ambaye hawezi kumpinga. Huu ni unafiki wa kiongozi Mweusi aliyejisifu kuwa alimfahamu Mweupe na sifa zake zote ila anaendelea kusalitika na hila za mkoloni na hata kuendelea kutimiza utashi wa mkoloni. Ndipo Mweupe anasema: ‘alienda mwili tu na roho yake ingalipo na kwamba anaishi ndani ya Mweusi’.

(uk 6)

Hali hii Mweusi haipendi ingawa anajua kuwa ni lazima amtegemee Mzuka (Mweupe) katika maarifa ya kuiendesha nchi. Sitiari hii inaibua maudhui ya unafiki kwani katika ubingwa huu hatuoni ubingwa wowote ila udhihirishaji wa kutokuwa na uwezo na ujuzi wa kuiendesha Kusinyika. Sitiari hii vilevile inaendeleza maudhui ya utegemezi kwani baada ya mkoloni kuondoka, viongozi Waafrika walioshika hatamu walisahau malengo yaliyowapelekea kupigania uhuru na kuendelea kutegemea wakoloni waliozidi kuwakandamiza na hata kuwafanya waonekane punguani katika mipango na mikakati ya kuiendesha na kuiendeleza nchi waliyorithi kutoka mikononi mwa wakoloni. Kwa hivyo usaliti unaojitokeza hapa ni usaliti wa kisiasa. Zinguo kama kiongozi wa Kusinyika anajipa moyo tu kwa kujiita bingwa lakini ukweli ni kwamba katika kujaribu kutimiza matakwa ya Mzuka, anashiriki katika mikakati ya kuitumbukiza nchi ya Kusinyika katika mashaka na misukosuko ambayo mwishowe inaisambaratisha nchi. Vyote hivi kwa sababu ya maslahi yake ya kibinafsi. Kwa hivyo tunaona kuwa, mataifa yaliyotawaliwa yalipigania uhuru wa kujitawala na kwa hivyo wakoloni wakang’olewa. Lakini uhuru walioutoa wakoloni kwa mataifa waliyotawala haukuwa wa kweli kwa sababu bado wakoloni walikuwa na njia nyinginezo za kuathiri na kuongoza matukio ya kisiasa na

hasa ya kuumiliki uchumi wa mataifa hayo. Hali hii inamfanya Zinguo kuwa na matamano ya kumwondoa mkoloni.

Kauli tuliyoinkuu hapo chini ni sitiari. Kauli hii ni usemi wa Zinguo anapomrejelea Mzuka ambaye licha ya kuondoka, ana hila za kuendelea kuinyonya Kusinyika kwa kutumia nguvu. Kwa hivyo, Mzuka, ambaye ni binadamu amepewa sifa za jini. Huu ni uhamisho wa sifa za kitu kimoja kuchukuliwa na kingine.

Hebu tutathmini kauli hii:

Toka! Jini mwiba mali yetu. (uk 12)

Zinguo (Mweusi) anamkemea Mzuka (Mweupe) kwa kumwita ‘zimwi mla watoto na jini mwiba mali ya Kusinyika’. Katika muktadha huu Mzuka ambaye ni mkoloni anapewa jina ‘zimwi’. Miongoni mwa sifa za zimwi ni: kiumbe anayeishi mwtuni na anayeweza kujibadilisha katika hali mbalimbali na huweza pia kudhuru. Katika matumizi ya kawaida ya maneno haya, sifa hizi kama vile kudhuru huhusishwa na dhulma dhidi ya wanyonge. Sifa hizi za kudhuru ni kama vile sifa za mkoloni za ubinafsi, kujitakia makuu, kukandamiza, wizi wa mali ya umma na hata kuuu. Fasili ya maneno haya katika hali dhahania ni kuwa Mzuka ambaye ni mkoloni hana nia njema kwa Kusinyika. Kwa kutaja haya tunaona kuwa nafsi ya Mzuka (Mweupe) ni uchoyo, ufiadi, wizi wa mali ya umma ili kujilimbikizia mtu binafsi, kujitakia makuu na kutojali masilahi ya wengine. Hila zake mbaya zinaleta maafa katika Kusinyika kwani watoto hawapati elimu, wanakufa kwa njaa na vilevile kitendo chake cha kuiwekea Kusinyika vikwazo mbalimbali ni ishara kuwa haijali Kusinyika na kwa hivyo kuitumbukiza Kusinyika katika umaskini. Zingua vilevile anamwita Mzuka ‘jini’. Hali hii inamfanya Mzuka kuwa nguvu nzito na kwa hivyo anaweza kufanya jambo lolote lile analotaka kulifanya pasipo pingamizi yoyote. Anaweza kujigeuza sura na hali yake jinsi apendavyo. Hali hii ni ishara kuwa Mzuka si mshirika wa Kusinyika wa kuaminika kwani sifa hizi za kuwa na uwezo wa kubadilikabadilika kama kinyonga ni hatari kwa mshirika wake ambaye ni Kusinyika. Haya yote yanatokana na hali ya juu ambayo amejuwekea Mzuka. Hivyo basi, vitisho vya Mzuka vya kuiwekea Kusinyika vikwazo ni ishara ya kutumia nguvu za kumfanya Zinguo amtii ikiwa anataka azidi kuwepo uongozini. Vitisho hivi vinaleta utiifu mkubwa kwa sababu ya uoga mkubwa alionao anayetishwa. Kwa hivyo Zinguo anaropokwa haya

baada ya kuonyeshwa yale yatakayomsibu ikiwa hatatii amri za Mzuka. Kwa hivyo Zinguo anamwita Mzuka ‘jini mwiba mali yetu’ kwa kuwa, wakati wakoloni walipofika katika bara la Afrika walijifanya marafiki wa watu weusi. Waliwalaghai Waafrika kwa kutumia mbinu na nyanja mbalimbali. Kwa mfano tunafahamu jinsi Biblia ilivyotumiwa ili kulainisha nyoyo za watu weusi. Baada ya watu weusi kukubali ulaghai wa wakoloni tunafahamu matokeo mabaya yaliyomkumba Mwafrika. Kwa mfano ardhi yake ilitakwa na Waafrika kufanywa maskwota. Hali iliyowatumbukiza wenyeji katika umaskini. Dhana ya umaskini ni ngumu kufasiriwa ingawa ni mojawapo ya maudhui yanayojitokeza kutokana na kauli hii ya Zinguo. Umaskini ni hali ya ukosefu wa pato na hasa kutokuwa na njia za kujikimu katika kupata mahitaji ya kimsingi ya maisha kama vile chakula, mavazi, makazi, elimu na hata huduma za afya. Haya yote ni haki ya kimsingi ya binadamu. Hali hii tunaiona Kusinyika na kisababishi chake ni Mkoloni.

Hata hivyo, kwa sababu ya uwezo wa kutafakari, ni kweli kwamba, Mwafrika hangeendelea kutawaliwa na mkoloni. Mwafrika anaamka na kujitetea ili kujiondoa katika dhulma hizi za mkoloni za kumnyima haki zake za kimsingi. Hali anayodhihirisha Zinguo kwa kumwita Mkoloni kwa majina haya yanayodhihirisha ukandamizaji. Sitiari iliyotumika hapa inamwonyesha Zinguo kumwita Mzuka kwa majina ya viumbe waovu wenye nia mbaya. Tunamwona Zinguo akijipurukusha kuikata minyororo iliyomfunga shemere.

Anajisuta na kutaka kujua sababu ambazo zinamfanya kutumikishwa. Kwa hivyo sitiari hii inadhihirisha kuwa Zinguo ametambua ulaghai wa Mzuka na amekata shauri kupigania haki yake. Hataki kunyanyaswa tena. Ameona ni bora kujiondoa katika ukoloni mamboleo.

Kwa kurejelea mtazamo wa Walpole, tunapata ufasiri wa sitiari tuliyoitambulisha hapo chini katika usemi wa Zinguo kwa kuhamisha sifa za shujaa na kumpa Zinguo.

Zinguo: Vinataka shujaa.
Nimpige mieleka Mzuka mkiona kwa macho yenu.
Mkiona!
Zinguo shujaa! (uk 13)

Katika kauli vinataka shujaa, maana yake haijitokezi katika ulimwengu halisi wa matumizi ya maneno haya. Katika kauli hii tunamwona Zinguo akibadilishwa na kuvishwa vazi la shujaa. Hatumwoni Zinguo kama Zinguo, tunamwona akijitaja kama shujaa. Miongoni mwa sifa za shujaa ni: ujasiri, nguvu, miujiza na kadhalika. Tunaona kuwa Zinguo ni mshindi lakini hatujui ni ushindi wa nini. Lakini katika maana kiushi kimuktadha, mazungumzo haya yanaonyesha Zinguo akijaribu kupigania haki yake kwani ulevi wa kupata uhuru ulikuwa umemwondoka kichwani. Kwa hivyo kama kiongozi ametanabahi na kwa hivyo anatilia shaka uhuru aliopewa na mkoloni. Amechoka na hila za mkoloni na amejitolea mhanga kuwaongoza wenzake katika safari ya kuulinda uhuru wao, kwani uhuru waliopewa ulikuwa na athari kubwa za ukoloni mamboleo. Kwa hivyo anaupiga vita ukoloni mamboleo.

Katika kauli hii yenye sitiari tunatambua kuwa ukoloni mamboleo ulikuwa na athari kwa mataifa yaliyokuwa mbali na nchi za wakoloni. Kwa hivyo kauli hii ya Zinguo inathibitisha kuwa kupambana na athari za ukoloni mamboleo si kazi rahisi. Ni kazi inayohitaji shujaa. Kwa kuuhusisha usemi huu na muktadha, nchi ya Kusinyika ilikuwa imepewa uhuru wa bendera tu. Ndiyo, Kusinyika ina uhuru, lakini uhuru uliojaa athari za kikoloni. Kwa mfano wana wimbo wa taifa. Ishara ya kuwa huru. Lakini viungo muhimu vya mfumo wa siasa kama vile sheria, katiba, mahakama, bunge na hasa maongozi yenyewe bado yanafuata yale yaliyorithiwa kutokana na mfumo wa kikoloni.

Mzuka mwenyewe anakiri kuwa hayo madhabahu ayachezeayo Zinguo aliyapanga yeye; Mzuka. Licha ya hayo, Zinguo hataki kuonyesha kushindwa. Hapendezwi na athari za Mzuka lakini inambidi ashirikiane naye hata kwa kutopenda. Katika hali hii tumechukulia uhuru kuwa uwezo wa nchi kujiendeshea ushauri wake yenyewe kwa kujitegemea katika uamuzi wa mambo muhimu ya kujistawisha na uzalishaji mali. Hali hii ya Zinguo kuwa na madai haya inatilia shaka uwezo wa Kusinyika kujitawala kikamilifu. Kwa mfano Wakenya wanapopigania katiba mpya wanapendekeza mfumo wa katiba za mabwana zao; mfano utolewe kutoka mataifa hayo ili kuwe na mfumo kama wao ingawa hatuko tayari kumudu mahitaji ya makadirio ya fedha kuendesha majukumu katika katiba hiyo.

Vilevile miaka mingi baada ya uhuru inatufanya kuwa na tajiriba ya udhaifu anaotuvuta nyuma kimaendeleo na kwa hivyo masumbuko haya yanafaa kuwa funzo tosha la kutufanya kuketi na kuwa na mfumo wetu binafsi wa kushughulikia matatizo yetu. Baada ya mkoloni kuutoa uhuru, viongozi wa Kiafrika walipapia nyadhifa za uongozi. Walikosa uwezo wa kuviendesha vyeo hivyo na kwa hivyo wakashindwa. Kwa hivyo wakaanza kusingizia wakoloni. Kauli hii kwa hivyo inazindua dhana ya uhuru na maana yake na namna Waafrika walivyo chukulia uhuru kuwa. Hata baada ya mkoloni kuondoka athari zake zilibakia katika utamaduni wa mtawaliwa. Tunaona maudhui ya unafiki yakiendelezwa hapa kutokana na ukosefu wa kuona sifa za kishujaa katika matendo ya Zinguo isipokuwa utegemezi. Kwa hivyo Zinguo ni shujaa tu kwa Wakusinyika ilhali ameshindwa kujiondoa katika minyororo ya kikoloni.

Katika kiwango hiki tunaendelea kuchanganua sitiari kwa kurejelea uhamishaji wa kitu kimoja kuwa kingine kwa kuzingatia sifa zao na jinsi sifa hizo zinavyohusiana. Katika usemi wa Zinguo kuna matumizi ya neno *dude* ambalo lina maana maalum. Ufasiri wa maana hii unajitokeza tu kwa kuzingatia muktadha wa matumizi yake. Hebu tutathmini kauli hii:

Zinguo: Na nyinyi mbona hamkulipiga hili dude?
Nyinyimsipolipiga haliendi! (uk 14)

Neno '*dude*' lina maana ya kitu kikubwa kisichojulikana. Dubwana. Huu ni ufasiri katika ulimwengu halisi. Katika hali dhahania ambayo ni ufasiri kimuktadha na vilevile kiukiushi katika matini tunaona hofu aliyonayo Zinguo katika kukabiliana na Mzuka ambaye anazijua athari zake. Zinguo anaogopa nguvu za mkoloni ndiposa anapokabiliana naye analiita *dude*. Mzuka ana mbinu za kumkabili Zinguo asizozielewa Zinguo. Kwa hivyo Zinguo anaamini kuwa mawazo, mbinu na ujuzi alionao Mzuka ni wa hali ya juu na kwa hivyo si rahisi kukabiliana naye. Kwa hivyo sitiari hii inaonyesha kuwa Mzuka ana sifa hizi za *dude* za kuwa katika hali ya kutoeleweka. Hii ndiyo sababu Zinguo anamithilisha na *dude*. Kwa hivyo tunapata fasili kuwa Zinguo ameshindwa kumkabili Mzuka kutokana na njama zake.

Sauti inaposema ‘ni wewe mzinguaji’ kauli hii inaibua sitiari. Tafakuri tunayopata hapa ni kuwa Zinguo ni mbinafsi na hajatoa nafasi kwa Wakusinyika kusaidia kupiga vita matamano ya Mzuka ambaye licha ya kuipa Kusinyika uhuru, hajaondoka kabisa. Kwa hivyo wakusinyika wamempa Zinguo sifa za mzinguaji lakini si kwa hiari kwani Zinguo amewatenga. Tukiitathmini kauli hii katika ukiushi wake ni kuwa Wakoloni walipogundua kuwa Waafrika walikuwa wanataka uhuru wao, walimpa Mwafrika elimu iliyomfanya kudumisha utamaduni wa kimizuka kwani walitaka kudumisha na kulinda masilahi yao katika mataifa haya. Miongoni mwa utamaduni huo kulikuwa na udikteta na ubinafsi. Hali hii tunaiona kwani Zinguo amerithi utamaduni wa Kimizuka ishara kwamba licha ya kupewa uhuru ameshindwa kujinasua katika kwapa za utamaduni wa Kimizuka. Mukadha wa matumizi ya sitiari hii unaibua maudhui ya ukoloni mamboleo kwani usemi wa sauti unaonyesha kwamba Zinguo anayejidai kuwa mzinguaji amekataa kuwashirikisha Wakusinyika katika utawala wa nchi. Anapenda udikteta na ubinafsi kwani anaamua kila kitu. Haya vilevile ni maudhui mengine yanayoibuka. Tunamwona Zinguo akiwa na haja ya kutaka kuidhibiti Kusinyika na vilevile kuimiliki huku Wakusinyika wakibakia nyuma bila kushirikishwa.

Katika kauli ya Zinguo tunayoitathmini hapa chini kuna sitiari. Sitiari hii tumeitambulisha kwa kuitilia mkolezo. Katika kauli hii sifa za mifupa zimehamishwa na kupewa Wakusinyika.

Zinguo: Hawa ni mifupa. Vifyefye; kama kaukau kwenye kikaango.(uk 21)
Mfupa ni kitu kigumu kilicho katika mwili wa mnyama au binadamu ambacho hushikilia minofu. Fasili tunayopata Zinguo anaposema haya ni kuwa Wakusinyika ni mifupa na katika hali ya kuwa mifupa bila shaka maana katika ulimwengu halisi haijitokezi. Katika hali hii sifa za mfupa zimehamishwa na kupewa Wakusinyika. Mfupa, kwa mfano fuvu la kichwa cha binadamu lionekanapo huwa linaashiria kifo au hali ya hatari na hutisha. Mifupa huwa ni ishara ya kiangazi, ukame na mateso kwa wanyama na binadamu kutokana na mazingira yaliyo kavu na yasiyoweza kuhimili maisha ya wanayoyategemea. Katika hali dhahania, ukiushi tulionao hapa ni kuwa hatuwaoni Wakusinyika wakiwa mifupa ila tunayofasili kuwa kutokana na usemi huo wa Zinguo ni kuwa Wakusinyika wanapitia dhiki kwa kuwa hawana chakula. Aidha, umaskini umeigubika nchi nzima. Wamekonda na kukondeana ndipo Zinguo anawaita mifupa na vifyefye. Kwa hivyo

Wakusinyika wanaogofya. Kukonda huku siko kukonda kwa maana iliyoko makamusini ila ni kukonda kunakoonyesha unyanyasaji na unyonyaji anaoutekeleza Zinguo pamoja na Mzuka katika mbinu wanazotumia za ukusanyaji ushuru ambapo anayetozwa ushuru tayari hana pato lolote hata la kujilisha yeye mwenyewe. Ni Mkusinyika ambaye kipochi chake ni chembamba na hakina pesa za ziada. Kauli hii katika maana kiushi inadhihirisha kuwa Zinguo anawahurumia Wakusinyika katika hali waliyomo ila hana jingine isipokuwa kutimiza mbinu alizofunzwa na Mzuka za kupata ushuru au pato la taifa ambalo linaishia mifukoni mwake na mifukoni mwa Mzuka.

Zinguo anakiri kuwa wameota misitu yote na kwa hivyo kuathiri mazingira yao ambayo ni chanzo cha mvua ambayo ikinyesha, chakula na mapato mengine yatakuwa kwa wingi. Wakusinyika watakuwa wenye afya na wenye kutia bidii katika kazi zao. Usemi huu bila shaka unaibua maudhui ya dhiki na umasikini iliyojaa njaa na mateso waliyonayo Wakusinyika kutokana na ukosefu wa chakula na mahitaji mengine ya kimsingi. Vilevile tunaona hali ambapo uchumi umekuwa hafifu na kwa hivyo kuwaacha katika hali ya kutojiweza licha ya Zinguo (kiongozi), kutaka kuwatoza ushuru zaidi ili kumfurahisha Mzuka ambaye ana njama zake za kutaka kuendelea kunyonya Kusinyika. Licha ya hali hii, Zinguo anaendelea kutumia mbinu alizofunzwa na Mzuka kuwatoza watu ushuru ingawa hawana lolote. Anamshurutisha Kaza ambaye ni kibaraka wake kuhakikisha kuwa kila mtu anatoa ushuru, kodi vilevile ni miongoni mwa ada zaidi ambapo kodi ya uegeshaji, forodha bandarini na kadhalika zinatozwa. Haya ni mapato ambayo yakielekezwa kwenye miradi ya kuiendeleza nchi, wananchi watanufaika. Hata hivyo, anaonekana kufuata mafunzo ya Mzuka na hata kumzidi. Hali hii ndiyo inayoitumbukiza Kusinyika katika hali ya kusambaratika.

Mzuka anapoona yamezidi; anajificha. Hali hii inamfanya Zinguo kuanza kujitapa kuwa ameshinda mwalimu wake bila kujua kuwa anawaumiza wanyonge ambao ni Wakusinyika. Sitiari fiche inajitokeza Zinguo anaposema kila mtu atoe 'kitu kidogo'. Katika ulimwengu halisi kitu kidogo ni kitu ambacho kinapopimwa kwenye mizani au kuangaliwa kwa macho tu hakina thamani kwa mwenye kukitoa. Lakini katika muktadha wa matini kunapokuwa na haja ya kuuwasilisha ujumbe wake maana ya ufiisadi ambao

humnyonya na kumguguna mwananchi mzalendo na kumnyima haki yake kikatiba kwa sababu ya mapendeleo inajitokeza. Sitiari hii kwa hivyo inaonyesha njama za Zinguo za kuendelea kuikandamiza Kusinyika licha ya Kusinyika kuwa huru.

Zinguo: Unaogopa mwanafunzi mwerevu?
Angurumapo simba? (uk 23)

Mara kwa mara katika utamaduni wa binadamu watu wanapohusishwa na majina ya baadhi ya wanyama, wao huhisi kuheshimiwa sana hasa majina hayo yakitumiwa kufaa sifa walizonazo. Mara nyingi wanyama ambao hupendelewa kwa sifa za ubora ni ndovu, simba, chui na hata fahali. Hawa ni baadhi tu ya wanyama ambao hurejelewa. Kuna hali ambapo licha ya kuwa na sifa za nguvu na nyinginezo bora, huwa na sifa hasi kwa mfano ujinga. Hali hii tunaiona katika sitiari hii.

Neno simba katika muktadha huu limetumika katika kutajirisha usemi. Sifa za mnyama huyu ni kuwa yeye huwa ni jasiri, mkali, mwenywe nguvu na ni mfalme wa mwituni. Vilevile ni mharibifu kwani huweza hata kusababisha kifo. Katika mukatadha, tukirejelea juhudi zake Zinguo za kutambua majibu ya vitendawili anavyotegewa na Mzuka, anajiona kuwa yeye ni gwiji bila kujua kuwa anaingia kwenye mtego wa Mzuka. Mzuka anamtegea vitendawili vinavyomfunza mifumo ya kiutawala ya Kimizuka. Hizi bila shaka ni juhudi za Mzuka za kumfunza Zinguo mbinu mbovu za kuwakandamiza Wakusinyika kwa kuwatoza ushuru mkubwa. Kwa hivyo anapotaka kukidhi haja zake za ushuru mkubwa bila shaka atatoa amri tu na bila shaka hakuna atakayepinga.

Sitiari katika mazungumzo haya inadhihirisha athari mbovu ambazo Mzuka amemwambukiza Zinguo. Zinguo hajali kiwango cha ushuru anachowatoza Wakusinyika. Hali hii ipo katika jamii ya sasa ambapo viongozi wa sasa wameshindwa kujitenga na athari za elimu ya kimizuka. Tumeshuhudia hali ambapo baada ya ugatuzi magavana walikuwa na azma ya kupata ushuru wa kiwango cha juu na hata kukawa na wale waliotaka hata kuwatoza wakulima wafuga kuku shilingi ishirini kwa kila kuku ili wawe na pato kubwa.

Sichana: Mimi mnyonge nanyongeka uchao
Mimi ndimi hayawani wa huduma
Najisitiri kwa matawi
Nyumba ya mama ganjo
Wana wanamalizika mama
Au umeridhi kunywa damu yao; (uk 25)

Wimbo huu unaimbwa na Sichana ambaye ni kijakazi wa Zinguo. Katika wimbo huu tamathali ya usemi ya sitiari imetumika. Kwa mfano:

‘Mimi mnyongenanyongeka uchao’

‘Mimi ndimi hayawaniwa huduma’

Katika muktadha wa matumizi ya ‘mimi mnyonge’ katika kazi hii tunaporejelea sifa za mnyonge hatuelewi ni unyonge wa aina gani kwani kuna unyonge wa aina mbalimbali. Kwa hivyo muktadha wa matumizi utatoa maana ya sitiari hii kikamilifu. Kwa mfano tunaweza kufasiri kuwa mnyonge ni mtu asiye na nguvu, mtu masikini au kabwela ama mtu mpole na mnyenyekevu mchochole na kadhalika. Kwa mfano katika methali ‘dau la mnyonge haliendi joshi, likienda joshi, Mungu kupenda.’ Tukiwa wasomaji wa matini haya tunafahamu madhila wanayopitia waimbaji wa wimbo huu; maana inayowasilishwa hapa ni kuwa Sichana hana haki na kwa hivyo ni mpole na mnyenyekevu. Hali hii ni hali inayoongezeka kila uchao kwani Zinguo kama kiongozi haonekani kutambua dhiki anazopitia Sichana. Kwa hivyo tumehamisha hali anazopitia Sichana na kuzilinganisha na maana ya neno mnyonge na kwa hivyo kuwa na ufasiri wa muktadha aliomo Sichana.

Katika usemi huu maneno ‘mimi’ na ‘mnyonge’ yana maana yake ya asili ambayo hayatoi maana katika hali dhahania ya kifasihi. Neno ‘mimi’ ni kiwakilishi cha Sichana na mnyonge ni hali ya kuwa dhaifu. Vilevile katika usemi ‘mimi ndimi hayawani wa huduma’. Ufasiri wa neno hayawani nao unasema hayawani ni mnyama wa porini au mtu mwenye tabia za kinyama; mpuuzi, baradhuli au mwendawazimu au katili. Bila shaka hii siyo maana inayojitokeza tunaporejelea matini. Ila maana inayojitokeza kiukiushi ni kuwa Sichana ni mkosa haki na kwa hivyo hawezi kujitetea au kupigania haki yake mbele ya Zinguo. Amefinywa na kukandamizwa na Zinguo ilhali anampa Zinguo huduma za kimsingi kwa mfano kuyaweka mazingira yake kuwa safi, kuandaa chakula

na hata kuwakaribisha wageni wajapo kumtembelea. Kwa jumla anafanya kazi za aina yote. Licha ya hayo, mazingira aishimo ni kinyume kwani hali yake ya afya haizingatiwi na mwajiri, ameliwa na funza na ni mwenye njaa; hali inayosababisha unyonge wake. Bila shaka hizi ni haki za kimsingi anazohitaji mfanyikazi aliyeajiriwa na ikiwa hazipo mfanyikazi lazima awe mnyonge na asiyeweza kutimiza wajibu wake. Hali hii vilevile inapelekea Sichana kuwa hayawani kwani hayawani hufanyishwa kazi bila mapumziko na malipo mazuri. Mara nyingi huishia kutumiwa kwa manufaa ya bwana wake na anapoishiwa na nguvu huachwa afe au huchinjwa ili kumfaidi bwana. Chambilecho usemi maarufu; mnyonge hana haki. Wimbo huu vilevile umeimbwa katika taasisi za kielimu. Kwa kawaida taasisi za kielimu huwa na hadhira kubwa kwani hujumuisha wazazi, watoto, walimu pamoja na jamii iliyoizunguka taasisi hiyo. Kwa hivyo dhiki anazozungumzia Sichana katika wimbo huu ni uwakilisho wa mateso inayopitia jamii hii.

Kauli ‘nyumba ya mama ganjo’ kwa kulitazama neno hili kikamusi, ganjo ni mahali palipotelekezwa au mahame. Kwa hivyo Sichana anaposema nyumba ya mama ganjo ana maana kiushi kuwa hali ya maisha ya mama yake ni ya dhiki. Kuna umaskini uliokithiri na kumfanya mama kuishi katika nyumba inayofanana na mahame; hali inayodhihirisha upweke na umaskini.

Bila shaka kauli hii inaibua maudhui ya nafasi ya wanawake katika jamii na katika mfumo mzima wa kiuchumi. Wanawake katika mfumo wa kiuchumi wananyanyaswa maradufu. Kwanza wananyanyaswa kama wanawake kimaumbile. Pili wanakandamizwa kama wafanyikazi. Utamaduni umempa mwanamke nafasi duni maishani na pindi akijaribu kukiuka nafasi hiyo huonekana kuwa msaliti. Kwa hivyo Sichana anabakia kuwa jikoni na kumwandalia Zinguo mlo ingawa anaishi katika mateso na dhiki. Hali hii ya ukandamizwaji ndiyo inayomfanya Zinguo kumnajisi Sichana, kumpa malipo duni, kutojali hali yake kiafya, kielimu, kimavazi na mahitaji mengine ya kimsingi. Kwa hivyo mwanamke ni mfanyakazi tu. Kwa hivyo mwanamke amechorwa katika hali ambayo haiendelezi hadhi yake katika jamii. Sifa hizi zinazotokana na kauli hii zinamfunga shemere na kumkwamisha katika maendeleo yake. Usemi huu unatuonyesha kuwa mwanamke ameachiwa majukumu yote katika jamii. Mwanamke amechorwa katika mazingira finyu yanayomnyanyasa na ambayo katu hayawezi kumkuza kimaendeleo.

Hali hii imesababishwa na mifumo ya kitabaka na utamaduni wa jadi uliosheheni dhana za kibaguzi na taasubi za kiume zinazokandamiza wanawake.

Katika ulimwengu halisi, haiwezekani nchi kuitwa ‘mama’ kama ilivyotajwa katika muktadha huu. Ila kuna ukweli katika matumizi ya kauli hii katika wimbo anaoimba Sichana. Mama ni mzazi na hivyo huwa kiumbe muhimu sana kwa alichokizaa. Katika hali hii, ni dhahiri kuwa ulinzi wa mama ndio bora kwani hujaribu kuzuia hatari zozote zisimfike mwana. Maana inayowasilishwa hapa ni kuwa Sichana analalamikia hali ya maisha katika Kusinyika ambayo ni ya kunyanyasa na kutesa. Kwa hivyo ni Wakusinyika na Kusinyika kujikomboa kutoka katika maangamizo ya athari za ukoloni mamboleo zilizoonekeni. Kwa hivyo Sichana hana mwingine wa kumlilia ila Kusinyika alimozaliwa na ambayo anaihudumia kwa uzalendo na unyenyekevu pamoja na heshima jinsi mwana humpa mama heshima na kuzidi kumtumainia hata akiwa katika ukubwa wake.

Zinguo: Basi hizo ni shule jinga! Walimu wake ni majinuni. Nitazifunga na kuwapa funzo hao walimu! (Uk 27)

Katika hali halisi ya matumizi ya kauli ‘walimu wake ni majinuni’, haiwezekani kwa shule kuwa jinga. Ujumbe tunaopata kulingana na matumizi ya kauli hii kwenye matini ni kuwa mafunzo waliyopewa wanafunzi katika shule hii yalikuwa ya kulalamikia aina ya uongozi uliokuwapo uliokuwa umejaa unyanyasaji, utabaka na kutojali haki za wananchi. Kauli hii vilevile inaendeleza maudhui ya elimu. Tunatambua kuwa elimu iliyotolewa ilikuwa ya kuendeleza unyenyekevu kwa utawala uliokuwepo. Hizi bila shaka ni sifa za mfumo wa kikoloni za kuwakandamiza watawaliwa kwa kuwapa elimu ya kuwafanya wao kuwa watumwa milele na wenye kutenda mambo bila kuuliza au kutaka kujua sababu za kufanywa yanavyofanywa. Ndipo Zinguo anasema ‘nitazifunga na kuwapa funzo hao walimu’. Hali hii vilevile inaonyesha ukosefu wa uhuru wa wafanyakazi kutenda kazi zao jinsi walivyozisomea ili kupata matokeo bora kwa manufaa ya Kusinyika.

Neno ‘majinuni’ humaanisha mtu asiye na akili, mpumbavu, punguani. Walimu ambao ni taa ya kuwapa Wakusinyika mwanga wa maendeleo kupitia elimu wanapewa jina hili.

Huku bila shaka ni kukosa kutambua umuhimu wa walimu kwa Wakusinyika. Hali hii inachangia katika matatizo yanayoikumba Kusinyika. Katika hali kiushi tunapata fasili kuwa Zinguo kama kiongozi anachangia katika upumbavu wa walimu anaodai kuwa majinuni. Walimu hawa wamekosa maadili ya kikazi kutokana na hali mbaya ya uongozi wake Zinguo ambao umeathiri sekta zote ikiwemo sekta ya elimu. Kwa hivyo uongozi wa Zinguo una upotovu, umejaa udanganyifu na unanawirisha unyonge katika jamii.

Mtu 1: Enzi ya Mzuka na sasa enzi ya Zinguo. Tuliyaona yakipaliliwa, Zinguo na Mzuka ni ambari na mzuwele!
Nendeni. Mnatucheka kwelisisi punguani

Mtu 2: Ameruhusu mizuka kuwa makuhanika katika madhabahuya Kusinyika. (uk 33)

Mtu 1 na Mtu 2 ni watu ambao ni mke na mume. Wahusika hawa wawili wanawakilisha mrengo mmoja wa Kusinyika. Mtu 1 na Mtu 2 wameishi katika nyakati mbili; nyakati ambazo mkoloni alitawala au wakati wa ukoloni mkongwe na wakati ambapo Zinguo aliwekwa mamlakani na mkoloni au wakati wa ukoloni mamboleo. Hali hii inawafanya kuwa na tajiriba ya kutosha ya kulinganisha sifa za uongozi wa nyakati hizi mbili. Katika usemi wake Mtu 1 anasema ‘....Zinguo na Mzuka ni ambari na mzuwele’. ‘Ambari’ ni kitu mithili ya anta ngumu chenye harufu nzuri na rangi ya hudhurungi, kinachotokana na samaki wa jamii ya nyangumi, kwa kawaida huliwa ili kuongeza nguvu. Ufasiri wa neno ‘nta’ tumeshaona kuwa ni kitu kinachofanana na gundi ngumu ambacho hutengenezwa na nyuki. Bila shaka ili nyuki kutengeza asali ni lazima kuwe na nta ambayo huwa vyumba spesheli vya kuhifadhi asali wanayokusanya nyuki.

Kwa hivyo kwa maana ya nje tunaona kuwa Zinguo na Mzuka ni ambari na mzuwele. Kwamba wanaambatana. Katika hali kiushi tunapata kuwa Zinguo na Mzuka wanajuana kivilemba. Ni washirika wakubwa ambao wanafanya mambo pamoja na kwa hali ya kushirikiana na kufaidiana.

Mzuka ana njama zake na kuna anavyomwelekeza Zinguo ili kufaidi kutokana na Kusinyika. Naye Zinguo anafanya juhudi za kumfurahisha bwana wake. Mtu 1 anaonekana kuwa makini pamoja na mkewe ambaye ni Mtu 2. Hali hii vilevile

imewafanya wao kujua kuwa Zinguo ametiwa silisili za ukoloni. Wanayafahamu haya kutokana na imani kubwa aliyokuwa nayo kwa mkoloni kwani alidhani mkoloni alisema mambo ya ukweli. Hata hivyo kwa sababu ya uwezo wa kutafakari wa msomaji, ni ukweli kwamba Mtu1 amewalinganisha na kugundua kuwa Zinguo ni mnafiki na ana uhusiano wa karibu na Mzuka. Mtu 1 na Mtu 2 wanaamuka na kuanza kuipa Kusinyika mwelekeo. Wanataka kuondoa Kusinyika katika minyororo hii ya uongozi mbaya uliojaa athari za mkoloni. Wanawatahadharisha vijana kwani umri wao una haki ya kuwafanya wao kulinganisha nyakati zote mbili za ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo na kutambua udhaifu wa mbinu za uongozi katika nyakati zote mbili na kupata mwelekeo unaoifaa Kusinyika. Uelewa huu wa kihistoria unawafanya Mtu 1 na Mtu 2 kudhihirisha uzalendo wao na ari ya kutaka kuikomboa Kusinyika kutoka katika ukoloni mamboleo.

Mtu 2: Ameruhusu mizuka kuwa makuhani katika madhabahu ya Kusinyika! (uk 33)

Katika ulimwengu halisi neno ‘kuhani’ lina maana ya kasisi au kiongozi wa Kiyahudi. Vilevile, kuhani ni mganga wa kienyeji anayebashiri mambo yatakayotokea siku za mbele au kutibu magonjwa kwa kutafsiri ndoto, kuangalia nyota na kadhalika. Kwa hivyo kuhani huwa ni mtu wa kuaminiwa katika jamii kutokana na wajibu alionao katika jamii anamoishi. Tunapojaribu kufasiri neno kuhani kutokana na uelewa huu hatupati maana. Kimuktadha, Mtu 2 anapotamka kauli hii anatuonyesha kuwepo kwa athari za kikoloni katika mbinu za uongozi za Zinguo ambaye alichukua uongozi kwa madai kuwa alitaka Kusinyika iwe nchi iliyo huru na yenye kujitawala. Kuhani bila shaka huwa na jicho la ndani na huweza hata kutabiri na kutoa mwelekezo ambao lazima ufwatwe na anayemsikiza ambapo akikosa kufuata bila shaka ataingia katika matatizo au atazidi kusononeka kutokana na mashaka yaliyompata. Zinguo kwa hivyo ni kiongozi ambaye hakujiamini na atakapo kufanya lolote ni lazima ategemee ushauri wa Mzuka ambaye ni mwenye ujuzi na nguvu za kumtawala Zinguo na Wakusinyika. Hali hii ndiyo inayowafanya wakusinyika, kupitia kwa Mtu 2 kusema kuwa Zinguo amemfanya Mzuka kuwa kuhani katika Kusinyika. Hali hizi wanaharakati ambao ni Mtu 1 na Mtu 2 wanazijua na kwa hivyo kama wazalendo hawapendi kuiona nchi yao ikitumbukia katika uongozi wa aina hii. Kwa hivyo wana uzalendo na wangependa kuihudumia nchi yao

kwa moyo wa dharti na wapo tayari kuitetea bila kujali masilahi ya kibinafsi afanyavyo Zinguo aliye na silisili za mkoloni.

Hali ya kauli hii bila shaka ni ya kujenga maudhui ya utegemezi na kuamini kuwa mawazo mazuri na uamuzi wenye kuleta mafanikio lazima utoke kwa wakoloni.

Katika mazungumzo ya wahusika tuliyoyanukuu hapa chini kuna sitiari. Sitiari hizi tumezidhihirisha kwa maneno yaliyokolezwa. Kwenye sitiari hizi, kuna maana zaidi ya maana za kawaida tunazopata katika maneno haya tunaporejelea muktadha wa matumizi yao. Hebu tuyatathmini mazungumzo haya.

Mtu 1: Soko halikosi wazimu.

Vijana: Mnatuita ng'ombe?

Mtu 1 na mtu 2: La ! hapana ng'ombe hapa.

Mtu 1 na Mtu 2: Ari yetu! Umoja ni nguvu. Wakati wa kusinyika kuwa moja ni sasa. (uk 34)

Neno wazimu lina maana ya kutokuwa na akili timamu; kichaa, umajinuni au uafkani. Maana hii inajitokeza katika ulimwengu halisi. Kwa kurejelea muktadha wa kauli ya Mtu 1 kuhusu swala la wazimu, tunamwona Mtu 1 akiwa amefadhaishwa na hali ya vijana kutofahamu mazingira yao vyema. Kwa hivyo Mtu 1 anawachukulia vijana kuwa watu wasio na akili timamu, wagonjwa wa akili au kichaa. Kwa hivyo Mtu 1 anatuonyesha jinsi vijana wasivyokuwa na ufahamu wa uongozi mbaya katika Kusinyika. Uongozi huu umejaa ubepari, unyanyaswaji na upofu mwingineo mwingi ulioisambaratisha Kusinyika. Mlinganisho huu wa moja kwa moja unaonyesha hali waliyomo vijana ambao hawashirikiani na wazee kujua historia ya nchi yao ili wawe na mwelekeo wa kuifanikisha nchi yao pamoja na kujenga uzalendo. Kauli hii vilevile inaonyesha umuhimu wa Mtu 1 na Mtu 2 katika kujaribu kuziba pengo la kihistoria na la kiwakati ambalo limetokea na ambalo Zinguo angependa kutumia hali ya vijana ya kutofahamu ukweli ili azidi kuwapotosha. Hali hii vilevile inarejelea majinuni. Ng'ombe pia ametumiwa kurejelea hali hii ya upumbavu. Mara nyingi katika jamii za Kiafrika mtu mjinga huitwa 'ng'ombe'. Katika kurejelea muktadha huu, hali ya vijana ya kutojua historia na chanzo cha matatizo yao katika Kusinyika inawafanya Mtu 1 na Mtu 2 kujishuku kuwa ng'ombe.

Hali ya kukosa kuwa na uongozi mzuri inasababisha mgogoro baina ya vijana na Mtu 1 na Mtu 2 ambao ni mke na mme. Mtu 1 na Mtu 2 wanawarejelea vijana kimapumbo. Neno wazimu lina maana ya hali ya kutokuwa na akili timamu; kichaa, umajinuni au uafkani. Sitiari hii inamrejelea Mtu 1 kimapumbo. Mtu 1 anawaona vijana kama waliokosa akili kwani licha ya kusinyika kujaa mateso kwa watu wake, vijana hawa hawaoni. Wanazidi kumfuata Zinguo kama watu walio na akili punguani. Kwa hivyo vijana na Zinguo wanajiona wamoja ndio maana wanajishuku kuwa ng'ombe wanapotahadharishwa na Mtu 1. Mgogoro unapanda Mtu 1 na Mtu 2 wanapoambiwa kuwa wao ni wendawazimu. Hali hii inaishia vijana kugundua kuwa Mtu 1 na Mtu 2 hawataki mzaha na kwa hivyo wanatokomea. Bila shaka hali tunayoona hapa ni mapambano ya walio na ufahamu wa uongozi mbaya wa Zinguo wakipigania kuwazindua walio usingizini na kuwataka wapambazukiwe na hali iliyopo ili Kusinyika iwe na mwelekeo mmoja. Ili kuokoa hali hii Mtu 1 na Mtu 2 wanaona ni bora kuungana dhidi ya hali hii na kwa hivyo kuafikiana kuwa umoja ni nguvu. Tamko hili la Mtu 1 na Mtu 2 ni sitiari inayorejelea maana kwa kwa Wakusinyika wote kuungana kuipinga hali hii wataiokoa nchi yao. Kwa hivyo sauti za wasiotosheka lazima zisikike na umoja huu utaifanya sauti hiyo kuwa kubwa zaidi na yenye kuleta mapinduzi. Kwa hivyo maudhui ya mapinduzi yanaibukia hapa.

Katika kauli zifuatazo za Vijana, Mtu I na Mtu II kuna sitiari. Wahusika hawa wanaitana kwa majina ya kuwarejelea viumbe wengine wanaodhani kuwa wanafanana nao kitabia. Tunapata mazungumzo haya:

Vijana: Kuna wendawazimu watatu....

Mtu 1: Majinuni watatu....

Sitiari hii inazua mgogoro baina yao ambapo kunakuwa uvumbuzi mkubwa wa vijana kuwa vibaraka wa Zinguo kwani wanadai kumfikishia Zinguo ripoti. Hali hii inaonyesha misingi ya ukoloni mamboleo katika kugawanyika kwa jamii ya Wakusinyika. Zinguo na Mzuka wamewateka akili za vijana bakunja na kwa hivyo kuwafanya vijana kuwa majinuni. Haya yanapoendelea wao wameitumia fursa hii kudhibiti uchumi na kuendelea kuwanyanyasa Wakusinyika kupitia asasi mbalimbali, hali inayoendeleza sura mpya ya ukoloni mamboleo.

Mtu 2: ...fikiria kuwa kabwela nchini mwako.

Usemi huu unamchochea Mtu 2 kupigania haki yake ili kujinasua katika minyororo ya ukoloni mamboleo. Sintofahamu iliyotokea baina ya vijana, Mtu 1 na Mtu 2 inatufanya tuelewe utengano uliopo baina ya vijana na wazee katika jamii hii. Aidha Mkusinyika amechorwa baada ya uhuru kuwa amenyanyaswa kupitia asasi mbalimbali zenye misingi ya kiuchumi kwa mfano utawala, biashara na dini.

Mtu 1 na Mtu 2 wanawakilisha wazee ambao wameishi katika enzi zote mbili na kwa hivyo kuwafanya kuelewa matatizo waliyonayo na hata kufahamu chanzo cha matatizo hayo na suluhisho vilevile. Vijana nao wanaonekana kuwa bendera ambayo hufuata upepo. Wanakuwa vibaraka wa Zinguo na kwa hivyo kuwa chanzo cha fujo. Kutokana na msukumo waupatao kwa Zinguo.

Mtu 1 anawaita ‘majinuni watatu’ majinuni ni watu wapumbavu, punguani au mtu aliyepungukiwa akili. Katika muktadha huu Mtu 1 na Mtu 2 wanawaona vijana kuwa wapumbavu kwa kuwa hawayaelewi mazingira waliyomo. Zinguo ameangamiza nchi kwa ukabila, njaa, ufisadi na kuangusha sekta muhimu zinazokuza uchumi wa nchi, hali iliyosababisha umasikini. Neno ‘kabwela’ kikamusi lina maana ya mtu wa kawaida asiye na pato la haja. Kwa kurejelea muktadha wa matumizi wa kauli hii tunafasili kuwa Mtu 2 hafurahii anavyoshughulikiwa na kiongozi aliye kwenye madaraka. Kuwepo kwake katika uongozi kumemfanya kuwa maskini zaidi ya alivyokuwa na hata kuishia kuwa mtwana. Katika hali yake ya utwana anawahudumia mabwanyenye wawili ambao ni Zinguo na Mzuka ambao wanamnyanyasa na kumfanya kukosa mwelekeo katika maisha. Sitiari katika usemi huu inaibua maudhui ya umoja ili kuwafanya Wakusinyika kutambua kuwa na mikakati ya mapinduzi yenye mwelekeo utakaowafaa na kwa hivyo kuanza kuijenga Kusinyika upya na yenye mafanikio kwa wote na ila si wachache na waliopoteza mwelekeo.

Katika usemi wa Zinguo tunaoulenga hapa chini kuna sitiari inayomtaja Zinguo kuwa mvumbuzi, mwokozi na mgunduzi. Kwa hivyo mhusika huyu anatumia sitiari hii kuondoa uchapwa lakini kwa njia fulani anaibua maana kuwa jukumu la kuubatilisha ukoloni mamboleo sio kazi rahisi kwani wanaotekeleza mfumo huu huwa macho na

wakali kwa yeyote anayethubutu kuwaingilia lakini akifaulu kutakuwa na afueni Kusinyika. Wao hulinda mfumo huu kwa silaha kali, mahakama na hata polisi na jeshi.

Zinguo: Hata mbuhapa hawakaribii. Malaria ishindwe. (uk 37)

Zinguo ni mvumbuzi. Zinguo ni mgunduzi! Zinguo ni mwokoziwa watu wake!

Kikamusi neno mvumbuzi lina maana ya mtu anayeanzisha jambo kwa mara ya kwanza katika jamii. Sifa za mtu kama huyu ni kuwa lazima awe ni mwenye busara, mvumilivu, mwerevu na mwenye azma ya kutaka kusaidia jamii kuepuka matatizo yanayoikumba. Huu bila shaka ni mtazamo wa maana ya usemi huu katika hali ya ulimwengu halisi bila kutazama matumizi yake kimuktadha. Tunapoitathmini kauli hii kwa kurejelea muktadha wa matumizi katika matini, tunakuwa na fasili tofauti. Kwanza tunazihamisha sifa za mvumbuzi na kumpa Zinguo.

Katika kauli ‘Zinguo ni mvumbuzi’ tunaelewa katika hali halisi ya maana ya maneno kwamba Zinguo ana uwezo wa kuanzisha, kugundua kitu muhimu kwa manufaa ya jamii. Zinguo ni mgunduzi! Kauli hii ni sawa na hiyo iliyotangulia. Anamaliza kwa kusema ‘Zinguo ni mwokozi wa watu wake.’ Maana katika hali halisi tunaona tu hali ya Zinguo kuwa mgunduzi na mwokozi. Lakini katika hali kiushi ni lazima turejeele muktadha. Zinguo ni kiongozi aliyepewa madaraka na mkoloni; Mzuka, na kwa hivyo ana wajibu wa kuwaongoza Wakusinyika katika kutambua vipaji vyao katika mawanda ya elimu, spoti, uzalishaji mali, tunu ya malighafi na faida chungu nzima zipatikanazo katika Kusinyika. Hata hivyo hapendezwi na tabia ya Mzuka ya kuingilia mfumo wake wa kuitawala Kusinyika na kwa hivyo anatafuta mbinu za kujaribu kumwondoa Mzuka. Zinguo anatumia mbinu zilizopitwa na wakati na ambazo haziwezi kumkomesha Mzuka kwani ni mbinu dhaifu. Kwa hivyo analalamikia ushirikiano wake na Mzuka wa kupewa wajibu wa kuingoza Kusinyika. Wajibu huu anauona kuwa na walakini kwa kuwa licha ya Mzuka kuondoka, athari za kimizuka bado ziko na Mzuka bado anaingilia jinsi anavyoiongoza Kusinyika. Ingawa anashirikiana na Mzuka kwa mengi, Zinguo hapendi hali hii.

Tunaloshuhudia hapa ni unafiki wa Zinguo kama kiongozi mchanga wa Kusinyika baada ya uhuru. Viongozi Waafrika walijisifu kuwa walimuelewa mkoloni na sifa zake sote na siri zake vilevile. Jambo la wazi ni kuwa hakuelewa hila za mkoloni na kwa hivyo kushindwa kumwondoa mkoloni kwani walitumia mbinu ambazo hata wao wenyewe kama viongozi hawakuzielewa. Kwa mfano Zinguo anatumia maji na moto kama njia ya kumfukuza Mzuka. Haya Mzuka anayaona kama mchezo na hata kuuzima moto huo Zinguo anapolala kidogo. Hali ya unafiki inajitokeza kwa kuwa hatuoni Zinguo akiyashughulikia matatizo ya Wakusinyika. Bado anashughulia kumuondoa mkoloni kwa hivyo anaona kuwa amesalitika na hila za mkoloni na kudanganyika kiasi cha kutouona uhuru wake pamoja na wa Wakusinyika. Anatimiza matakwa ya mkoloni bila kujua kwani walipopigania uhuru hawakutafuta maarifa ya kumpigia mkoloni ila walitegemea mbinu walizofunzwa na mkoloni ndipo Zinguo anapojaribu kuondoka katika minyororo ya mkoloni anapata pingamizi kubwa na mbinu anazotumia ni dhahaka kwa mkoloni. Mzuka anajua kuwa mbinu alizomfunza Zinguo ni za kudhihirisha ubinafsi ambapo bila shaka ni aina ya sifa ya uongozi ambao hauwezi kupendezwa na Wakusinyika. Kwa hivyo Zinguo hana mtagusano na Wakusinyika. Zinguo anaposema kauli hizi bila shaka ni mwenye kujitapa na kutowashirikisha Wakusinyika katika uamuzi wa maamuzi muhimu ya Kusinyika. Hali hii inawafanya Wakusinyika kujitenga naye na kwa hivyo kumpa Mzuka nafasi rahisi ya kupangua mikakati yake ya kumpinga. Kwa hivyo, kauli hii ya Zinguo ya kujiita mwokozi ni njia moja ya kujiliwaza kwani haungwi mkono na Wakusinyika. Vilevile, Mzuka anamtumia ili kushibisha nafsi yake. Kwa hivyo ingawa Mzuka amempa uhuru, Zinguo anajihisi huru lakini hana nguvu na uwezo wa kujinasua kutoka katika ujanja wa kimizuka.

Katika usemi huu wa hadhira kuna sitiari. Sitiari hii katika hali dhahania inatoa mwanga kuwa misaada itokanayo na mkoloni huja na masharti. Hali hii huwa kinyume kwani nchi hizi zinazosaidiwa huwa huru lakini licha ya viongozi wake kuhubiri uhuru huu, wanatawaliwa na wanaowasaidia kwa ushirikiano wa kuisambaratisha nchi. Tunasoma.

Hadhira: Umetufionza!

Umeifionza (uk 39)

Fyionza ni kitenzi kinachomaanisha kuvuta kitu cha majimaji mdomoni kwa kutumia nguvu za mashavu na ulimi. Katika ulinganishi huu tunaona kuwa mwenye kufyonza ndiye mwenye nguvu na bila shaka kinachofyonzwa humalizika kulingana na uwezo wa anayefyonza. Katika hali hii sitiari katika kauli hii inawarejelea Zinguo na Mzuka mtawalia. Mzuka amemwambukiza Zinguo tabia ya unyakuzi na kujilimbikizia mali. Mbali na haya anamhadaa kwa zawadi ndogo ndogo kama sharubati na mikate.

Kauli hizi ni sitiari kwani kitendo cha kufyonza huwa ni cha mdudu kwa mfano kupe au mbu. Katika hali kiushi, tunavyoona ni kwamba hadhira imezindukana na sasa ni lazima wamwambie Zinguo ukweli wa mambo. Wamechoka na yote yafanyikayo madhabahuni na kwa hivyo wanautafuta uhuru wao wa kusema na kurekebisha uozo ulioko katika madhabahu ili kuinusuru Kusinyika. Tunaloshuhudia katika kauli hii ya hadhira ni vilio vya umma. Watu ambao ndio nguzo ya Kusinyika wanaweza kudanganywa kwa muda fulani tu na mara wanapotanabahi wameshika kasi ya kujiondoa katika ukoloni mamboleo ili wajikomboe. Kauli hii vilevile inaibua ukosefu wa uaminifu katika uongozi mbaya wa Wakusinyika na kwa hivyo wanalotangaza bayana ni kuwa wanajua kinachoendelea madhabahuni. Zinguo kama kiongozi anawanyang'anya watu mali yao bila aibu pamoja na kukitumia cheo chake vibaya. Hadhira ni watetezi wa kweli na wazalendo kwani wanamtahadharisha Zinguo dhidi ya utamanifu wake.

Katika usemi wa Sauti na Zinguo kuna sitiari. Sitiari hizi tulizozitambulisha kwa mkolezo zina maana zilizohamishwa na kulinganishwa na kulinganishwa na kitu kingine. Hali hii kwa hivyo inadokeza maana tofauti na maana yake ya kawaida. Tunasoma.

Sauti: Usijitie uhakimu bure, ukubwa ni hadhi na kujiepusha na..

Zinguo: Mimi ni nabii wenu. Mimi ni mwakilishi wenu (uk 40)

Neno 'ukubwa' lina maana ya kuwa na cheo, umbo au umri zaidi ya wengine. Nalo neno hadhi lina maana ya heshima, staha au turuhani. Katika ulimwengu halisi maana hizi za maneno haya hazitufaidi. Lakini katika muktadha wa matumizi ya maneno haya tanahamisha sifa za neno ukubwa na kulipa neno hadhi. Katika hali ya kuwa mkubwa kwa maana ya kuwa na cheo, tunaibukiwa na sifa za uwajibikaji, uwezo wa kutimiza

jambo, kuunganisha, kuelekeza na hata kufanikisha maono ya watu au wafusi wako. Nalo neno hadhi likipewa sifa hizi basi hufanikisha matarajio hayo yote ya sifa za ukubwa.

Kauli ‘ukubwa ni hadhi’ inaturejesha katika ukweli ambao mtawala Zinguo anaukimbia. Umma umechoka kupotoshwa muda mrefu. Kwa hivyo wamechoka na mfumo huu wa Zinguo ambao haujali maslahi yao ila kuzingatia tu mtaji utokanao na nguvu zao na kujinufaisha kama mtu binafsi.

Sauti: Mimi ni sauti yenye nafsi kubwa ya kuzingua
Mzuka (uk 42)

Hebu tutathmini kauli hii ‘mimi ni nabii wenu’ neno ‘mimi’ ni kiwakilishi cha nafsi ya kwanza na ‘nabii’ ni mtu anayesadikiwa kuwa na nguvu maalum za kumwezesha kusema mambo ambayo Mungu anataka kueleza watu wake; mtume, rasuli. Kwa kuyasoma maneno haya kwenye matini bila kurejelea muktadha hakuna fasili yoyote tunayoweza kupata. Zinguo anaposema kuwa yeye ni nabii anajipa uwezo wa kuwahudumia Wakusinyika. Anadai kuwa nafasi aliyomo ni nafasi aliyopewa na akina babu wa kusinyika na kwa hivyo haifai kwa yeyote kujitokeza ili kutaka kuchukua nafasi hiyo. Anadai kuwa gwanda la uongozi alilonalo alipewa na babu wa kusinyika na kwa hivyo hawezi kuliweka chini kiholela. Kwa kurejelea muktadha huu tunaona Zinguo akikwamilia madarakani na kujiona kuwa yeye ndiye bora na chaguo la wazee. Sitiari hi inatujengea picha ya ubinafsi ambapo Zinguo hawatambui kuwepo kwa jamii ya Wakusinyika. Bila shaka huu ni mfumo wa ubepari. Kama mfumo huu ungetambua kuwepo kwa jamii ya Wakusinyika, ungemfanya Zinguo kufikiria kabla ya kuendelea kuharibu na kuchafua mazingira ya nchi ya Kusinyika na pia kusababisha uchafuzi wa jamii unaodhihirika katika umasikini, unyakuzi wa ardhi, udhalilishaji, ukiwa, ufukara na uvunjaji wa sheria. Hali hii inaipelekea sauti kutoa kauli yenye tahadhari kuwa ‘mimi ni sauti yenye nafsi kubwa!’ hii vilevile ni sitiari inayomkumbusah Zinguo ambaye ni kiongozi kuwa Mkusinyika ana jukumu vilevile katika kutoa maamuzi muhimu ya kuiongoza nchi. Hali hii Zinguo ameipuuza na kuwaacha Wakusinyika kwa kutowashirikisha katika uongozi wa Kusinyika. Huu ni ubinafsi. Kwa hivyo usemi huu wa sauti ni tahadhari ya mapinduzi kwa Zinguo dhidi ya ubepari na ukoloni mamboleo kwani kama kiongozi, amewapuuzilia mbali na ila hajatimiza chochote na sauti hii si ya

mmoja ila ni Wakusinyika wote wanaopitia mateso ya uongozi mbaya wa Zinguo. Kwa hivyo kauli hii ni ya wengi ambao wataendelea kumkosoa ili kuwe na mwelekeo bora Kusinyika.

Kauli ‘mimi ni nabii wenu’. ‘Mimi ni mwakilishi wenu’. Ni kauli inayoibua kiburi alichonacho Zinguo. Zinguo ni kiongozi na ana tabia ya kupenda kujisifu pamoja na kuonyesha kiburi, kutenda mambo ili kuonyesha ulimwengu badala ya kuwafaidi watu. Tabia ambayo ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya Kusinyika. Huku ni kujisifu kusikokuwa na maana yoyote kwani Zinguo anaukimbia uhalisi. Tumeona kuwa Kusinyika ina uongozi mbaya kwani Zinguo hawashirikishi wananchi wenzake katika uongozi wake. Hali hii imepelekea kuzinduka kwa Wakusinyika ambapo wanamshauri na kumkosoa anapokosea. ‘Mimi ni sauti yenye nafsi kubwa’. Katika sitiari hii dhana ya uzindukaji wa Wakusinyika inajitokeza kupitia sauti ambapo pametajwa udhaifu alionao Zinguo katika uongozi wake kwa mfano kukosa kuwashirikisha Wakusinyika katika maamuzi muhimu ya nchi, ukosefu wa umoja na hata busara katika uongozi wake.

Kwa hivyo kutokana na kiburi cha Zinguo na wingi wa majisifu, anazidi kupoteza wakati kwa kujizungumzia binafsi badala ya kufanya kazi kwa nguvu na bidii. Hali hii imechangia pakubwa katika kuporomoka kwa uchumi na hali ya maisha.

Mzuka: Mambo sasa yataimarika. Hii ndiyo njia yangu ya kushirikiana na washirika wetu. Akili ni nywele, Zinguo ana zake! Fikiria utakavyoilipia hisani. (uk 46)

Methali anayoitumia Mzuka ni yenye sitiari. kulingana na Wamitila (2001:9) methali hii ina maana kuwa akili za watu hutofautiana kama zilivyo nywele kichwani. Methali hii hutumiwa kumzindua mtu anayeshangaa kuwa watu wanafanya mambo kwa namna tofauti na anavyoyafanya yeye. Tafsili hii haitupi ufasiri tunaotarajia kutokana na kauli hii kwenye matini. Kauli hii Mzuka anitoa akiwa na lengo. Anaitaja methali hii baada ya kumrubuni Zinguo kwa kumpa fimbo ya kuwachunga Wakusinyika, kofia kama taji na hata kuvalishwa gwanda. Haya yote anayopew hapewi bure ila kwa lengo la kumfaidi Mzuka. Usemi huu kwa kweli unadhihirisha njama alizokuwa nazo mkiloni kwa nchi za Afrika. Kupitia kauli hii kimuktadha tunagundua kuwa fadhila anazopata Zinguo kutoka kwa Mzuka haziendi bure kwani anadai kurudishiwa fadhila hizo baada ya kutoa elimu

yake kwa Zinguo. Hali hii bila shaka inawaacha Wakusinyika katika dhiki kwani mali yao asili kama vile misitu, ardhi na madini vinasafirishwa kwenda ng'ambo kumfaidi Mzuka na Zinguo. Wakusinyika hawafaidi kwani wanalalamika kukosa haki za kimsingi kama vile kukosa uhuru, chakula na hata matibabu. Zinguo anawajibu kwa kuwaambia kuwa Mzuka hajaleta misaada ya kuwezesha haya. Kauli hii inaibua maudhui ya utegemezi na ukoloni mamboleo.

2.2 Chuku

Wamitila (2008:394) ameanisha chuku chini ya tamathali za usemi za maneno. Anasema chuku ni tamathali za usemi za maneno ambazo zimejengwa kwenye neno au maneno fulani. Wamitila (2008) anasema chuku ni tamathali ya usemi inayoeleza hali ya sifa ya kitu kuelezwa kwa namna inayokuza sifa zake au kuzidunisha sifa hizo kuliko hali yake ya kawaida.

Chuku kwa hivyo ni hali mbapo maelezo yanatiliwa chumvi kwa minajili ya kulisimua ama kuelezea hali fulani. Kwa msingi huu basi huwa pana ukinzani kati ya hali inayosemwa na ukweli wenyewe. Hii ni sifa ambayo inahusishwa kwa kiasi kikubwa na kinaya. Kwa mfano 'ni rahisi kwa ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko kwa tajiri kuingia ufalme wa mbinguni.' Hii ni chuku maarufu ya Biblia.

Oiro (2014) akimrejelea Wales (1989) anasema Wales alionelea kuwa mara nyingi mwandishi anapotumia chuku huwa hana lengo la kudanganya kwa kuwa akili ya binadamu ina uwezo wa kuchuja habari katika usemi hadi ukweli udhihirike. Kwa hivyo kwa muktadha wa lugha ya kila siku kuna maana ya kuongeza chumvi ama kuzidisha maelezo kuhusu kitu fulani. Tunapotumia chuku huwa tunaikuza au kuifanya ndogo sifa ya kitu fulani kuliko kilivyo katika hali ya kawaida. Kukuzwa huku au kudumishwa huku hufanywa kwa kupita kiasi. Kwa mfano kudunisha – msichana yule amevaa nguo fupi inayomtosha mtoto wa miaka mitatu.

Kukuza – Ana dhahabu inayoweza kujaa nyumba nzima.

Kwa kawaida chuku huwa ni tamathali ya usemi ya kusisitiza tu na haitumiki kudanganya. Hutilia mkazo hali au jambo ili jambo hili lijitokeze waziwazi kulingana na jinsi lilivyokuzwa au kudunishwa.

Wamitila (2003:194) anasema kuwa chuku inapotumika katika kazi ya sanaa sifa fulani kukihusu kitu fulani hukuzwa kupita kiasi. Kukuzwa huko kunaweza kuwa kwa udogo au ukubwa. Nia hasa ya kuitumia chuku ni kulifanya jambo fulani litokeze kwa uwazi zaidi kuikuza sifa fulani au kumfikirisha msomaji kwa kuona uzito uliopo. Anatoa mfano ‘alipoachwa na mpenzi wake, Sero alilia machozi ya ndoo nzima’ au ‘alikuwa tajiri aliyesifiwa na kila mtu lakini siku hizi hana chochote hata nzi hawamkaribii. Maoni ya Kuhenga (1977), Madumulla (2009) na msokile (1993) yanaoana na ya Wamitila na Wales.

Kauli tunazozishughulikia katika usemi tulioutambulisha kwa mkolezo hapo chini zina chuku. Kauli hizi zilizotiwa chumvi zinadhihirisha kuweko kwa msisitizo wa aina fulani. Kwa mfano:

Mweusi: Mzuka! Nitamzingua nimbandue abanduke bandu bandu. Mimi mzinguaji gwiji! Wembe ni ule ule uliomnyoa awali! Utatapikamadini na vyote ulivyokula kwenye madhabahu haya yetu. (uk 8)

Maana ya nje ya ‘mzinguaji gwiji’ ni kuwa Zinguo ni mtu mwenye uwezo au bingwa wa kusomea mtu kurani na kumwomba Mwenyezi Mungu ili asipate balaa au madhara. Bila shaka kwa kusoma tu kuwa Mweusi ni ‘mzinguaji gwiji’ hatufasiri maana inayojitokeza katika ulimwengu halisi wa kazi hii. Bila shaka kauli hii imetiwa chumvi kwamba Mweusi si mzinguaji wa kawaida tu ila ana uwezo mwingi wa kumwondoa Mweupe licha ya kuwa hataki kuondoka. Katika kauli hii tunamuona Zinguo akijigamba kwa sababu ya uongozi wake. Kwa hivyo kauli hii inarejelea sifa na tabia zake Zinguo. Anaona kuwa mbinu zake za uongozi zitamwezesha kupambana na Mzuka ambaye ana njama za kutoondoka Kusinyika. Anapomwambia ‘utatapika madini na vyote ulivyokula...’ ameongeza chumvi katika usemi huu kwani akitumia neno ‘utatoa’ au rejeshu’ kauli hiyo itakuwa ya kawaida. Matapishi ni kile kilichoingia tumboni ambacho hulazimika kutoka kwa kutopata mazingira yanayofaa. Mara nyingi huwa ni mazingira yaliyojaa. Katika ukiushi wa kauli hii tunaona kuwa Zinguo ana ufahamu kuwa Mzuka aliipora Kusinyika mali asili na kupeleka kwao mizukani. Kwa mfano madini, wanyama pori, vipuri vya wanyama na kadhalika. Matapishi huwa ni kitu ambacho hakifurahishi na hutoa harufu mbaya. Huwa hakuna yeyote anayefurahia kilichotapikwa kwani huwa

hakivutii machoni. Usemi huu katika ukiushi wake tunaona kuwa chochote ambacho Mzuka amekichukua kwa kumhadaa Mkusinyika hakiwezi kurudi katika hali kilivyochukuliwa. Mzuka ana haja ya kufaidika kutokana na maliasili ya Kusinyika na kwa hivyo haja yake ni kupata mazalisho ya nchi ya Kusinyika kwa bei rahisi na kisha kuyasafisha na kurudi kuyauza humo humo nchini kwa bei ya juu kuliko alivyonunua. Hii ni njama ya kibepari ambayo humfaidi binafsi na wachache ambao wanaunga njama zake mkono. Hali hii anaipenda Mzuka na Zinguo kwa kuwa katika upande wa watu wenye uwezo, wenye mali, wanaomiliki nyenzo na njia kuu za uzalishaji mali. Wakusinyika waliobaki ni masikini wasiokuwa na chochote, binadamu wnaonyonywa nguvu na jasho lao. Wakusinyika wameingizwa katika umasikini hali ambayo ni ukosefu wa pato na hasa kutokuwa na njia za kujikimu katika kupata mahitaji ya kimsingi ya maisha kama vile chakula, makazi, mavazi na mambo mengi ambayo ni haki ya binadamu ya kimsingi kama vile elimu, huduma za afya na kadhalika.

Katika usemi huu uliotiwa chumvi, msanii anaibua maudhui ya ulowezi na unyonyaji. Mkoloni alipoingia Afrika aligundua kuwa nchi za Afrika zilikuwa tajiri wa madini na mengineyo mengi yaliyomfaa kama bepari. Kuja kwake kulimfaidi kiasi kikubwa kwani aliupata utajiri wa Afrika haujaingiliwa na wanyakuzi. Hata sasa bado anafaidi kwani ameweza kuifanya Afrika kuwa tegemezi kiwango kuwa ni lazima Waafrika waendeleo kutegemea mikopo, misaada ya vyakula, dawa, teknolojia, elimu na hata mikakati ya kafanya maendeleo.

Mtoto 2: *(Akimsihi mwenzake) Tucheze kidogo zaidi. Labda hawajapata chochote! Njaa itatutafuna zaidi tukienda na matarajio makubwa.*
(uk 9)

Mtoto 2 anaposema ‘njaa itatutafuna zaidi tukienda na matarajio makubwa’ ana maana kuwa walikuwa na njaa kupita kiasi. Njaa hii ilikuwa kali na ingezidi kiwango cha kawaida. Njaa kwa kawaida haina meno na inaposemekana kuwa inatafuna, basi huwa imepita kiwango cha kuhimiliwa.

Watoto huwategemea wazazi kwa kila kitu. Mzungumzo waliyonayo watoto hawa ni ya kutilia shaka uwezo wa nchi wa kuwakimu raia wake kwa lishe bora na kwa hivyo afya njema. Bila shaka kiongozi; Zinguo: licha ya kuwa alikuwa amekabidhiwa madaraka na

uhuru na kufanywa kiongozi wa Kusinyika alilalamikiwa na wengi wakiwemo watoto kwani hawakuwa na lishe ingawa walikuwa huru. Bila shaka hii ilikuwa ishara ya uchochole. Chuku hii kwa hivyo inajenga taswira ya mambo yalivyo katika nchi ya Kusinyika. Maudhui ya umasikini yanaibukia hapa na kuendelezwa.

Hali hii ilithibitisha kuwa sekta ya kilimo imesambaratika kwani ndiyo uti wa mgongo wa nchi ya Kusinyika.

Mzuka: (*Taratibu*) Bado hujakua! Bado hujakomaana mbinu mufti za kujihami dhidi ya mibabe. Mizinga ya kukopesha. Mtandao huna! Angani hujafika. Elimu ya kupigana unayo? Mbinu zako zanuka! Dhaifu (*anatema*) (uk 15)

Babe ni jitu kubwa lenye nguvu: jitu, mtemi. Kauli hii ya Mzuka inaonyesha kwamba Kusinyika ilikuwa bado nchi changa ambayo ilihitaji uongozi wenye busara ili kufanikisha maendeleo. Maana ya juu ni kuwa mibabe ni watu walio na nguvu. Hii ni chuku kwa kuwa Mzuka angependa ahusudiwe na Zinguo kwa sababu ya uwezo wake mkubwa wa zana za vita, uchumi na hata katika viwango vinginevyo mbalimbali. Kwa hakika ufasili kimuktadha wa neno hili mibabe ni nchi zilizostawi na zenye uchumi uliostawi. Zinguo bado anatumia mbinu dhaifu alizofunzwa na Mzuka ambazo zimepitwa na wakati. Zinguo anatumia maji na vikuku. Kawaida maji hupatikana popote na yanaweza kupatikana na yeyote. Hali hii inayafanya maji kama silaha kuwa kitu cha kawaida ambacho yeyote anaweza kukitumia. Kulingana na Wamitila mbinu ya chuku yaweza kuwa ya kukuza au kudunisha. Kutia chumvi huku ni kwa kudunisha kiwango cha elimu ya sayansi ya Kusinyika ambayo Mzuka anajua bado ni ya chini na kwa hivyo anaposema. ‘mbinu zako zanuka! Dhaifu!’ katika ulimwengu wa hali halisi ni kwamba ujuzi wa Zinguo wa kutumia vikuku na maji ni mbinu zilizopitwa na wakati na kwa hivyo si kwamba zinatoa harufu, ni kwamba hazifai tena na hazitumiki katika ulimwengu wa sasa. Hapa, mbinu zimehusishwa na kitu kinachoweza kuoza kama vile chakula. Chakula kinapotoa harufu ya uozo bila shaka hakiwezi kukubalika tena kwa matumizi yoyote, hutupwa mbali. Kwa hivyo mbinu anazotumia Zinguo zimepitwa na wakati na kwa hivyo hazimtishi Mzuka. Huku ni kudunisha. Hata hivyo ni njia moja ya kumkejeli Zinguo ambaye ameshindwa kutumia raslimali ya Kusinyika kuiendeleza Kusinyika katika sekta zote za kuendeleza nchi.

Mzuka: Hujui kutumia raslimali yenu kujenga madhabahu dhabiti! Nchi inanuka umaskini. (uk 15)

Kauli ‘nchi inanuka umaskini’ ni kauli yenye chuku. Katika ulimwengu halisi tuna fasili kwamba kitu kinachonuka ni kitu kinachotoa harufu mbaya kwa sababu ya kuoza. Bila shaka kitu hiki huwa hakivutii na hakuna atakaye kusonga karibu nacho kwani husababisha kichefuchefu. Maelezo haya hayatupi ufasili kimatini. Katika muktadha wa matumizi ya chuku hii tunaona kuwa umasikini ulioko nchini kusinyika ni wa kiwango kisichokubalika. Kumbuka harufu mbaya husambaa kote kote. Kwa hivyo umasikini katika kusinyika umesambaa na kuwaathiri Wakusinyika wote. Bila shaka hali hii inatokana na uongozi mbaya wa Zinguo ambaye anaifyonza Kusinyika kwa kujilimbikizia mali n ahata kuiweka katika nchi za nje.

Kauli hii ya Mzuka inasisitiza ukweli kuwa Zingua ambaye ni kiongozi ameshindwa kuiongoza nchi kimaendeleo; hali anayosababisha umasikini ambao ni mojawapo wa maudhui yanayoibuliwa na kuendelezwa na chuku. Uongozi wa Zinguo ni uongozi mbaya na kwa hivyo umefikia kiwango ambacho hakiwezi kuvumilika tena. Ni uvundo mkali.

Zinguo: Panda madhabahuni ndipo mjue kuzingua Mzuka si jambo la kuchezeza. Huu si mchezo wa watoto. Ni kufa na kupona. (akishika tumbo) ndugu zangu mimi nimekuwa nikikeshwa hapa nanjaa. Siwezi kukataa kula au kunywa. Kwa hilo nisameheni. Nia ipo lakini tumbo langu tupu. Nala kidogo ili nijinusuru. (uk 20)

Zinguo anatia chumvi ujuzi wake wa uongozi wa nchi ya Kusinyika na kwa hivyo hakuna mwingine anayeweza kudhubutu kukabiliana na Mzuka. Huenda ni kweli kuwa ana ujuzi wa kukabiliana na Mzuka lakini si kweli kuwa ni yeye tu katika Kusinyika ambaye anaweza kumkabili Mzuka. Huenda Wanakusinyika wenzake wamenyimwa nafasi ya kuiongoza Kusinyika kujikomboa katika ukoloni mamboleo. Ili kuifasiri kauli hii iliyotiwa chumvi, muktadha wa usemi huu ni muhimu. Tunafahamu kuwa Zinguo hawaruhusu Wakusinyika kuwa na usemi katika maamuzi muhimu ya Kusinyika. Kwa hivyo ameitawala Kusinyika na kuifanya kuwa yake binafsi. Zinguo ni mtu wa kujitapa. Bila shaka hivi ni vitisho tu ili asiwe na pingamizi kutoka kwa Wakusinyika wenzake.

Kauli hii ya Zingua anaitoa baada ya kupewa zawadi kadha zikiwemo sukari, sharubati na mkate. Mzuka anayafanya haya ili kumrai Zinguo kukubaliana na hila za Mzuka za kutaka kuinyonya Kusinyika. Kwa kurejelea mawazo ya Wamitila(2003) chuku yaweza kutumiwa kuikuza sifa fulani kupita kiasi au kukuza huku kunaweza pia kuwa kwa udogo au kudunisha. Kauli hii ya Zunguo inaonyesha jinsi anavyomuabudu Mzuka kiwango cha kuamini kuwa hata kuwa naye na kugusana ni jambo la kimiujiza au ajabu ambalo lazima alifahamishe umma. Kwa hivyo tunapata fasiri kuwa Mzuka amejijweka katika hali ya juu na hali hii inatokana na kuwa anaweza kutekeleza mengi. Hali hii inamfanya Zinguo kumuona Mzuka kama Mungu na hata kuchukulia kuwa ni jambo la kujivunia kumkabili. Usemi huu unakamilika anaposema kuwa aliyoyatekeleza, yaani kumzingua Mzuka si mchezo wa watoto. Ni kufa na kupona.

Hii ni chuku kwani Zinguo anapokumbatiana na Mzuka ni sawa na kumsujudia. Anachukulia kwamba amepata nafasi ya pekee ya mahusiano na Mzuka. Hali hii ni ishara ya ushindi kwa Mzuka kwani Zinguo amekuwa zuge na kwa hivyo Mzuka anaweza kumtawala pasipo na wasiwasi. Mbali na haya tunapata chuku zaidi Zinguo anaposema kuwa “nala kidogo ili nijinusuru”. Kwa kweli huku kula kidogo si kidogo ila ni kinyume na njama zake za kutaka kushibisha tumbo lake. Katika kauli hizi maudhui ya unafiki na ufasidi yanaibuka. Zinguo anaonyesha unafiki kwa kuwa amewahadaa Wakusinyika kwa kukubali zawadi ndogo ndogo kama sukari, sharubati na mkate kinyume na mambo muhimu yanayoifaa Kusinyika. Ili kutimiza matakwa ya Mzuka anaanzisha utozaji ushuru akisingizia maendeleo. Wananchi wanatozwa ushuru wa kiwango cha juu ilhali hawana uwezo kwani sekta za kuzalisha mali kama vile biashara na kilimo zimesambaratika na kuwanyima pato.

Katika usemi ‘nala kidogo ili nijinusuru, kuna chuku. Katika ufasiri wa kauli hii, Zinguo anadogosha kiwango cha ushuru anaotaka kutoka kwa Wakusinyika. Kwa kweli kwa kuizingatia kauli hii tunaona kuwa hatuwezi kufasiri kimuktadha kuwa Zinguo anataka kidogo tu, ila ana lengo la kujilimbikizia mali kwa kusingizia kujinusuru. Katika matumizi ya kauli hii yenye chuku tunafasili kuwa Waafrika wamesawiriwa kuwa hawajapata ukombozi kamili. Udhalimu wa kitabaka ungali unaendelea kupitia ukoloni

mamboleo. Tumeona kuwa ukoloni mamboleo ni ile hali ya wakoloni kuendelea kuwanyanyasa na kuwadhulumu Waafrika kwa kuwatawala kupitia kwa tabaka la vibaraka Waafrika. Hapa mwafrika anasawiriwa kumsaliti Mwafrika mwenzake. Hali hii inajidhihirisha katika uchumi ambapo mahitaji na nguvu za mwafrika hutumiwa na mfumo wa kimataifa wa kibepari. Kauli hizi zinataka kuonyesha jinsi juhudi za ukombozi za Mwafrika zilivyosalitiwa.

Zinguo: Hawa ni mifupa. Vifyefye; kama kaukau kwenye kikaango.

Mzuka: Bado kuna wenye afya tele. (uk 21)

Kauli hii ya 'hawa ni mifupa. Vifyefye' ni kauli iliyotiwa chumvi. Katika matumizi ya ulimwengu halisi tunaweza kuchukulia mifupa kuwa kiunzi cha mifupa au gofu la mtu au hata mifupa mitupu. Tunapotathmini kauli hii katika hali yake ya matumizi halisi hatupati maana tuanyoitarajia. Lakini tunaporejlea muktadha tunatambua kuwa huu ni usemi unaibua chuku au kutia chumvi katika hali ya maisha ya Wakusinyika. Kitu ambacho kimegeuka na kuwa mifupa ni kitu kinachotisha machoni kwa yeyote akitazamacho. Hali hii inajenga picha ya mauti na maangamizi katika Kusinyika. Kauli hii kwa hivyo inaonyesha kuwa mfumo wa Kimizuka wa kuitawala Kusinyika hata baada ya kuipa Kusinyika uhuru ni wa dhulma na uliojaa unyonyaji na kuzidi kuvumilia mfumo huu kumewaangamiza wanajamii hii kiwango cha kubakia mifupa na vifyefye na kwa hivyo wamezidi kupatwa na taabu na mashaka mengi.

Kauli ya Zinguo inaonyesha hali waliyomo Wakusinyika licha ya Mzuka kumlazimisha kuwatoza ushuru mkubwa. Anaposema hawa ni mifupa, hana maana kuwa Wanakusinyika wamegeuka mifupa ila ana maana kuwa uwezo wao kiuchumi ni finyu na kwa hivyo hawana mali ya kuweza kutozwa ushuru mkubwa utakaomfaidi Zinguo na Mzuka. Ndio maana pato lao limekonda na kwa hivyo hawana minofu kutokana na hali zao za kiuchumi zilizosambaratika. Hali hii inamfanya Mzuka kumnyanyasa Zinguo pamoja na Wanakusinyika kwani Zinguo anafuata mbinu za kimizuka na kuishia kuwatoza Wakusinyika ushuru wa juu.

Zinguo: Tega

Mzuka: Nyingi kama...

Zinguo: (Akichekacheka) Changarawe.(uk 22)

Mzuka anapotega kitendawili “nyingi kama...” kisha Zinguo anamjibu ‘kama changarawe’ ana maana ya kumzindua Zinguo atambue njia nyingi za kumnyonya Mwanakusinyika kwa jina la ushuru. Miongoni mwa njia hizi ni kutozwa vitu ushuru katika viwango mbalimbali ili awe na pato kubwa. Kweli baada ya kuidhinisha njia hizi zote za kutoza ushuru anagundua kuwa ‘*vat isfat.*’ Anapiga kifua na kupiga ngumi ukuta bila kujua kuwa mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe.

Katika wimbo anaoimba Sichana kuna urudufu wa

madini yako wanyama wako fahari yako

maziwa yako kito

mito yako

anga yako je?

Katika kauli hizi kwenye wimbo huu kumejengwa uradidi wa kila kitu kuwa cha Zinguo. Hii ni chuku. Ametia chumvi kwa kutaja kila kitu kinachopatikana Kusinyika kuwa cha Zinguo licha ya Kusinyika kuwa na wana wake ambao wanafaa kuwa sawa mbele ya sheria zinazoiongoza Kusinyika. Matumizi haya ya chuku yanaibua maudhui ya ubinafsi. Kutoka mwanzoni tunamwona Zinguo mwenye kujijali na kutowajali wenzake. Anapokea mikate, sharubati na zawadi zinginezo kutoka kwa Mizuka bila kuwajali anaowaongoza. Mbali na hayo, anajiona kuwa yeye ndiye mwenye uwezo wa kuiongoza Kusinyika na hakuna mwingine. Anaposema kumkabili na hata kumkumbatia si kazi rahisi ni kauli inayomaanisha kuwa ni vigumu kuwa kiongozi na hali hiyo anataka ibakie miujiza kwa Wanakusinyika ambao bila shaka wamechoka na kuishi katika dhiki.

Sichana anasema katika wimbo ‘ujakazi ni wangu, ujira wangu japo mkonde natoa za utendaji.’ Sichana anaposema ujira wake mkonde ana maana kuwa malipo au mshahara anaopewa ni duni na hawezi kujikimu kwa ujira huo. Anaendelea kusema kuwa anatoa na za utendaji. Kauli hii ya Sichana katika wimbo anaoimba inathibitisha kuwa Sichana kama mfanyakazi ana malipo mabaya yasiyoweza kukidhi mahitaji yake mbali na hayo malipo duni, anatozwa ushuru na kumuacha katika hali mbaya zaidi ya umaskini huku akitegemewa na wazazi wake kwa mahitaji ya kimsingi. Huu ni mzigo mkubwa kwa Sichana ambaye umri wake ni mdogo; umri wa miaka kumi na sita tu. Kauli hii iliyotiwa chumvi inaibua na kuendeleza maudhui ya uzalendo. Tunamwona sichana akipambana kutimiza wajibu wake licha ya dhiki anazopitia kama mfanyikazi.

Kwa mapana wimbo huu unafunzwa shuleni. Hali hii inafanya madhila yajitokezayo kwenye wimbo huu kuwa malalamishi ya kila Wakusinyika kwani shule ni kiungo muhimu cha jamii ambacho huwa na jukumu la kuangaza macho na ufunguo wa maisha bora kwa jamii. Kauli hizi katika wimbo zinaibua maudhui ya uongozi mbaya ambao umeielekeza nchi kuwanyanyasa raia wake na kuwanyonya pato dogo walilionalo. Tamaa waliyonayo viongozi inawaelekeza kupata pato kubwa kupitia ushuru ambao wanawatoza wananchi waliochoka kwa kufanyishwa kazi bila mishahara ya kuridhisha. Zinguo anakiri haya anapozinguliwa na Mzuka. Anakiri kuwa Wakusinyika wana njaa na ukame, maradhi mengi na vilevile usafiri ni ghali na mgumu kutokana na barabara mbovu. Hiki ni chanzo cha wimbo huu uliobeba madhila wapitiayo Wakusinyika.

Katika mstari mmoja Sichana anasema ‘najisitiri kwa matawi.’ Bila shaka hii ni chuku. Haiwezekani katika hali halisi kuwa Sichana anafunika uchi wake kwa matawi. Lakini katika ukiushi wa kauli hii ni kwamba kutokana na hali yake ya kazi na ujira anaopewa pamoja na wale wautegemeo mshahara huu, hawezi kujinunulia nguo. Pato analopewa kama mshahara linategemewa na wengi na kwa hivyo inakuwa vugumu yeye kujinunulia nguo. Katika chuku hii maudhui yanayoibuliwa ni ya umaskini uliowakumba Wakusinyika. Hali yao kama wafanyakazi ni duni, hali ya wazazi wao vilevile ni duni na kwa jumla jamii nzima inaishi katika hali duni kwani wanaishi katika mazingira mabaya ambayo hayavumiliki.

Sichana: ...(*Akitafuta mwiba*) Naliwa na funza sijafa? Viatu ni ghali
Sichana. Ukinunua viatu mama na ndugu zako watazongwa nanjaa.
(uk 26)

Kauli hii inaonyesha Sichana ambaye anajiuliza swali lililojaa chuku ‘naliwa na funza sijafa?’ Katika hali halisi mtu hawezi kuliwa na funza huku angali hai. Kiukiushi Sichana analalamikia na kusikitikia mizigo aliyobebeshwa na viongozi wa Kusinyika ambao ni wabinafsi, wafisadi na wasiojali masilahi ya umma. Anadhihirisha kutozwa ushuru, kulipwa mishahara midogo, kutegemewa na wazazi ilhali pato lake ni dogo. Anajiuliza swali hili lililojaa chuku au kutiwa chumvi nyingi ili kumwonyesha msomaji makali ya madhila anayopitia huku walionavyo au mabwanyenye kwa mfano mwajiri wake

wakimtegemea kuruka hadi kiwango cha juu. Kwa hivyo huku kuliwa ni kunyanyaswa na walio na madaraka katika serikali ambao ni lazima wamtoze ushuru na katika kutozwa ushuru huo hawatimizi yanayofaa kutekelezwa na ushuru huo. Wakusinyika wanalalamikia kukosa elimu, afya na barabara nzuri.

Zinguo: Kuja huku! Nitajikaza kuwa nawe. (uk 28)

Katika ulimwengu halisi mtu ambaye ana mahaba na mwenzake hutaka kuwa naye kila wakati. Ikiwa kuna uvumilivu wa hali fulani basi huwa kuna tashiwishi. Katika hali dhahania ambayo ni hali kiushi, usemi huu umetiwa chumvi. Zinguo angeusema tu kwa kutumia maneno ya kawaida. Anaposema kuwa atajikaza, bila shaka anayerejelewa ana hitilafu fulani ambayo haimpendezi.

Kauli hii ni chuku ya kufanya kitu kiwe kidogo. Zinguo anaona kuwa Sichana si mwanamke wa hadhi yake, licha ya hayo anajishawishi akilini na kumnajisi ili kujiondolea uchu wa mapenzi. Maudhui yanayoibuka hapa ni uzinzi au uasherati. Uasherati unadhahirika kama ukosefu wa maadili miongoni mwa wanajamii. Katika jamii nyingi za Kiafrika, uasherati ni kitendo ambacho hushusha hadhi ya mwanamke pasipo kumhusisha mwanamume. Zinguo ni mtu na mkewe lakini anamkosea mkewe heshima kwa kufanya tendo la ndoa nje ya ndoa yake rasmi. Anapotaka kumwelezea Kaza kuhusu alivyojitakasa kwa kumtumia sichana, Kaza hafurahishwi na kitendo hiki kwani anamwona kama aliyekengeuka na kufuata tabia za wakoloni.

Zinguo: Ati umaskini unazidi!

Watu kula panya na matunda ya msitu, na Mungu amewapa bure bilashi.

Kaza: Kesho watatuingilia na nyumbani kwakekwa wake zetu! (uk 31-32)

Zinguo anatia chumvi kauli yake anaposema ‘watu kula panya na matunda ya msitu na Mungu amewapa bure bilashi’. Bila shaka anazungumzia vyakula wanavyotegemea Wakusinyika katika dhiki walizonazo. Usemi wake una kinaya ingawa unajaribu kufanya hali ya kuwepo na njaa Kusinyika kuonekana kuwa si ya kuleta hali ya wasiwasi. Athari iliyoko ya njaa kwa kuonyesha kuwa aghalabu kuna cha kutia mdomoni. Hali hii

inaonyesha kuwa Zinguo ni kiongozi aliyetosheka na uhuru wa bendera tu ambao anauchukulia kuwa mwanzo na mwisho wa kila kitu. Anakosa kutambua kuwa baada ya uhuru kunakuwa na jukumu la kujenga taifa, na pia utamaduni wa Mkusinyika lazima udumishwe. Na kwa hivyo Zinguo amepuuza wajibu wake wa kufanya kazi na kuzalisha mali na hata kukuza vyakula huku wakingoja kwenda ng'ambo kuombaomba misaada. Kwa hivyo athari za mkoloni alizonazo Zinguo zimemfanya kukengeuka na hata kusahau utamaduni wake. Vyakula anavyotaja kuwa viliwe na Wakusinyika havipo katika utamaduni huu licha ya Mungu kuviweka duniani bure bilashi. Kwa hivyo kauli hii inathibitisha wazo kuwa Zinguo yumo katika kiza cha kutoyaelewa matatizo yanayoikumba Kusinyika.

Kaza ambaye ni kibaraka cha Zinguo anaonyesha kutopenda kwake tabia ya Mzuka ya kuendelea kutaka kuingilia uendeshaji wa Kusinyika. Kauli yake ' kesho watatuingilia na nyumbani kwa wake zetu' ina maana kuwa tabia ya mkoloni haina kikomo vilevile hawaheshimu haki za binadamu wengine. Zinguo pamoja na Kaza ni viongozi wanaojitakia makuu na hawajali maslahi ya wengine. 'Kuingilia na nyumbani kwa wake zetu' kuna maana kuwa mkoloni ana haja ya kutaka kujua siri za ndani ya nchi ya Kusinyika ili atoe mwelekeo au kupendekeza suluhisho la matatizo ambayo yanafaa kushughulikiwa kindani. Mkoloni anapofanya hivi anafanya kwa manufaa yake mwenyewe.

Umati: Ha ha ha ha!

Mtu 1: (*Bila kulazimishwa*) Piteni mwende! Piteni mdiriki kula hiyo tamu inayowatekenya.Ndio maana mnatucheka kupinda migongo. Ubikira wa nchi yetu....
Iwapo umri hauujui historia basi miaka ni ya nini? (uk 33)

'Piteni mdiriki kula hiyo tamu inayowatekerenya' ni kauli iliyotiwa chumvi. Katika ulimwengu halisi kauli hii itaandamana na vyakula ambapo hatuwezi kupata maana halisi kifasihi tunavyotarajia. Katika ukiushi wake kauli hii itamaanisha kuwa Wakusinyika wanaofurahia uongozi wa Zingua ni sharti wachukue tahadhari ili wasiendeele kutumbukia katika matatizo ya uongozi mbaya ambao Zinguo ameurithi kutoka kwa

Mzuka. Kauli hii inazua maudhui ya uwajibikaji au uzalendo. Mtu 1 anaonyesha uzalendo kwani hataki kuiona nchi ikitumbukia katika uongozi mbaya. Anapigania haki yake na kwa hivyo tahadhari anayoitoa ni ya kuwafungua Wakusinyika macho.

Aidha, Mtu 1 na Mtu 2 ni Wanakusinyika ambao walioonja enzi za ukoloni mkongwe na sasa wanapitia hali ya maisha ya ukoloni mamboleo. Hali ya uongozi uliopo haiwaridhishi na kwa hivyo wameonelea kuwa ni jukumu lao kuwazindua Wakusinyika kuanza kupigania haki yao upya. Zinguo anaipotosha nchi kwa kuitumbukiza katika umaskini, njaa, ufisadi, unyakuzi wa ardhi kwa kumsimgizia Mzuka. Jukumu lao katika kazi hii ni kuunganisha nyakati hizi mbili. Wana lengo la kuleta umoja. Mtu 1 anaposema:

Mtu 1: Mnatucheka kweli sisi punguani
 Ndio maana mnatucheka kupinda migongo

Kauli ‘mnatucheka kweli sisi punguani’ ni kauli yenye chuku. Katika hali halisi ni kawaida mtu aliye na akili punguani kuchekwa kutokana na vitendo vyake visivyoambatana na vya binadamu aliye na akili timamu. Kulingana na muktadha wa matumizi ya kauli hii tunafasili kuwa Mtu 1 anatajiriba ya uongozi wa nyakati zote mbili; wakati wa ukoloni mkongwe na wakati wa ukoloni mamboleo. Hali hii inawafanya kuwa na ufahamu wa historia ya uongozi wa Kusinyika wa Zinguo na mtangulizi wake; mkoloni. Mtu 1 kwa hivyo ana nafasi bora ya kuwasimuli Wakusinyika ya kale na ya sasa na kutoa mwelekeo mwafaka wa kuikomboa kusinyika kutoka mikononi mwa viongozi wadhalmu haswa wale waliochukua hatamu baada ya mkoloni kuondoka. Kwa hivyo Mtu 1 anachekwa kwa sababu ya umiri wake. Kupinda mgongo ni ‘uzee’ au kuwa na umri mkubwa. Katika kupinda mgongo huku ana maana ya kula chumvi nyingi. Hali hii kwa hivyo inampa uwezo au jukumu la kupitisha historia ya uongozi wa kusinyika kwa kizazi kipya ambao ni vijana.

Bila shaka kauli hizi zimetiliwa chumvi. Fasili wanayotaka kupitisha ni kuwa aliyotenda Mzuka si mambo ya kufanyiwa mzaha. Kwa hivyo mabaya ya Mzuka wanayajua kwa kuwa waliyashuhudia. Kizazi cha sasa hakielewi haya ndiyo maana wanawacheka kiwango cha migongo kupinda. Huku si kucheka kwa kawaida.

Katika hali kiushi kucheka huku kunaashiria ujinga wa vijana wa kukosa kudadisi chanzo cha matatizo yaliyoko. Vijana wana udhaifu wa kuwahusudu wanasisia na kutimiza matakwa ya viongozi hao katika hali pofu. Kumbukumbu za mienendo ya Mzuka zinamfanya Mtu 1 kuutahadharisha umati kwani Zinguo naye ana silisili za Mzuka anayejifanya ameondoka na kumbe yupo.

Zinguo: ...Ni mawazo ndugu zangu. Kuzingua mizuka kunataka ufumbe macho uwaze na macho ya ndani...

Zinguo: Zinguo awafie kwa kuwabebea mizigo yenu! Msifikiri napenda ukuhani saana.

Katika kauli ‘kuzingua mizuka kunataka ufumbe macho na uwaze na macho ya ndani...’ kuna chuku. Tunachukulia hivyo kutokana na hali ya kuwaza na macho ya ndani. Katika matumizi halisi ya kauli hii utiaji chumvi kwenye kauli hii unajitokeza Zinguo anaposema kuwa kuzingua mizuka kunamhitaji kuwaza kwa macho ya ndani. Hali hii inadhihirisha kuwa Zinguo anamfahamu Mzuka na kwa hivyo si kweli kuwa ayatendayo anayatenda kwa kutojua. Ana uelewa wa hila za Mzuka na kwa hivyo anahitaji juhudi zake binafsi na kuungwa mkono na wakusinyika kisha mambo yatakuwa sawa.

Zinguo anatia chumvi swala la kuingoza Kusinyika. Huenda ni kweli kwamba ili kuiongoza Kusinyika kunahitaji ujuzi mwingi. Kwa hivyo anachoashiria Zinguo ni kuwa kuiongoza nchi ya Kusinyika bila athari ya kimizuka si swala rahisi. Vilevile Zinguo anajigamba na kuwaambia Wakusinyika kuwa hakuna mwingine ambaye anaweza kuwa na ujuzi huu isipokuwa yeye. Katika chuku tunayoirejelea kiukiushi hapa, tunakumbana na maudhui ya maana ya uhuru. Zinguo alikuwa kiongozi mpya baada ya Mzuka kuondoka. Hata hivyo Mzuka hakuondoka kabisa na kwa hivyo uhuru alioutoa ulikuwa kijisababu tu. Zinguo akiwa kiongozi aliyeachiwa cheo na mkoloni alikosa uwezo wa kuliendesha taifa na kwa hivyo anamsingizia Mzuka.

Katika sehemu inayofuata Zinguo anaitaja hadhira kunung’unika. Anasema ‘mnatarajia Zinguo awapigania. Zinguo awafie kwa kuwabebea mizigo yenu.’ Ukweli ni kwamba Wakusinyika wamegundua ukoloni mamboleo katika uongozi wa Zinguo na kwa hivyo wameamuka na kutaka atekeleze wajibu wake. Wanapigania haki yao ili waongozwe vyema kupitia madhabahu aliyoachiwa Zinguo.

Katika kufasiri chuku hii Zinguo aliyeshindwa kuyatekeleza majukumu yake anaonelea kuwa hafai kubeba mizigo ya Kusinyika na kuwa si jukumu lake kuipa Kusinyika mwelekeo na kwa hivyo shida za Kusinyika hazimhusu. Zinguo analalamika kuwa hadhira isifikiri anapenda ukuhani sana. Kauli hii inadhahirisha kuwa Zinguo ni mnafiki na kweli hana mipango ya kuachia uongozi. Aidha si mzalendo kwani angekuwa anaipenda nchi yake, angitumikia bila kulalamika.

Katika chuku tuliyoitambulisha kwa mkolezo hapa chini katika usemi wake Zinguo, kuna kiwango kikubwa cha Zinguo kueleza makossa yaka kuwa madogo na ambayo yanahitaji msamaha kutoka kwa Wakusinyika. Hii ni chuku ya kudunisha kitu kikubwa kuonekana kidogo.

Zinguo: (*Akijitia ujasiri*) Kosa dogo tu ndugu zangu. Kuteleza sio kuanguka (*kwa kurai*)
Nyinyi nipeni fursa ya tatu mwone nitakavyomfanya huyo Mzuka.
Nitamtia humu(*anakunja konzi*)
Msichoke katu!
Zinguo ana funguo nyingi na atafungua kila mahali, kufichua janja ya huyu nduli,(uk 43)

Kauli hii ‘kosa dogo tu’ imetiwa chumvi. Hii ni chuku ya kudunisha au kufanya kitu kuonekana kidogo. Zinguo anajua kuwa yeye kama kiongozi aliyechukua hatamu baada ya mkoloni, hapendwi na wengi. Anajua kuwa chanzo cha mateso wanayopitia Wakusinyika ni yeye na kwa hivyo lazima atafute njia ya kupunguza ubaya wake ambao wanakusinyika wameuona. Tunaona tayari ameshaongoza kwa mihula miwili na hakuna mafanikio waliyoona Wakusinyika.

Ili kuwarai Wakusinyika wamchague, anatoongoza kwa maneno matamu kuwa ana funguo nyingi na kwa hivyo atafungua kila mahali kufichua janja za huyu nduli (Mzuka).

Kwa kusema kuwa ana funguo nyingi anarejelea ujuzi wake wa kuendesha nchi na kusuluhisha matatizo ambayo miongoni mwao ni kukabiliana na hila za mkoloni. Mzuka tayari ameshindwa na mbinu zake katika mihula miwili iliyotangulia.

2.3 Tashbihi

Wamitila (2003:39) anasema tashbihi ni ulinganishi wa moja kwa moja. Anatoa ulinganishi kwa mfano; *Juma ni mkali kama simba* na *Farida anaimba kama kasuku*. Anaendelea kusema kuwa ulinganishi huu hudhamiria kuisisitiza sifa fulani na pia kutujengea picha ya aina fulani akilini. Vilevile ulinganishi huu unaonyeshwa kwa matumizi ya viungio : kama, mfano wa, sawa na, kama vile, mithili ya, tamthili ya , ja (katika ushairi) na kadhalika. Mohamed (1995), Ruhumba (2001) na Kuhenga (1977) wana maoni sawa na Wamitila.

Leech (1965:156) anasema ulinganisho huu wa vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti hubainisha maana kwa njia iliyo wazi kabisa.

Kwa hivyo kwa kushughulikia tashbihi wasanii wameshughulikia mambo makuu matatu ambayo ni **kizungumziwa**, **kifananishi** na **kiungo**. Kizungumziwa ni kitu halisi ambacho huzungumzwa na kitu kinachofananishwa kwa fumbo. Kifananishi kipo katika mawazo na huzingatia maana dhahania na kiungo ni sifa zipatikanazo katika kitu kinachozungumzwa. Kazi yake kuu ni kuhusisha vitu vyote viwili katika kuunda maana kama inavyoonekana katika mifano tuliyotoa hapo juu.

Wamitila(2003:193) anasema kuwa huu ni ulinganishi wa moja kwa moja kwa mfano *Juma ni mkali kama simba*. Ulinganishi huu unadhamiriwa kuisisitiza sifa fulani na pia kutujengea picha ya aina fulani akilini. Ulinganishi huu unaonyeshwa kwa viungio kama alivyotaja Msokile. Kwa hivyo Msokile na Wamitila wana maoni sawa. Tamthilia ya *Zinguo la Mzuka* imetumia tashbihi kwa kiwango kikubwa.

Sauti: Sisi kama maji hufuata mkondo. (uk 14)

Maana asili ya kauli ‘sisi kama maji hufuata mkondo’ ni hali ya maji kufuata njia yake. Maana ya tashbihi hii katika ulimwengu halisi wa matumizi yake haijitokezi. Lakini katika ulimwengu dhahania wa kazi hii, tunapata ufasiri tofauti kabisa kulingana na muktadha wa matumizi wa kauli hii. Anayetoa kauli hii bila shaka anataka kuonyesha uongozi wa kidikteta alionao Zinguo. Kiongozi huyu hawachukulii Wanakusinyika wenzake kama binadamu. Amewadharau na kuwaweka katika kundi la watu ambao wanafaa kutawaliwa tu na hawana uhuru wa kusema wala nafasi ya kujadiliana na viongozi jinsi ambavyo wangependa kuongozwa. Kwa hivyo tukitafakari kulingana na

muktadha wa tamthilia hii tunaona kuwa Wakusinyika walikuwa wamechoka na jinsi walivyoongozwa na Waafrika waliochukua uongozi kutoka kwa Wakoloni. Tabaka zima la viongozi wapya waliorithi nafasi zilizoachwa na Wakoloni baada ya uhuru lilikua na tabia au sifa za uchoyo, ufisadi, ubinafsi, wizi wa mali ya umma ili kujilimbikizia mtu kibinafsi, kujitakia makuu na kutojali maslahi ya wengine pamoja na kukwamilia madarakani. Viongozi hawa waliwanyima Wakusinyika nafasi kutagusana nao. Kwa hivyo Wanakusinyika wamegundua kuwa baada ya kupata uhuru wa bendera, uhuru ule ulikuwa ni wa bandia. Viongozi hawa kwanza hawakujua la kufanya katika madaraka yao mapya. Sauti inayotoa kauli bila shaka inaelewa kuwa mkoloni alikuwa amewarubuni na kuwa hajaondoka ila alijigeuza umbo kwa kuwaambukiza viongozo waliochukua hatamu tabia za Kimizuka; chanzo cha ukoloni mamboleo.

Kauli hii inayosemwa na mhusikahuyu natuonyesha unafiki wa kiongozi huyu; Zinguo. Alikuwa akijisifu kuwa alimfahamu mkoloni na sifa zake zote na hata siri zake zote. Hali hii ni tata kwa kuwa iwapo kweli alimwelewa mkoloni, alishindwa kutumia ujuzi huo kumwondoa mkoloni kabisa na kuangamiza athari zake zote. Zinguo alisalitika na hila za mkoloni akadanganyika kiasi cha kuuza uhuru wake kwa kutimiza utashi wa Mkoloni bila kujua. Vilevile hakutafuta maarifa ya kumpigia mkoloni.

Katika hali hii Zinguo ameonyesha ubinafsi na kutowashirikisha Wakusinyika katika uamuzi wa maswala muhimu ya kuiongoza nchi. Anapolemewa na mbinu za Mzuka za kuendelea kutimizwa anayotaka, anairejelea hadhira ambayo ni umma walionyanyaswa naye na wamemgundua kuwa yeye; Zinguo, anayekataa kuwashirikisha katika uongozi na kwa vile anajifanyia mambo yote yeye, Wanakusinyika hawana budi kuendelea kuamuliwa mambo naye.

Zinguo: Hawa ni mifupa. Vifyefye, kama kaukau kwenye kikaango. (uk 20)
Kifyefye ni uchane wa ubua. Ubua nao ni kipande cha shina la mmea wa mtama au mhindi kilicho chepesi sana. Kaukau nacho ni ni chakula cha kuvunjika kwa urahisi. Kavuu. Kauli hii katika ulimwengu dhahania tunapata fasili ifuatayo:
Ukiushi unaojitokeza katika tashbihi ‘Vifyefye, kama kaukau kwenye kikaango’ ni kuwa katika uhusiano wa mkoloni na mtawaliwa, dhamira kubwa ya mkoloni huwa ni kuyanyonya mataifa machanga kiuchumi. Mzuka na athari zake anamfanya Zinguo

kuwatoza Wakusinyika ushuru wa kiwango cha juu. Viazi viwekwapo kwenye kikaango huwa vina majimaji na umbo lake huwa ni mvingo. Baada ya kuchomwa na mafuta yaliyo moto viazi hivi hunyauka na kukauka na huishia kuwa kavu. Wakusinyika tayari ni wachache wa pato na uchumi wao ni wa kiwango duni. Hawana kazi, sekta ya kilimo imesambaratika na vilevile wameshindwa kuyamudu maisha kwani wanaishi maisha ya kijungumeko. Katika kauli ‘vifyefye, kama kaukau kwenye kikaango’ ni kauli inayojenga taswira ya dhiki, mateso na unyanyasaji wanayopitia katika Kusinyika iliyo huru. Wamenyonywa na kuachwa bila chochote na Wazungu Weusi ambao ni Waafrika waliochukua hatamu za uongozi na Mkoloni aliyemtawala. Uhuru huu hauna maana kwao kwani afya yao ni mbaya, hawana lishe bora na kwa hivyo wanazidi kupata mateso ya kuzidi kuchomwa kama kaukau kwenye kikaango. Kauli hii inaibua maudhui ya ukoloni mamboleo. Utozaji ushuru ni mbinu ya mkoloni ya kumnyanyasa mnyonge ili kujinufaisha yeye binafsi. Zinguo anaitumia mbinu hii hata baada ya mkoloni kuondoka na kulijaza tumbo lake. Mzuka ana haja ya kuudhibiti na kuusimamia ule mfumo wa uchumi wa mataifa machanga kwa kutoa mikopo, viwanda, biashara na Nyanja zingine mbalimbali za kiuchumi. Haya yote mwananchi wa kawaida ndiye anayelipa. Aidha haya yote ni kwa manufaa yake binafsi kama bwanjenje. Mbinu hizi za mkoloni alizojifunza Zinguo zinawaacha Wakusinyika katika hali mbaya kiuchumi ambayo ni njia moja ya kuwakandamiza.

2.4 Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyukuwa hai au vyenye uhai huwasilishwa au kusawiriwa kwa namna iliyosawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi. Aghalabu tamathali hii hutumiwa pia kurejelea sifa ya kuwapa wanyama sifa za kibinadamu na huwa na dhima ya kutilia mkazo wazo au jambo fulani.

Wamitila(2003:194) ana maelezo kuwa ni hali ambapo kitu kisichokuwa na uhai au uwezo wa kuhisi (urazini au ung’amuzi) wa kibinadamu kinapewa sifa hiyo. Wamitila anaendelea kusema kuwa hali hii huipa kazi ya kisanaa mvuto. Vilevile tashihisi huweza kutumiwa ili kuleta athari fulani ya kihisia. Anatoa mfano: *miti ilimuinamia na kumsalimu alipoingia kwao kwa mara yakwanza baada ya kutoka vitani au bahari ulifuka kwa hasira kubwa na kuifanya safari yetu kuwangumu.*

Utafiti wetu umelenga jinsi tamathali hii ya usemi ya tashihisi ilivyotumika katika hali kiushi ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui mbali na kuyaibua.

Mtoto 1: Tumejaribu kuifukuza hii njaa kwa kucheza. Haiendi. Inatuangalia tu.

Mtoto2: (Akimsihi mwenzake) Tucheze kidogo zaidi. Njaa itatutafuna zaidi tukienda na matarajio makubwa. (uk 9)

Katika ulimwengu halisi tukisema tumejaribu kuifukuza hii njaa kwa kucheza na haiendi ni sawa na kusema tunakimbizana na njaa unyonyo. Kamusi ya Karne ya ishirini na moja (2013) inatoa maana ya njaa kuwa ni hisi ya ukosefu wa chakula tumboni au uhaba mkubwa wa chakula. Njaa imepewa uwezo wa kuwa na mwendo na hata kujihusisha katika kufukuzana na watoto. Hii ni sifa ya binadamu au mnyama. Katika ulimwengu halisi wa matumizi ya maneno haya si kawaida kuona matendo kama haya. Mbali na haya njaa imepewa uwezo wa kuwa na macho “inatuangalia tu”. Huu ni uhuishi. Vitendo hivi vya neno njaa, vimetiwa uhai ili kutilia mkazo dhiki waliyopitia watoto kutokana na ukosefu wa chakula. Kusinyika ni nchi iliyopata uhuru na kwa hivyo, ina uwezo wa kujiendesha. Ni jambo la kusikitisha na kuvunja moyo kuwa watoto ambao ni Kusinyika ya baadaye wanapitia madhila ya kuhangaishwa na njaa badala ya kufurahia utoto wao na kuwa vyema ili wawe watoto ambao wanajiweza kimwili. Kwa kutoa kauli hii, wanadhiki uongozi wa Kusinyika ambao umeshindwa kuwalea watoto wao. Kauli hii ya tashihisi inatilia shaka maana ya uhuru waliopata kutoka kwa mkoloni na kwa hivyo kujenga taswira ya udhaifu wa uongozi uliochukua hatamu baada ya Mwafrika kupigania uhuru.

Mtoto 2 anasema ‘njaa itatutafuna zaidi na hawana haja ya kuenda nyumbani’. Kauli hii inaonyesha kuwa uwezo wa wazazi wa kuwalisha watoto kutokana na pato walilopewa kule vibaruani lilikua dogo na kwa hivyo kuwafanya wawe na maisha ya kijungumeko.

Maudhui yanayoibuliwa hapa ni ya umaskini, haki za watoto na malezi. Uhuru wa Kusinyika haujawapa Wakusinyika faida yoyote ila kwa wachache walio na vyeo serekalini na wakaribu wa Zinguo. Umasikini huo ndio unapelekea watoto kupewa malezi duni ambapo mahitaji ya kimsingi kama chakula hayapatikani. Licha ya wazazi

wa watoto hawa kufanya vibarua, wameishia kuishi maisha ya vijungumeko na hawana akiba yoyote. Hali ambayo ni hatari kwa maisha ya baadaye ya watoto hawa ambao ni Kusinyika ya baadaye, kwani wataishi kuwa wategemezi wa tabaka la juu ambalo ni la akina Zinguo na Mzuka. Kauli hizi za watoto vilevile zinaibua maudhui ya uongozi mbaya uliojaa ufisadi, ukabila, ubinafsi na unyanyasaji. Unamuonyesha Zinguo kama kiongozi aliye dhaifu, asiyewajibika na kutojali Wakusinyika kwani hawapi mwelekeo mzuri wa kuzalisha mali Kusinyika ikiwemo kilimo. Ukosefu wa mwelekeo kama huu kutoka kwake umefanya sekta zote kusambaratika na kwa hivyo kuiangamiza nchi.

Mzuka: Mvi huona mbali; fungua macho utazame.

Zinguo: Naogopa kupora mama yangu, sijui watoto wetu baadaye watakuaje! (uk 23)

Katika sehemu hii tungependa kutathmini kauli ‘mvi huona mbali’. Maneno haya yanasemwa na Mzuka. Mzuka amempa Zinguo maarifa ya kupata mali kutoka kwa wananchi ambao ni vifyefye. Mzuka kwa hivyo anajitapa kuwa amebobea katika mambo hayo kutokana na tajiriba aliyonayo. Kwa hivyo Mzuka anaona kuwa ana maarifa ya kumpa Zinguo ili kuzalisha mali kutokana na ushuru wanaotozwa Wanakusinyika. Zinguo anatumia maarifa haya ya kimizuka na kupata fedha za kutosha katika hazina yake baada ya kumwamrisha Kaza kukusanya ushuru bila kupoteza hata kidogo.

Kwa njia nyingine kauli hii ni ya kumtahadharisha Zinguo kumakinika kwani kitendo chake cha kuwatoza Wakusinyika ushuru mkubwa ni cha kuwanyanyasa na kuwanyonya Wakusinyika. Kwa hivyo, ni vizuri akichukua tahadhari kwani Wakusinyika wakimgeuka bila shaka atapoteza amani aliyonayo. Tahadhari hii inachukuliwa na Zinguo vibaya kwani hataki kuelekezwa na anajiona amebobea maarifa ya kuiongoza Kusinyika hata kama ni kuwakandamiza Wakusinyika. Ushuru huu waliotozwa Wakusinyika unahitaji kuelekezwa katika maendeleo ya nchi. Zinguo amechukua pato hili la taifa na kutumia kwa mahitaji yake binafsi na hata kuweka masalio katika nchi za kwa Mizuka. Tashihisi hii kiukiushi inaendeleza maudhui ya ubadhirifu wa mali ya pato la Wakusinyika. Fedha hizi anazokula Zinguo zinafaa kutoa elimu kwa watoto wa Kusinyika, kujenga vituo vya afya, kutengeza barabara na kuimarisha taasisi zingine muhimu za kuwatunza Wakusinyika. Haya anayataja Zinguo mwenyewe anapofunzwa mbinu za kupata mtaji na Mzuka. Yote haya ni mambo Zinguo kama kiongozi anayajua kwani kabla hajaanza

kuwatoza Wakusinyika ushuru katika viwango mbali mbali vya uchumi anakiri kuwa anajua matatizo wanayopitia lakini inawabidi watoe kitu kidogo ale. Matumizi haya ya tashihishi kwa hivyo yanaibua maudhui ya uongozi mbaya uliojaa ufidia ambao hauna mwelekeo kwani pato la kitaifa la Kusinyika linaishia katika mifuko ya wachache huku wengi wakiathirika. Mbali haya Zinguo anasema kuwa anaogopa kumpora mama yake. Mama hapa ni neno linalorejelea nchi ya Kusinyika. Huu ni uhuishaji. Mapato yote anayochukua Mzuka yanatoka Kusinyika. Dhana ya neno mama huwa ni kuendeleza kizazi au kuzaa. Katika hali hii tunarejelea mali iliyomo Kusinyika.

Sichana: Ujakazi ni wangu

Ujira wangu japo mkonde (uk 26)

Katika kauli hii anaibua madhila anayopitia kama kijakazi. Katika maana halisi ya maneno haya bila shaka ni hali ya ujira kuwa mwembamba au malipo au mshahara usioweza kukidhi mahitaji yake. Katika hali kiushi kulingana na muktadha ambao wimbo unaimbwa, mwimbaji analalamikia hali ya mshahara duni licha ya yeye kutimiza wajibu kwa moyo mkunjufu na kwa uzalendo. Mshahara huu hauwezi kutosheleza mahitaji yake. Mbali na kutotimiza haya, analipa ushuru, ishara ya mzigo zaidi aliobebeshwa na viongozi wenye silisili za ukoloni mamboleo. Kwa jumla wimbo huu una jukumu la kumzindua Zinguo kimawazo. Lakini Zinguo hapendezwi na anayoyasikia kutoka kwa Sichana. Anamkemea.

Sichana: Tulifundishwa shuleni!

Zinguo: Basi hizo ni shule jinga! Walimu wake ni majinuni (uk 27)

Katika kauli ‘basi hizo ni shule jinga!’ kuna uhuishi. Shule imepewa sifa ya kibinadamu ya kuwa na udhifu wa kutojua kitu fulani. Kwa kuitathmini kauli hii kimuktadha tunatambua malengo aliyonayo Zinguo.

Katika hali hii mkengeuko umeibukia katika kauli anazotoa Zinguo. Mtu akiwa amekengeuka basi huwa amezuzuka, amefuata na kuamini jambo lisilo la kweli. Mara nyingi mkengeufu huwa ameamini na kufuata njia au tabia potovu na yenye kumpoteza kimaisha. Ule uzuzu humtenganisha mtu na nafsi yake ya kweli na kumfanya avae nafsi ya kinafiki. Tunamuona Zinguo amekengeuka kutokana na kauli hii. Kama kiongozi aliyechukuwa hatamu baada ya ukoloni, tunamtarajia kuimarisha taasisi zote ikiwemo ya elimu ili kuboresha maisha ya Wakusinyika. Mawazo yaliyoko kwenye wimbo ni

malalamishi ya umma (Wanakusinyika wenye tabaka la chini). Zinguo anatumia mbinu za Kimizuka kwani yote ayafanyayo ni kwa manufaa yake mwenyewe na ya Wamizuka kwani anataka wamsujudie, amegeuka Mzungu Mweusi na kutengana na jamii yake ya Kiafrika kabisa. Anatumia maisha ya anasa; anamnjisi Sichana. Anataka utukufu na heshima za kibinafsi bila kujali hali ya jamii inayomtegemea kama kiongozi. Sababu ya hili ni kuwa Zinguo amekengeuka na hata kutofahamu muundo, shabaha na mahitaji ya jamii nzima anamoishi. Vilevile amekosa kutambua uzalendo ni nini au jukumu lake kwa taifa lake. Hali hii inamfanya Zinguo kumnajisi Sichana kwa kisingizio kuwa mkewe hayupo.

2.5 Kejeli

Kejeli ni mbinu pana, ambayo huchukua nafasi kubwa na kutoa mchango wake si katika mazungumzo tu bali pia katika utoaji wa mawazo yetu ya kila siku. Katika fasihi, mbinu ya kejeli imetumiwa na inaendelea kutumiwa na waandishi ili kuwezesha hadhira au wasomaji wafikirie kwa undani swala linaloonelewa ili waweze kupata ujumbe uliokusudiwa kufikishwa kwao. Wamitila (2008:395) anasema kuwa kinaya au kejeli ni tamathali ya usemi ambayo inahusisha ukinzani kati ya hali ilivyo na inavyosemekana kuwa. Wamitila anaendelea kusema kuwa kinaya hujengwa kwenye msingi wa kuwepo na msigano au mgongano fulani kati ya hali halisi na matarajio ya wanaohusika. Wamitila akimrejelea Gibbs anasema kuwa katika msingi huu inahalisi kusema kuwa kinaya si tu swala la lugha au balagha bali pia huhusisha akili au ubongo kwa kiasi kikubwa.

Mbatiah (2001:27) anasema kejeli ni maneno yanayotumika katika matamshi na ambayo huwa ni maneno ya kuchoma, kukata na kutia uchungu. Mbatiah anaendelea kusema kuwa ingawa kejeli huchukuliwa kisawe cha kinaya, inafaa kuisitiza kuwa kejeli ni aina ya kinaya yenye ukali wa kipekee. Kwa hivyo kinaya huwa na jukumu la kutoa maana, kinyume na kinachosemwa kwa ajili ya kuonya, kushutumu au kumtweza mtu.

Kuhenga (1977) anakubaliana na Mbatiah. Naye anasema kejeli ni usemi wa kimafumbo ambao humuudhi mtu kwa nia ya kumuonya kichinichini bila ya bughudha. Tamthilia tulizochagua zimejikita katika dhana ya kejeli. Kejeli katika tamthilia hizi imetumika

kuielezea historia ya nchi nyingi za kiasia ikiwemo Kenya kuanzia kabla ya uhuru, baada ya uhuru na hata hivi sasa. Kwa hakika kazi tulizoteua zinaelezea kimaudhui mwelekeo wa nchi nyingi za afrika ikiwemo Kenya. Kabla ya uhuru na jinsi zinavyoendelea zikiwa huru hadi sasa. Miongoni mwa sababu zilizowafanya L. Sanja na K. Walibora kuandika kazi zinazoihusu jamii ni ufasidi, usaliti, unyanyasaji na dhulma, malezi kwa mtoto wa kike na kiume, swala la ndoa na uchumba, uongozi mbaya, elimu na maridhiano zilivyokuwa zimekithiri ndani na nje ya uongozi uliokuwepo madarakani.

Viongozi hawa walianzisha matabaka ya watu, wakaendeleza rushwa ufasidi na mambo mengine machafu katika jamii. Tukiangalia kabla ya uhuru, wakoloni waliwadhalilisha wanainchi kwa kuwalaghai, kuwanyanyasa na kuwadhulumu mali yao kwa hila na pengine kwa kutumia kwa kutumia nguvu. Bada ya uhuru viongozi waliowachagua waligeuka kuwa wazungu weusi na wakawa wakiiga matendo na mienendo waliyokuwa nayo wakoloni. Aidha hadi hivi sasa viongozi wa kiasia wawapo madarakani hukengeuka na kuwa manyang'au, mafasidi, mafedhuli, wenye tamaa za madaraka na ujasiri wa kulikandamiza tabaka la wanyonge. Kwa hali hiyo waandishi K. Walibora na L. Sanja wameichora kejeli kwa kutumia fikra mbalimbali katika tamthilia. Maudhui yanayojitokeza kwa kutumia kejeli yamelenga kuwasema watu hawa waliobeba dhamana kubwa katika jamii zao. Kwa kuzingatia maudhui ya kazi hizi tulizoteua, waandishi hawa wametuonyesha madhara ya uongozi mbaya, ufasidi, ubadhirifu wa mali ya umma, maridhiano na maudhui mengine na kuweka mikakati ya namna ya kuudhibiti uongozi kama huo kwa njia ya kejeli. Kejeli kwa hivyo zimetumiwa kwa njia spesheli kuibua maudhui kwa mfano ukoloni mamboleo, utegemezi, uongozi, maridhiano na kadhhalika.

Kwa hivyo kejeli hutumia nafasi kubwa katika jamii ya wasanii si katika mazungumzo tu bali katika namna wanajamii wanavyotoa mawazo yao katika uwanja wa mawasiliano. Kejeli ni mojawapo ya mbinu zinazotawala mazungumzo ya wanajamii ya kila siku na hujenga katika msingi wa kuwepo msigano au mgongano wa namna fulani kati ya hali ya maisha na matarajio ya baadaye ya wanaohusika.

Mweupe: Mtu mweusi anajua maana ya uhuru? Anajua uongozi?

Mweusi: Ukiritimba. Enhe! Ulambatano! (uk 6)

Kauli anazotamka Mweupe kumlenga Mweusi si kauli za kukubalika hata katika hali ambapo mtu fulani amepata usaidizi kutoka kwa mwingine. Bila shaka haya ni maswali ya kuudhi. Maswali haya yanaweza kumfanya mtu kuona uchungu kutokana na anavyoambiwa.

Ni kweli kuwa Mzuka alimpa Zinguo elimu ya Kimizuka ili kuwa na uwezo wa kuiongoza Kusinyika ambayo ni nchi iliyotawaliwa na Mkoloni. Elimu hii ya mkoloni ilikusudiwa kuwatayarisha viongozi wapya wa mataifa huru kudumisha utamaduni na mfumo wa siasa na kiuchumi ambao ungedumisha, kuimarisha na kulinda masilahi ya Wakoloni. Hali hii bila shaka ingedumisha uhusiano baina ya Mkoloni na mtawaliwa. Tunaona haya katika kauli ‘nani alikutoa matongo machoni, nani alikuvalisha nguo akakuwekea sherehe ya tambiko?’ maneno haya bila shaka si maneno ya kukubalika kwa urahisi kwani yanakera na kuchoma. Kumbuka kauli hizi zinatajwa katika nchi ya Kusinyika. Kauli kama hii inachimiza kejeli katika uhuru aliopewa Mweusi. Kwa hivyo Mweusi amegundua kuwa uhuru ule ni wa bandia na Mweupe bado ana haja ya kumwingilia Mwafrika kiuchumi na kitamaduni na hata kisiasa. Hali hii ilimdhaliisha kiongozi Mwafrika kwani huu ulikuwa ukweli kwani viongozi hawa kwanza hawakujua la kufanya katika madaraka yao mapya. Hali iliyowaudhi viongozi Waafrika pamoja na waliotawaliwa. Hali hii inamfanya Mweusi kutamka kauli ‘ukiritimba. Enhe! Ulambatano’ hali inayoonyesha kukasirishwa na kuchomwa na ukweli wa Mkoloni. Zinguo naye si mjinga kwani anafahamu wazi wazi uwongo wa Mkoloni na hila zake.

Kejeli inatokea tunapona jinsi Mweusi anavyopokea maswali haya. Kwanza anakasirishwa nayo na kumrushia Mweupe maneno makali. Kauli hii katika ukiushi wake ina maana kuwa mkoloni alikuwa amepa Mwafrika elimu ya kumtayarisha kuwa kiongozi. Haya aliyafanya kwa malengo fulani: kuendelea kufaidika kutoka katika nchi hizi alizozikalia. Mwafrika naye alitaka kujiendeshea mambo yake mwenyewe kwa kujitegemea. Jambo ambalo lilikuwa gumu na bado ni gumu hadi sasa kwani nchi nyingi za Kiafrika bado hazijajitawala. Hali hii inamtia machungu Mweusi ambaye anajaribu kujiondoa katika minyororo ya ukoloni. Matumizi ya kejeli hii yanaibua maudhui ya ukoloni mamboleo na athari zake. Mweusi ni kweli amepewa uhuru wake na Mweupe.

Ila uhuru huu una hitilafu. Bado Mweupe anataka kujua anavyoiendesha nchi licha ya kumfunza mbinu za kuiendesha nchi. Kutopatana kimawazo kunamfanya Mweupe kumfokea Mweusi ukweli wa mambo naye Mweusi hapendezwi na jambo hili. Hali inayoleta kutoelewana baina ya Mweupe (Mzuka) na Mweusi (Zinguo). Mweusi anachomwa na maneno yake mweupe.

Sichana: Naandaa meza nisiyoila.(uk 25)

Katika lugha ya kawaida Sichana anaposema kauli hii, kwa maana ya nje ni kuwa anajishughulisha kuweka chakula kilichokwishapikwa mezani. Kwa kuzingatia kauli hii katika ukiushi, kauli hii inaweza kumaanisha mambo tofauti kutokana na miktadha mbalimbali kulingana na tamthilia hii. Hapa tunamchukulia Sichana kama mwakilishi wa Wakusinyika wengine ambao ni umma na wenye tabaka la chini. Zinguo na wengine wachache wanaopata raha kutokana na jasho la wengine ni wa tabaka la juu. Sichana anaimba wimbo aliofunzwa na mwalimu wake shuleni; kwa maana kuwa kauli zilizomo katika wimbo huu ni uwakilisho wa malalamishi ya walio wengi ambao ni umma. 'naandaa meza nisiyoila'. Ni usemi unaomaanisha kuwa Sichana ni mmoja wa wanaotozwa ushuru na kwa hivyo wanaotozwa ushuru hawapati huduma walioahidiwa na kwa hivyo wameishia kuishi katika dhiki ya umasikini na njaa licha ya kuwa waadilifu na kutekeleza wajibu kwa kufanya kazi. Wimbo huu kwa hivyo umebeba machungu wanayopitia Wakusinyika ambao ni wazalendo na wenye kuishughulikia viongozi wao bila pingamizi. Hali hii inakejeli uongozi uliopo kwani unafaa kuwaondoa Wakusinyika katika madhila na umasikini uliowazunguka baada ya kupigania uhuru. Kauli hii inachangia katika kuibua maudhui ya uongozi mbaya ambao umepelekea kutungwa kwa nyimbo zilizo na hisia za umma na zinazofunzwa katika taasisi za elimu ambazo ni chombo muhimu cha kuleta mabadiliko. Hii ni ishara ya kutotosheka kwa umma na namna ya uongozi uliokuwa umeshika hatamu baada ya wakoloni kuondoka. Uongozi ule ulikuwa umejaa ufisadi, uchoyo, ukabila na zaidi ya yote viongozi walikuwa watumwa waliowastahi na kuwanyenyekea mabwana wao wa kikoloni. Matabaka yaliyokuwepo yalitengana kama mbingu na ardhi. Tabaka la juu lilikuwa la watawala ambao walikuwa na uwezo wa kiuchumi na kisiasa ingawa kwa kuwakalia wanyonge walikuwa wengi; umma. Tabaka la pili lilikuwa la watu maskini ambao walikuwa wengi. Hili ndilo tabaka

alilokuwemo Sichana ambaye licha ya kumfanyia bwana wake kazi ya kumtunza kwa kumuandalia chakula na kasri lake tunamuona akiwa mwenye njaa na malalamishi mengi.

2.6 Tanakuzi

Tanakuzi ni mbinu ya kusisitiza ujumbe kwa kuambatanisha maneno ya kinyume au yanayokanushana. Pia huitwa takriri tanakuzi.

Wamitila (2008:405) ana maoni kuwa tanakuzi ni dhana ambayo hutumiwa kama mbinu ya kiusemaji au kibaalagha kurejelea msembo ambao unaonyesha ukinzani wa mawazo na aghalabu katika muundo wa kisambamba. Dhana ya tanakuzi huweza kutumiwa kwa upana kuelezea ulinganuzi wa moja kwa moja. Wamitila vilevile ana mawazo kuwa tanakuzi ni miundo ambayo kimsingi inajenga ukinzani fulani. Kauli au maneno yanayotumiwa yanaweza kuonyesha kupingana fulani katika kiwango cha juujuu ingawa katika kiwango cha ndani yana maana wazi. Hebu tutathmini mazungumzo haya.

Mzuka: Kwa kula hali wao matumbo yakinguruma? Kwa kuwafuga?

(uk 12)

Katika kauli hii kuna ukinzani wa mawazo. Hebu tujaribu kuichanganua kwa mtazamo wa kiwango cha juujuu na kiwango cha ndani asemavyo Wamitila (2008:508). Katika kiwango cha juujuu tunaona kupingana katika maneno ‘kwa kula’ na ‘wao matumbo yakinguruma.’ Katika tafsili yetu ya juujuu tunamwona aliyekula kuwa yule ambaye ana shibe na aliye na tumbo linalonguruma kuwa aliye na njaa. Bila shaka aliyekula huwa ameshiba na aliye njaa huwa tumbo linanguruma kwa sababu ya njaa.

Katika maana ya ndani ni muhimu kurejelea muktadha wa mazungumzo haya. Kauli hii Mzuka anaitamka baada ya kugundua udhaifu wa Zinguo ambaye alichukua hatamu za uongozi kutoka kwa Mzuka. Mzuka amegundua kuwa Zinguo ni mbinafsi na mwenye kujitakia makuu. Hali hii Wakusinyika wanaifahamu na hawapendezwi na tabia hii katika nchi yao iliyo huru. Zinguo anaonekana kutopenda hali au tabia ya Mzuka ya kuingilia uongozi, siasa na uchumi wa Kusinyika. Kwa hivyo anatomia mbinu zake duni kumfukuza. Anatomia maji na vikuku, mbinu iliyopitwa na wakati na ambayo ni hafifu mbele ya Mzuka aliye na elimu bora zaidi. Tanakuzi hii inadhihirisha udhaifu katika

uongozi wa Zinguo ambaye ni mfidadi na mwenye kuwanyonya na kuwakandamiza Wakusinyika. Kwa hivyo ni wazi kuwa Zinguo ni kabaila na Wakusinyika waliobaki ni wachochole kwani wana njaa na hawajiwezi. Hali hii haiwapendezi na kwa hivyo Mzuka naye anatumia mwanya huu kumtishia Zinguo ili aendelee kumtimizia matakwa yake.

Mzuka anapotoa kauli hii ana maana kuwa Zinguo ni mbinafsi. Amewakandamiza Wakusinyika kwa kuwatoza ushuru na hata kuwekeza katika nchi za ng'ambo. Nchi anayoiongoza, wananchi huwana chakula na kazi na kwa hivyo wanapitia madhila mengi. Kauli hii kwa hivyo inaibua dhana ya mabwenyenye na wachochole na kwa hivyo anadhihirisha kuwa Zinguo na watu wake wana mali na uwezo wa juu kisisa na kiuchumi.

Tanakuzi nyingine tunaipata katika usemi huu: hebu tutathmini kauli hii.

Zinguo: Huu si mchezo wa watoto. Ni kufa na kupona! (uk 20)

Kwa kuitazama maana ya juujuu, neno 'kufa' linakinzana na neno 'kupona'. Kufa ni kuondokewa na uhai ilhali kupona ni hali ya kuepuka mauti au hali yoyote hatari. Katika kurejelea muktadha wa kauli hii tunaona kuwa Zinguo anaitamka anapojaribu kukabiliana na hila za Mzuka ili kumwondoa katika kujaribu kuingilia mfumo wa uongozi wake. Wakusinyika wamechoshwa na mfumo huu wa uongozi anaodhihirisha Zinguo katika Kusinyika. Zinguo vilevile hapendi kupingwa kwa hivyo amechukulia kukabiliana na Mzuka kuwa kazi ngumu na ambayo si ya kufanyiwa mzaha. Kauli hii kwa hivyo inaonyesha kuwa kupambana dhidi ya Mzuka si jambo la mzaha ila ni jambo linalohitaji ukakamavu na hekima.

Zinguo angependa kudhihirisha kuwa yeye ni kiongozi mwenye uwezo. Mbali na hili tukumbuke kuwa mkoloni alipoondoka alihakikisha kuwa viongozi wapya walidumisha utamaduni, mfumo wa kiuchumi na kisiasa uliodumisha na kulinda maslahi ya wakoloni. Kwa hivyo hata Zinguo atie juhudi za kutaka kuwa huru bila utegemizi kwa mkoloni anajikuta katika hali ya kutojielewa kwani ni lazima ajitahidi kudumisha uhusiano baina yake na mkoloni na hata mtawaliwa ili matakwa yake yatimizwe. Kwa hivyo uhuru walionao ni wa bandia na kwa hivyo bado kuna mapambano ya kujaribu kujinasua katika

mitigo na athri za mkoloni. Hata hivyo Waafrika hawakuwa na la kufanya ila kujitahidi kuimarisha uhuru wao. Kauli hii inajenga maudhui ya unafiki kwani licha ya Zinguo kujisifu kuwa anamfahamu Mzuka, ameshindwa kumng'oa.

Zinguo: Wamekufa ijapo wako hai na macho wanapepesa.

(*Akiwaza*) lakini ni watu wetu! (uk 22-23)

Katika kuirejelea kauli hii katika maana ya juujuu tunaangalia maneno 'wamekufa' na 'wako hai' kauli hizi zina ukinzani. Kufa ni hali ya kutokuwa na uhai na kuwa hai na hali ya kuwa hai ni kuwa katika hali ya kuendelea kuishi.

Kauli tunayoirejelea ni 'wamekufa ijapo wapo hai na macho wanapepesa'. Usemi huu ni wenye ukinzani. Zinguo anaposema maneno haya katika hali halisi ya matumizi ya maneno haya haiwezekani kuwa watu wa Kusinyika wamekufa na kwa wakati mmoja wako hai. Tunapata maana kimatumizi tu kwa kuichunguza kauli hii kimuktadha. Zinguo anaitamka kauli hii baada ya Mzuka kumtegea vitendawili ambavyo anavitegua na hata kujigamba kwa Mzuka kuwa amekuwa mwerevu kumshinda mwalimu wake. Vitendawili hivi vimejaa mafunzo ya njama za Mzuka za jinsi ya kumnyanyasa Mkusinyika kwa kumtoza ushuru wa juu katika viwango mbalimbali. Kwa kuirejelea kauli hii tunaona kuwa Wakusinyika wamenyonywa na Zinguo kiwango cha wao kuonekana wafu. Wanatozwa ushuru mkubwa, hawana chakula, wanafanyishwa vibarua na hata uchumi wao umezoroteka. Kwa hivyo hali yao ya maisha ni ya dhiki na wanapitia mateso ambayo yamewaacha katika hali mbaya. Hata hivyo katika hali yao mbaya hiyo; bado Zinguo ana matumaini ya kuendelea kupokea ushuru kutoka kwao. Ukiushi wa usemi huu inaibua maudhui ya maana ya uhuru. Uhuru walionao Wakusinyika hauwafai ila umewatumbukiza katika madhila.

Sichana: Unalisha wa mbali na wa karibu (uk 25)

Ukinzani unaonekana katika maneno 'mbali' na 'karibu' katika ulimwengu halisi mbali ni nomino inayomaanisha mwendo mrefu. Karibu nayo ni nomino yenye maana sio mbali. Hali hii halisi haiwezi kutufanikisha kufasiri maana ya tanakuzi hii. Tanakuzi hii tunaipata katika wimbo unaoimbwa na Sichana. Wimbo huu amefunzwa shuleni. Katika matumizi ya maana ya maneno haya kwa maana yao kikamusi haiwezi kutoa ujumbe au

kuibua maudhui. Maudhui yanaibuka tu katika ukiushi wa kisemantiki. Kauli katika wimbo inaposema:

‘unalisha wa mbali na wa karibu.’ Bila shaka wa mbali hapa ni Mzuka ambaye ni mkoloni. Naye wa karibu ni Mkusinyika ambaye anafanya kazi kwa bidii ili kumlisha huyo wa mbali. Kauli hii inaibua maudhui ya madhara ya ukoloni mamboleo na uongozi mbaya. Zinguo ni lazima atimize matakwa ya bwana wake ili azidi kuiongoza Kusinyika. Bila kufanya hivyo anawekewa vikwazo na kutishiwa kutimuliwa katika uongozi na mkoloni. Katika kauli hii msomaji anafasiri kuwa Zinguo ambaye ni kiongozi wa Kusinyika anadumisha na kulinda maslahi ya wakoloni ili kubakia uongozini au kwa manufaa yake mwenyewe. Kwa hivyo Zinguo anaonyesha udhaifu katika uongozi wake kwani hana msimamo wa kujiondoa katika minyororo ya wakoloni na anakosa maongozi dhabiti ya kiuchumi na kisiasa. Kwa hivyo Zinguo hajajitolea kuulinda na kuikuza Kusinyika kimaendeleo. Hali kadhalika kupitia Zinguo, Kusinyika imejiingiza katika uhusiano mpotovu na nchi za ng’ambo. Hali ambayo ni hatari na inayowapelekea Wakusinyika kutunga nyimbo zinazodhihirisha mateso na uongozi mbaya kutokana na ushirikiano wa kiongozi wao na Mzuka.

Zinguo: (Akimwamuru) Haya, toka uende kwenu!

Mbio sana, nikifumba na kufumbua macho uwe umeenda tayari! (uk 27)

Kauli inayojitokeza hapa pia ni tanakuzi, katika hali halisi ya matumizi ya maneno haya ‘kufumba na kufumbua macho’ ni kitendo cha kufunga macho na kufungua (kupepesa). Lakini maana kiushi tunachukulia kwamba Zinguo kama kiongozi anaelewa sheria za Kusinyika mbali na heshima anayohitaji binadamu kama kiumbe; Zinguo anaposema ‘kufumba’ tafsili yetu ni kuwa Zinguo anavunja sheria kwa hiari. Anaelewa anachotaka kutekeleza lakini ni mkaidi tu. Kufumbua macho ni kutanabahi na kurudia hali yake ya kawaida ya kifikiria na kuheshimu sheria. Ufasiri huu una maana kifasihi kwa kuwa kimuktadha Zinguo amemtajia Sichana kuwa alikuwa amesahau kuwa mkewe hakuwepo na kwa hivyo hali hiyo imempa nafasi ya kumnajisi Sichana licha ya Sichana kujaribu kujitetea. Kauli hii kwa hivyo inaibua maudhui ya taasubi ya kiume pamoja na nafasi ya mwanamke katika jamii. Zinguo anamwonyesha Sichana ubabe na kumdharau kwa kuwa

ni mwanamke kiwango cha kumlazimisha kuhusiana naye kimapenzi licha ya yeye kuwa na mke halali katika ndoa.

Wafuasi: Wamefufuka!

Sio wafu tena

Sio punguani tena wamezindukana (uk 92)

Tanakuzi hii inatufafanulia hali ya kupambanukiwa kwa wafuasi wa Zinguo wanapoona mabadiliko katika Wakusinyika. Kwa kawaida punguani ni mtu asiyekuwa na akili timamu, kichaa, mwendawazimu au chakaramu. Hali hii ni kinzani kwani waliokuwa wakimfuata Zinguo kwa lolote alilosema wamegundua Wakusinyika waliochoka na mienendo ya Zinguo wamekataa na kwa hivyo kupigania haki yao. Kauli hii inaibua maudhui ya maana ya uhuru. Wakusinyika wanaoipenda Kusinyika hawataki hali iliyopo Kusinyika kuendelea ila wanataka mabadiliko ili uhuru wao uwafae.

2.7 Oksimora

Katika kufasiri dhana ya oksimora tumefuata mawazo ya Wamitila (2008:404) anaposema kuwa oksimora ni tamathali au mbinu ya usemaji au balagha ambayo inahusisha kuweka vitu viwili pamoja au kuvigotanisha vitu ambavyo kimsingi vinakinzana. Anazidi kufafanua kuwa oksimora inafanana na kweli-kinzani ila oksimora ina ubanifu mkubwa zaidi. Maelezo yake yanasema oksimora huwa na maneno mawili yaliyogotanishwa, tofauti na kweli-kinzani ambayo inahusisha kauli pana zaidi.

Hebu tuchanganue usemi huu:

Kaza: *(Anamchoma Zaidi)* Ukweli mtamu.

Kumbe mkuki kwa nguruwe.....

Katika usemi ‘ukweli mtamu’ kuna mgotano. Kawaida usemi huu huwa ‘ukweli mchungu’ katika hali ya Kaza kubadilisha hali ya ukawaida wa usemu huu anaufanya kuwa oksimora. Katika hali ya ulimwengu halisi ukweli huchoma na kumfanya mtu kukasirika na hata kuzua ghasia. Hii ni maana ya juujuu. Katika maana ya ndani muktadha wa matumizi ya usemi huu utatufaa. Kauli hii Kaza anaitamka wanapotiwa kizuizini wakiwa na Zinguo. Kaza anaonekana kupambanukiwa na kwa hivyo kugundua kuwa Zinguo hakumfaa kwa vile alijinyakulia ardhi, akajpa kandarasi nahata kupeleka hela ughaibuni bila kumpa Kaza. Huu ndio ukweli unaomchoma Kaza. Lakini kwa kaza

ni ukweli mtamu kwa kuwa amegundua siri za Zinguo na yuko tayari kukataza kwani Wakusinyika wamechoka na kwa hivyo kuwaondoa mamlakani ili wapate mwelekeo wenye manufaa.

Kwake Zinguo ukweli huu ni mtamu amefaidi kwa kumtumia kaza kujilimbikizia mali. Kaza anamwambia Zinguo. ‘kumbe mkuki kwa nguruwe.....’ huku ni kutilia mkazo oksimora hii.

2.8 Hitimisho

Katika sura hii tumeona fasili mbalimbali za tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora zilivyotumika katika kuibua maudhui na kuyaendeleza katika *Zinguo la Mzuka*. Tumetambua kuwa tamathali za usemi zinapotumika katika kazi za fasihi bila shaka msanii huwa na maana kiushi. Maana hii hujitokeza kulingana na muktadha wa matumizi wa tamathali hiyo ya usemi. Kwa hivyo msanii huteua tamathali kimakusudi ili kuwasilisha ujumbe Fulani aliokusudia kuifikia hadhra yake.

SURA YA TATU

UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA *MBAYA WETU*

3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumetambua na kuchanganua jinsi matumizi ya tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora zinavyoibua na kuendeleza maudhui katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*. Tumefanya hivyo ili kupata mifano zaidi haswa ya tanakuzi na oksimora ambazo zimetumika katika matini hizi tulizoteua. Tumefafanua tamathali hizo kwa kurejelea ukiushi unaojitokeza katika kauli zilizobeba tamathali tulizotaja hapo juu.

3.1 Sitiari

Kwa mujibu wa mbinu hii ujumbe na maana yake hujitokeza kimuktadha katika hali inayoondoa chapwa. Kwa hivyo maoni ya Wamitila (2008) kuhusu sitiari yanatufaa. Wamitila (2008:420) katika kuelezamaana ya sitiari ana maoni kuwa kuna **kilinganishi, kilinganishwa** na **msingi**. Kilinganishi ni kile kinachotumiwa kama msingi wa kufananisha, kilinganishwa ni kile kinachofananishwa na msingi ni ile sifa yenyewe ya ulinganishi. Kwa mfano:

Mtu II: Almuradi tabia ya wizi ndiyo nta inayotuunganisha kitaifa

...hata wananchi wa kawaida kama mimi na wewe ni wezi tu.

(uk 3)

Katika kauli iliyo katika mkolezo ambayo imesemwa na Mtu II tunaweza kutambua kilinganishi ambacho ni 'nta', kilinganishwa ni 'tabia' na msingi ni sifa ya nta ambayo ni kitu kinachofanana na gundi ngumu ambacho hutengenezwa na nyuki. Ili kupata fasili kamili ya sitiari hii ni muhimu kurejelea gundi. Gundi huwa na sifa kama vile: majimaji, mnato na vilevile kugandisha. Katika matumizi ya sitiari hii katika ulimwengu halisi, hatupati maana. Maana hizi za kikamusi hazitupi fasili yoyote ya kutufaa. Katika hali dhahania ukiushi kisemantiki huleta maana kimuktadha kulingana na vile msomaji anavyofuatilia mtiririko wa matendo katika tamthilia. Kwa hivyo tunaufasiri kuwa Mtu II anaposema kauli hii, anarejelea uozo wa tabia ya wizi iliyokithiri katika jamii hii. Katika jamii hii kitendo cha wizi kinachukuliwa kama utamaduni na yeyote atendaye kitendo

cha wizi haonekani kuvunja sheria. Tabia ya wizi ni jambo la kawaida. Tabia ya wizi imekuwa mazoea. Kwa hivyo sitiari hii inarejelea sifa na tabia ya wanajamii hii. Yeyote katika kijiji hiki hadhubutu kumchukulia mwizi hatua za kisheria ili kuwezesha utangamano katika jamii. Tabia hii ya wizi ina mizizi hata kwenye sekta muhimu za serikali kwani pesa zinazotengewa miradi ya jamii hazitimizi wajibu huo ila huishia katika mifuko ya watu binafsi. Tukirejelea muktadha wa kauli hii tunawapata wahusika Mtu I na Mtu II wakizungumzia madhara ya kikojozi na mwizi. Wanajiuliza kati ya kikojozi na mwizi ni yupi anayehujumu jamii zaidi. Ubishi uliopo umezuka kwa kuwa Mtu II amemwita Mtu I kikojozi. Kutokana na matini tunafahamu kuwa unywaji pombe kupindukia ndiyo sababu ya Mtu I kuwa kikojozi. Katika hali yake ya kuwa kikojozi hatimizi wajibu wake wa kuishughulikia jamii yake na hata kufanya kazi ili kujikuza kiuchumi. Tukumbuke kuwa jumla ya pato la taifa hutegemea utendaji kazi wa wananchi. Kwa hivyo ikiwa Mtu I anajishughulisha na kunywa pombe kiasi cha kujisahau na kuwa kikojozi, basi anachangia katika kuhujumu uchumi wa taifa. Katika mazungumzo yao vilevile wanawataja wafanyakazi mbalimbali kwa kutumia tamathali ya tabaini: ‘na wezi na wapunjaji hapa kwetu wako tele. Si majaji, si mawakili, si wahubiri, si maaskari polisi, si....’

Hawa vilevile wanahujumu pato la taifa kwani kwa kuiibia serikali, wanakwamisha miradi mbalimbali ambayo ingeinufaisha jamii. Katika muktadha huu tunafasiri kuwa tabia ya wizi katika jamii hii ni tabia ya kawaida na si jambo la kushangaza ikiwa mtu atapatikana akivunja sheria ya aina hii. Kwa hivyo hali hii imekuwa mazoea au utamaduni wa jamii hii ingawa ni utamaduni unaoirudisha jamii nyuma.

Usemi huu kwa hivyo unaibua maudhui ya ufisadi ambao umeivunja jamii na ambao umekuwa jambo la kawaida kwani hata viungo muhimu vya serikali vinavyofaa kuiendesha serikali vinajihusisha na ufisadi pamoja na kuzorotesha maendeleo ya nchi. Nyingi ya pesa za kuiendeleza nchi zinaishia kuwanufaisha watu binafsi. Ni jambo la kushangaza kuwa vitengo vinavyofaa kuwaadhibu wanaojihusisha na wizi wa aina hii vinatajwa. Kwa mfano mawakili na maaskari polisi.

Wanajamii hii wote wameathiriwa na kwa hivyo kuishia kuwa wezi. Mfano ni Fiona. anauza pombe haramu, ni mwizi kwani kulingana na usemi wa wanywaji, yeye hungoja

wakati wamelewa chakari na kuwaibia kwa kutowarudishia chenji. Kuna wizi wa aina mbili; wizi anaotekeleza Fiona ambao unarejelea sekta ya biashara na wizi wa kimabavu ambao unamshirikisha Matari na maafisa wakuu katika serikali.

Hata hivyo Mtu I na Mtu II wanaposema wao pia ni wezi tunaona kuwa ni washirika wa Matari. Matari anapoiba huleta na kuwanunulia pombe wao pia wakanywa pombe iliyonunuliwa na Matari kutokana na fedha zilizoibwa kutoka kwa aila yake. Mtu II anaafiki haya anapotaja methali ‘baniani mbaya kiatu chake dawa’. Hii ni methali ya kisitiari kwani inaonyesha kwamba Mtu II hapendezwi na tabia ya Matari ya kuwaibia watu, kwani methali hii inamaanisha mtu hawezi kuwa mbaya zaidi kwani kuna jinsi anavyoweza kumfaidi mwenzake kutokana na ubaya wake. Vilevile Mtu I na Mtu II wanajiibia wakati wao maalum wa kufanya kazi ili wawe na pato la kuikidhia jamii yao; hawafanyi kazi ila kushiriki tu katika kunywa pombe ambayo wamenunuliwa na Matari. Haya yote yanawafanya kutowajibika kwa familia zao kwani hawazishughulikii. Maudhui mengine yanayojitokeza ni madhara ya dawa za kulevya ambayo tunayaona kwa Mtu I, Mtu II na Mtu III. Hawana uwezo wa kuwa na uamuzi wenye busara kwani wanatoa uamuzi kulingana na kiwango cha ulevi walichonacho. Kwa mfano Mtu II anauwezo wa kuwaza vyema na kutoa mawazo mapevu kabla ya kunywa buzaa lakini punde anywapo anakuwa na maamuzi mabaya.

Matumizi ya kilinganishi, kilinganishwa na msingi yanatufaa katika kuchanganua kauli za Mtu I katika semi zifuatazo. Katika semi hizi maneno mwokozi, korosho na dawa yatatufaa katika mchakato huu na kutuwezesha kuchanganua maana zinazoibuka kutokana na ukiushi ulioko katika kauli hizi.

Mtu I: Huyu ni mwokozi wetu...eeh!

Mtu I: Hana mkono wa korosho. Matari...

Mtu I: Nasi dawa yetu ni Matari. Ah!

Katika kauli ‘huyu ni mwokozi’ kilinganishi ni ‘mwokozi’ na kilinganishwa ni ‘huyu’. Msingi basi ni tabia ya mwokozi. Mwokozi huwa na sifa ya ukombozi hasa inavyofahamika katika dini ya Wakristo au tunaweza kusema kuwa ni mtu anayewatoa wengine katika shida. Hali hii bila shaka haiwezi kuleta maana yoyote bila muktadha kurejelewa. Kwa kurejelea muktadha wa mazungumzo ya wahusika katika matini: kauli

‘huyu ni mwokozi wetu’ ni sitiari. Katika matumizi ya ulimwengu halisi tumeona kuwa neno mwokozi hutumika katika muktadha wa dini kumaanisha mtu aliye na uwezo wa kuepusha yeyote aliyemkubali na mateso au dhiki. Katika ulimwengu dhahania wa sanaa tunayoirejelea, Mtu I anamwona Matari kuwa mwokozi kwa kuwa yeye ni mtegemezi wa Matari. Matari ana uwezo wa kiuchumi kutokana natabia yake ya wizi na kwa hivyo ni mfadhili wake wa pombe wainywayo kwa Fiona. Hali hii kwa hivyo inamfanya kupata kinywaji bila kutoa jasho kwani wakati wowote Matari ajapo baada ya kuiba kwao nyumbani, huwapa kinywaji wote waliopo bila kubagua na kwa hivyo kumfanya Matari kuwa na thamani kubwa kwao. Fasili hii inajitokeza kwa sababu ya ukiushi unaojitokeza kulingana na muktadha wa kauli hii. Maudhui yanayoibuka hapa ni ya utegemezi. Mtu I na Mtu II ni wategemezi wa Matari na ikiwa Matari hayupo au hana pato, basi mipango yao ya kuburudika kwa kinywaji cha buzaa inatumbukia nyongo. Hali hii inawafanya Mtu I na Mtu II kumwona Matari kuwa mkarimu kiasi cha kumfafanua kuwa ‘hana mkono wa korosho’. Tunafahamu kuwa korosho ni mbegu laini ya rangi ya maziwa yenye ganda gumu juu ambayo iko kwenye kitako cha bibo na huliwa baada ya kuchomwa. Msingi huu wa kilinganishi ndio tunaourejelea: sifa hii ya ganda gumu. Kulingana na muktadha wa usemi huu, tunaona kuwa Matari si mkono birika ambaye akipata hadondoi. Cha Matari kinaliwa na wenzake kwa kuwa hana sifa ya kutogawa kwa wenzake. Usemi huu ni wa kumsifu Matari kuwa si mchoyo kwani anapopata cha kuliwa, marafiki zake hawaachwi nyuma. Katika hali hii Mtu I na Mtu II wanamwona Matari kuwa dawa. Kwa hivyo katika ulimwengu dhahania Matari ni kilinganishi kutokana na sifa yake ya kutokuwa na mkono wa birika. Katika ulimwengu wa matibabu, dawa huleta afueni kwa mgonjwa. Kwa hivyo wategemezi wa Matari wanapata afueni kwa kujipatia kinywaji cha bure kutoka kwa Matari.

Katika usemi ‘unakuwa kikojozi’ kilinganishwa hapa ni Mtu I na kilinganishi ni kikojozi nazo sifa za kikojozi ni msingi. Ili kuondoa uchapwa, tunaishughulikia kauli hii katika matumizi yake kimuktadha. Matumizi katika muktadha wa kauli hii yanadokeza maana tofauti na matumizi ya kauli hii katika ulimwengu halisi. Kwa hivyo maana itakayoibuka katika usemi tulionukuu hapo chini, unaosemwa na Mtu II, ni lazima itokane na iungane na jumla ya muktadha katika matini hii. Kwa hivyo sitiari hii ina

maana katika matini hii na wala sio nje ya matini hii. Vilevile sitiari hii imetumika ili kudokeza maana tofauti na maana yake katika matumizi ya ulimwengu halisi. Hata hivyo sitiari hii haiwezi kumaanisha chochote msomaji atakacho ila maana huongozwa na muktadha. Kwa hivyo maana dhahiri ya sitiari hii ina thamani ya kipekee kulingana na muktadha wa matumizi yake. Hebu tutathmini kauli hii:

Mtu II: Nasikia mkeo an'lamika siku hizi...ukilewa chakari unakuwa kikojozi...unalowesha malazi kama kitoto. (uk 6)

Mtu I: (kwa mtu II) acha kujifanya mtakatifu hapa. Wafikiri sisi hatukujui...eeh...lofa wewe!

Kikojozi ni mtu anayekojoa kitandani akiwa usingizini. Matumizi ya neno kikojozi katika ulimwengu halisi hayatoi maana ya kutufaa katika hali hii. Lakini katika hali dhahania ya matumizi ya kauli hii ya Mtu II, kuna maana mfichamokulingana na muktadha katika matini. Katika kufasiri sitiari hii, tunamuona Mtu I akiwa mtoto. Mtoto kawaida huwa hawajibiki kwani anawategemea wazazi katika mahitaji yake yote. Mtu I anasawiriwa kama mtoto kwani hawajibiki wala kuyashughulikia majukumu yake kwa wanawe na mkewe. Kazi yake kunywa tu. Hali hii imezua ubatilishaji wa majukumu. Bila shaka majukumu yake ameyaachia mkewe ambaye ana jukumu la kuwatafutia watoto chakula, mavazi, nyumba na hata elimu. Kwa jumla mke amechukua mahali pa mume na kumkidhia mahitaji yake. Hata hivyo mkewe Mtu I ana jukumu la ziada kumtunza mumewe ambaye ni mlevi chakari na kikojozi.

Maneno haya ya Mtu II yanamkejeli Mtu I ambaye bila shaka anapandwa na hasira kwa kuitwa kikojozi. Hali hii inaonyesha kuwa hapendezwi na hali aliyomo ingawa ni kweli. Fasili hii tunaipata tu kwa kuichanganua kauli ya Mtu II kwa kuzingatia ukiushi uliomo katika kauli hii. Mtu I vilevile anatupasulia mbarika kwa kutuambia sifa za Mtu II kwani anamuita 'lofa', 'mfasiki'. Marejelezi haya ni ya kisitiari kwani lofa ni mtu asiye na kazi, mzururaji, ombaomba. Hizi ni maana katika ulimwengu wa halisi. Hii ni nafasi aliyomo Mtu II ambaye ametutambulia udhaifu wa Mtu I. Kulingana na ufasiri katika hali dhahania. Kwa hivyo wote hawawajibiki kwa jamii zao, wamewaachia wake zao majukumu ya kuzitunza jamii zao. Muktadha wa matumizi ya maneno haya ndio unaotuwezesha kufasiri maana mfichamo katika sitiari hizi. Maana hii mfichamo bila shaka ni kiushi. Sitiari hizi kwa hivyo zinaibua maudhui ya kubatilishwa kwa uwajibikaji

katika jamii ambapo siku hizi au katika jamii hii wanaume wamepiga kambi katika vilabu wakinywa pombe huku wakiwa wamewaachia wake zao majukumu ya kuwatunza watoto na mambo mengine muhimu nyumbani.

Sitiari tunayoishughulikia katika usemi wa Mtu II uliopo hapa chini vilevile imechukua mtazamo wa kilinganishi, kilinganishwa na msingi. Ufasiri wa kauli tunayotaka kuishughulikia ina maana yake katika muktadha wa matumizi yake katika matini.

Mtu II: Hilo Lila halijui haliwezi. Anaishi jijini lakini mshamba pale alipo.

Ufasiri wa neno mshamba katika ulimwengu halisi, ni mtu anayedharauliwa kwa kutojua mambo ya mjini. Kwa hivyo mtu anayerejelewa kuwa na sifa hizi huwa hana makini na mara nyingi hukosa mazoea ya kulinda mali yake dhidi ya wizi. Kwa hivyo Matari anaitumia nafasi hii kwa manufaa ya kujinufaisha kutokana na udhaifu huu alio nao Lila na kuiba pesa taslimu elfu tisini. Usemi huu hauwezi kueleweka kuwa na maana hii katika ulimwengu halisi. Muktadha wa matumizi ya usemi wenye sitiari wa Mtu II unakuwa na maana tu unapotathminiwa katika muktadha wa matumizi yake. Sifa ya kutokuwa makini bila shaka ndiyo inayozingatiwa hapa. Mazoea haya ndiyo yanamtia mashakani licha ya Lila kujua kuwa Matari ana mkono mrefu. Kwa hivyo hali hii anaidhihirisha Matari baada ya kumuibia Lila pesa zake. Anamuita mshamba. Hali inayodhihirisha ukosefu wa maadili katika jamii hii.

Matari vilevile anaonyesha kutowajibika kwani licha ya mamake kuwa mgonjwa anawaibia aila zake na hashughulikii ugonjwa wa mamake. Ni jambo la kushangaza kuwa Lila anatoka mjini kuja kumshughulikia mamake ilhali yeye yupo. Mbali na hayo anamwibia Lila hapo alipo mamake.

Katika kufasili kauli katika usemi wa Matari tunatumia maoni ya mtaalamu Leech (1969) anayesema kuwa sitiari huhusishwa na sheria mahususi ya uhamisho inayosema **A** ni kama **B** ikiwa na maana kuwa **A** ina tabia au sifa kama **B** ingawa **A** na **B** ni vitu viwili tofauti, huwa kuna uhusiano fulani yavyo unaovifanya vihusishwe. Uhamishaji wa maana unatokana na uwezo wa msemaji wa kulinganisha mambo tofautitofauti maishani. Sitiari kwa hivyo huwa na nyuso mbili, uso mmoja ni ule wenye maana iliyo wazi na mwingine ni wa maana fiche. Katika uchanganuzi wetu wa kauli ya Matari, tuna maana katika

ulimwengu halisi na maana mfichamo ambayo huibuka kutokana na matumizi ya usemi huu kimuktadha. Hebu tutathmini kauli hii.

Matari: Yani mimi mwehu kiasi gani hata nikuibie wewe dadangu ilhali mama mgonjwa hali yake taabani?

Lila: Matari! Acha kunichezea akili. Wewe mtu kweli au nduli? (uk 15)

Katika kauli ‘Yani mimi mwehu kiasi gani hata nikuibie wewe...’ tumhamisha sifa za mwehu na kumpa Matari. Kwa hivyo Matari amechukua sifa za mwehu na kuonekana kuwa mwehu kutokana na vitendo vyake. Katika hali hii kilinganishi ni mwehu na kilinganishwa ni Matari (kwa kurejelea nafsi ya kwanza; mimi) kisha msingi ni sifa za mwehu.

Neno ‘mwehu’ lina maana ya wazimu au mtu aliye na akili razini. Miongoni mwa sifa za mwehu ni kutofanya mambo kwa kukadiria athari za matokeo ya jambo alifanyalo, kufanya mambo kinyume na matarajio na kadhalika. Matari anatumia kauli hii anapokabiliwa na Lila ambaye ni dadake. Matari amemwibia Lila shilingi elfu tisini na hataki kukubali kuwa ameiba. Hali hii inadhihirisha sifa za nomino aliyochagua kujilinganishia. Hali hii inamfanya Matari kuwa mnafiki. Hali hii inaonyesha kiburi alichonacho Matari. Ana tabia ya wizi na hataki kukubali kuwa yeye ni mwizi. Matumizi ya kauli hii katika matini yanaibua maudhui ya upotovu wa vijana.

Katika kauli ifuatayo tungependa kupata fasili ya neno ‘maskini’ kwa kuzingatia muktadha wa matumizi yake. Kauli hii ya Lila vilevile ni sitiari. Neno hili linatumiwa na Lila anapokuwa katika mazungumzo na babake.

Lila: Nikakutana na wifw Vero. Nilidhani maskini kajipeleka mwenyewe hospitalini.(uk 26)

Sitiari tunayotathmini imeonyeshwa kwa mkolezo hapo juu. Sitiari hii imedokezwa kwa neno ‘maskini’. Maskini ni nomino inayomaanisha mtu mchochole au asiye na wakumsaidia katika madhila yake. Hii ni maana ya nje ya usemi huu. Katika hali dhahania, tunaona kuwa Vero anaishi pekee kijijini kwa kuwa mumewe anafanya kazi mjini. Katika maisha ya ndoa, Tonge anafaa kuwa karibu naye wakati huu ili amsaidie wakati huu wa uja uzito. Hali tunayoshuhudia ni kinyume kwani Tonge hayupo kutimiza

wajibu huu. Hata hivyo, Licha ya kuwa mja mzito, anayashughulikia majukumu yake vilivyo kwani anawalisha mifugo alioachiwa na mumewe kuwatunza. Tazama wakati anapokutana na Lila. Saa kumi na mbili asubuhi akiwa tayari amejua kuwa ameibiwa ng’ombe. Hali hii inaonyesha kuwa Vero ni mwanamke mwenye bidii na kwa hivyo anawajibika katika kujaribu kuzalisha mali katika familia yake. Katika hali kiushi kuna uhamishi wa sifa za maskini na kumpa Vero. Miongoni mwa sifa za maskini ni kipato kidogo, dhiki, ulemavu wa mwili, kutegemea misaada na kadhalika. Neno hili vilevile huwa ni tamko la kumhurumia mtu aliyefikwa na mkasa au tatizo kubwa. Sifa hizi haziingiliani na Vero ila sifa ya mwisho. Sifa hii ya mwisho inaleta maana tunaporejlea hali ya ujauzito wake na kuibwa kwa ng’ombe wake. Vero anataabishwa na hali ya wizi iliyomkumbwa na hakubali kupoteza jasho lake kwa njia rahisi hivyo. Hatua aliyochukua inaonyesha kuwa ana fununu ya kule waendapo ng’ombe baada ya wizi. Hali hii yaweza kuchangiwa na uhusiano wake wa kimapenzi na Matari ambaye kufikia wakati huu anashukiwa kuwa ameshiriki katika kitendo hicho cha wizi wa ng’ombe. Hali hii inaibua maudhui ya bidii na uwajibikaji. Vero hajitendekezi.

3.2 Chuku

Chuku ni tamathali ya usemi inayoeleza hali ya sifa za kitu kuelezwa kwa namna inayokuza sifa zake au kuzidunisha sifa hizo kuliko hali yake ya kawaida. Chuku kwa hivyo ni hali ambapo maelezo yanatiliwa chumvi kwa minajili ya kuisimua ama kueleza hali fulani. Kwa misingi hii basi huwa pana ukinzani kati ya hali inayosemwa na ukweli wenyewe. Hebu tutathmini usemi huu:

Mtu II:wacha kumbughudhi Fiona bure bilashi...we’ kunywa bwana... kunywa ulewe mpaka uone vimulimuli.

Mtu II: Umekunywa pombe ya Fiona miaka nenda miaka rudi...mbona hujapofuka au kufa? Eh? ...twakuona u pale pale tena vilevile...hupandi hushuki..leo unaleta uzushi gani tena? (uk 1)

Katika kauli zilizopo hapo juu za Mtu II tulizodokeza kuna chuku. Katika ulimwengu halisi neno vimulimuli lina kisawe cha vimetameta na humaanisha mdudu kama nzi anayemetameta usiku. Mtu akinywa hadi afikie kiwango cha kuona vimetameta huwa amekunywa mvinyo kupindukia. Kwa hivyo neno vimulimuli linaitambulisha chuku hii

na kuufanya usemi huu kuonekana kutiwa chumvi. Ili kupata fasili kimuktadha tunauhusisha usemi huu na maneno mengine katika muktadha wa matumizi yake.

Mtu II anatia chumvi kiwango cha pombe anachotaka Mtu I anywe. Hali hii inadhihirisha kwamba Mtu II anajua madhara ya pombe na kwa hivyo anauonea fahari unywaji pombe. Kwa kweli unywaji pombe huu si wa kimzaha. Bila shaka ni unywaji ambao baada ya kileo hicho huwa mlevi amelewa chakari kiasi kwamba hajitambui.

Katika kuifasiri chuku hii katika hali yake kiushi ni kuwa ulevi wa aina hii ni wa kuiangamiza jamii kimaendeleo kwani baada ya kulewa chakari bila shaka hakuna kazi yoyote inayoweza kutekelezwa. Kwa hivyo Mtu II anamhadaa mwenziwe anywe hadi ajisahau. Katika hali ya kujisahau, majukumu vilevile yatasahaulika kwani Mtu I si mtoto; ni mtu na mkewe na watoto.

Chuku hii inaibua maudhui ya uwajibikaji mbali na starehe wanazotaka Mtu I, Mtu II na Mtu III. Hawana jingine la kushughulikia isipokuwa kunywa pombe kupindukia. Hii ni hali ya hatari kwani itaathiri hali ya maisha ya baadaye ya jamii nzima ambayo imeganda kimaendeleo na haina mwelekeo. Anaposema ‘umekunywa pombe ya Fiona miaka nenda miaka rudi... mbona hujapofuka au kufa?’

Mtu II anaendelea kutia chumvi unywaji wa pombe. Kwa hivyo anawachochea wenzake. Kulingana na kauli hii anafahamu madhara ya unywaji pombe kwani anataja kupofuka na kufa. Katika kauli hii kiukiushi, hali hii inadhihirisha kuwa ni mazoea ya wanaume katika kijiji hiki kunywa pombe na kuwa haijulikani wameinywa pombe hii kwa muda gani. Katika kauli ‘miaka nenda miaka rudi’ chuku inajitokeza kwani si rahisi kusema ni miaka mingapi inayozungumziwa. Tunafsiri kuwa bila shaka ni muda mrefu sana kiasi cha Mtu II kutojua idadi halisi ya miaka ya unywaji pombe. Aidha, kauli kuwa Mtu I anakunywa pombe ‘miaka nenda miaka rudi’ haiwezi kuwa kweli katika ulimwengu halisi kwa kuwa maisha ya binadamu si marefu kiasi hicho. Kitendo cha kuanza kunywa pombe kwa hivyo kilianza wakati fulani na kutokana na urudufu kikazoeleka na ndio maana Mtu II amekiona kama mazoea. Hali hii ya kunywa pombe kwa muda mrefu imesambaratisha na kuzorotesha maisha yao na kuwafanya kubakia walipo. ‘hawapandi hawashuki’.

Maudhui yanayoibuka hapa ni athari za dawa za kulevya kwa jamii. Mtu II ana usemi kuwa ‘u pale pale tena vilevile’ hii ni kauli inayodhihirisha kubaki nyuma kimaendeleo kwa wanaojishughulisha na pombe. Hakuna faida yoyote wanayopata kama wanywaji isipokuwa kuharibu wakati na pesa. Kama walevi, wamebakia kupiga kambi kwa Fiona badala ya kujishughulisha na kilimo ili wawe na pato, kuwaelimisha watoto, na shughuli zingine muhimu walizotelekeza. Muktaadha wa mazungumzo haya unadhihirisha hali ya kubakia nyuma kimaendeleo kwa wanaume wa jamii hii kwa sababu ya unywaji pombe.

Chuku hulifanya jambo la kawaida kuonekana kuzidi kiwango cha kuaminika katika ulimwengu wa kawaida. Hali hii ndiyo tunataka kuitathmini katika kauli ya Mtu II anapomzungumzia Fiona.

Mtu II: Kwa kweli hata huyu Fiona tunayelienzi tembo lake na kukimezea mate kiuno chake naye pia anapenda kupunja watu. (uk. 3)

Kauli hii katika ulimwengu halisi si sawa. Mtu hawezi kumeza mate kwa sababu ya kiuno cha mtu tu. Katika hali dhahania na vilevile kulingana na muktaadha, kauli hii imerejelea urembo aliokuwa nao Fiona. Hali hii inawafanya wanaume kukimezea mate kiuno chake kilichokuwa mviringo na ambacho kilizungushwa na Fiona alipojipendekeza mbele ya wanaume. Kauli hii kwa hivyo inatambua urembo wa mwanamke huyu. Kuna uwezekano kuwa madai ya wanaume hawa ni kweli lakini umekuzwa kwa maneno haya kiasi cha kuhisika kuwa hamna ukweli wowote katika maelezo hayo. Urembo huu bila shaka si wa kawaida kwani huwavunja wanaume shingo wanapovutiwa na uzuri wa kiuno cha binti huyu.

Kauli hii inaibua maudhui ya uasherati unaoibuka mtu anapokuwa ameathirika kwa kileo. Bila shaka huropokwa na kuwa mwenye kutojali kiasi cha kujisahau na kwa hivyo hadhi yake hushuka. Walevi hawa hawaonekani kuepuka hali hii. Naye Fiona anatomia fursa hii kuziteka akili zao bakunja. Kama wateja, wanaendelea kwenda kwa Fiona kwa sababu ya kiuno chake cha mviringo na mvinyo wanaokunya kila siku.

Katika kauli ifuatayo chuku imetumika kufafanua juhudi za Mzee Temba katika kubadili maisha yake na ya jamii yake katika jamii hii. Wazungumzaji wametia chumvi katika mazungumzo yao kuelezea hali hii. Kwa mfano:

Mtu II: Mzee Temba anayeheshimiwa ndani na nje ya kijiji chetu kwa ukulima na ufugaji wake.

Mtu III: Hajui anafedhehesha ndugu zake wenye bidii ya mchwa ...(uk 6-7)
Dai kwamba Mzee Temba anaheshiwa ndani na nje ya kijiji limetiwa chumvi kwa sababu haiwezekani kuwa ni yeye pekee anayejishughulisha na kilimo kiasi hicho katika ulimwengu halisi. Hata hivyo Mtu II anataka wasomaji na wanaoshiriki naye katika mazungumzo kuamini kuwa hali anayodhihirisha Temba ni ya kupigiwa mfano. Aidha, ana maana kwamba hamna yeyote wa kiwango hicho katika ukulima katika jamii hii. Kauli tunazozirejelea ambazo zinatambulika kwa mkolezo katika mazungumzo baina ya Mtu I na Mtu II ni semi ziliotiwa chumvi. Ili kuzipa sifa za chuku, tumeteua maneno ‘ndani’ na ‘nje’ kwa kuyasoma maneno haya tunaona kuwa maneno haya yanapanua mawanda ya umaarufu wa Mzee Temba na kumfanya kujilikana kwa watu wanaoishi karibu naye na wale wanaotoka mbali naye.

Kauli hii kwa hivyo inadhihirisha kuwa Temba ni mzee anayeheshimika sana katika jamii hii. Usemi huu umetiwa chumvi unapotathminiwa kimuktadha kutokana na bidii na umaarufu wa kiwango cha kilimo alichokuwa nacho Mzee Temba. Katika ukiushi wa chuku hii ni kuwa Temba ni mzee anayejulikana katika jamii yake na jamii zinazoizunguka jamii hii. Sababu inayomfanya kuheshimika ni kuwa ana bidii na bidii hizo zinaonekana katika kilimo anachoendesha. Mzee Temba ni tofauti na wanajamii hii ambao wanajihusisha na wizi na unywaji pombe.

Wanawe Tonge na Lila vilevile wamefuata mkondo huo wake na kwa hivyo wanafanya bidii na kujizalishia mali. Tunaona Lila akija kumtembelea mamake mgonjwa akiwa na bunda la noti linaloibwa na Matari. Tonge vilevile anafanaya kazi mjini na pia amemstawisha mkewe nyumbani kwa kumnunulia ng’ombe wa maziwa. Hali hii inamfanya kuwa mwenye bidii na mwenye kujitegemea. Kauli hii katika maana yake kiushi inaibua maudhui ya uvivu na uzembe. Kauli inatolewa na Mtu II. Wanapoyasema maneno haya, hawapo kazini. Wanazungumzia bidii za wenzao na jinzi bidii hizo zinavyopondwa na Matari ambaye ni mwana wao.

Neno ‘uzembe’ lina maana ya ulegevu ambao tunaushuhudia kwa Matari na walevi wenzake. Hawapendi kufanya kazi na kwa hivyo wanaishia kumtegemea Matari anayeiba

kutoka katika aila yake na kutumia fedha hizo kuwanunulia pombe. Kutokana na uvivu na uzembe wanajamii hii wameshindwa kutenda kazi. Kupitia kauli hii tunaona kuwa uvivu na uzembe ni magonjwa yanayoonyesha kuwa jamii nzima imedidimia na mwisho itaangamia.

Kitendo hiki cha wizi ambacho Matari anawafanyia wazazi wake hakiwapendezi wanajamii hii wakiwemo walevi wenzake ingawa kwa kinaya wao wenyewe hawajioni kuwa wanachangia kuendelezwa kwa tabia hii ya uzembe na uvivu.

Usemi wa Mtu III kwamba wanawe Temba wana bidii za mchwa umetiwa chumvi. Miongoni mwa sifa za mchwa ni ushirikiano, bidi na utaratibu wa kufanyia mambo. Hali hii huwawezesha mchwa kufanikiwa kujenga kichuguu kikubwa ambacho hutumika kama makao kwao. Katika hali dhahania ya matumizi ya kauli hii ya Mtu III, tunaona sifa ya bidii ikiwafanikisha wanawe Temba. Tonge na Lila wanadhihirisha haya.

Katika nukuu ifuatayo tungependa kutathmini mchango wa neno ‘mjaalaana’ katika usemi anaotupa Mtu II.

Mtu II: Yule mjaalaana Matari tumwambae kama mgonjwa wa ukoma.
Hata salamu msimpe... (uk 7)

Katika ulimwengu halisi tukisema mtu ni mjaalaana bila shaka atachukuliwa kuwa yeye ni mtu aliye na laana nyingi sana.

Kwa mtazamo wa ukiushi tukizingatia muktadha tumehusisha laana na jaa la taka na kwa hivyo kuwa na ufasiri tofauti. Neno laana lina maana ya kukosa neema ya Mungu au ghadhabu ya Mungu. Tukimwangalia Matari kama mhusika tunagundua kuwa anaisababishia aila yake aibu. Anajihusisha na wizi wa mali ya babake na nduguye. Mbali na hili, Matari ni mzinifu kwani wanajamii hii wanaufahamu kuwa ni yeye aliyempachika Vero mimba. Usemi huu kwa hivyo una maana kuwa Matari ana laana nyingi sana. Ufasiri huu unatokana na matendo anayotimiza katika kazi hii tunayoirejelea. Tukirejelea Mtu II anaposema:

Mtu II: Hata nyie nyote mwajua kwamba Matari anafanya makosa makubwa...anaabisha ukoo wake, Matari.

Kwa hivyo ni dhahiri kuwa kitendo cha Matari cha kuwa mwizi hakiwapendezi wanajamii hii. Ndio maana Mtu II anaitamka kauli hii. Anawaibia wazazi wake vipuli vya trekta na kuvizuza, hali inayomrudisha nyuma Mzee Temba kwani analazimika kuviagizia kutoka ng'ambo. Mbali na hilo, Matari anajihusisha na kunywa pombe kila siku, ni mpenzi wake Fiona na mbali na hilo, anampachika Vero mimba. Bila shaka hizi ni laana nyingi. Kauli hii kwa hivyo inaibua na kuendeleza maudhui ya upotovu wa vijana. Matari anayerejelewa amepotokana hayajali maisha tena. Jambo la muhimu kwake ni kujifurahisha kwa kunywa pombe, wizi na uasherati.

Kauli hii kwa hivyo ni chuku ya kuonyesha kiwango cha upotovu alio nao Matari na hasara anayoiletea aila yake. Tabia ya Matari ya kuwa mtovu wa nidhamu inachangiwa na mamake, Mtu II pamoja na Fiona. Wamempa Matari majina chungu nzima. 'Matari kitindamimba, Mwanakindakindaki, Mburu Matari Hatari bin Temba.

Katika kiwango hiki tungependa kutathmini chuku katika kauli anayoitoa Matari anapozungumzia mali katika jamii yao. Ni muhimu kueleza kwamba ili mawasiliano yafaulu, lazima msikilizaji au msomaji aelewe ni katika muktadha gani usemi umeshiriki katika mazungumzo kwa wale wasiohusika. Hali hii hutokea katika kujaribu kukisia idadi tu. Maana hapa hujitokeza kuwa chuku kwa msemaji kutokuwa na idadi kamili ya kinachozungumziwa. Hebu tutathmini kauli ya mkolezo wa wino katika usemi wa Matari:

Matari: Isitoshe, kaka Tonge naye, shamba lake la kupigiwa mfano. Mifugo hawahesabiki. Zaidi ya hayo ana mke mrembo na sasa mja mzito sikwambii ile kazi afanyayo ya afisakilimo inayompa mapeni yasiyo hesabika.(uk 14)

Matari anatia chumvi kiwango cha mali ya Tonge ambaye ni nduguye kwa kudai kuwa shamba lake ni la kupigiwa mfano na vilevile mifugo hawahesabiki. Huenda ni kweli kwamba shamba la Tonge ni la kupigiwa mfano na lina mifugo wasiohesabika. Lakini si kweli kwamba mifugo hawa hawawezi kuhesabika, ni idadi tu haijatajwa. Ujumbe tunaoupata hapa ni kuwa Tonge ana mali mengi kutokana na bidii yake ya kujihusisha na

kilimo. Hali hii Matari anaifahamu na kwa hivyo anajigamba kwa wenzake kwao wanajiweza. Kauli hii vilevile yaweza kuthibitisha hali yake ya kujihusisha na wizi.

Chuku katika maneno haya anayoyasema Matari inarejelea uzembe wake. Amebakia kusifu vya nduguye ambaye ana bidii pamoja na mkewe. Ana mifugo ambao hawawezi kuhesabika kwani Matari anaweza kukadiria tu, ‘.. ana mke mrembo’ huyo si mke wa kawaida tu ila ni mke mwenye kutajika. Mwenye sura nzuri ya kuvutia na vilevile Tonge ana kazi nzuri ambayo ina mshahara mzuri. Matari kama kijana hana yote haya, hana mke, kazi na lolote alifanyalo ili kupata mtaji. Alichu nacho ni majina ya sifa tu. Chuku hizi katika hali kiushi zinazua na kuendeleza maudhui ya uwajibikaji. Tonge ana bidii kwa hivyo anajishughulisha na mambo ambayo yanamjenga kiuchumi. Shughuli hizi zinamwondoa katika kujihusisha na matumizi ya vileo. Anajinyima anasa kinyume na Matari anayependa vileo na anasa na hana kazi.

3.3 Tashbihi

Tashbihi ni ulinganishi wa moja kwa moja na ulinganishi huu hudhamiria kuisitiza sifa fulani na pia kutujengea picha ya aina fulani akilini. Ulinganishi huu huonyweshwa kwa matumizi ya viungio: kama, mfano wa, sawa na, mithili ya, tamthili ya, ja na kadhalika. Tashbihi vilevile ni mbinu ya uhusisho na ulinganishi ambapo vitu viwili huhusishwa baina ya neno kama, kama vile, useme, mithili ya, mfano wa na kadhalika. Tashbihi huwa na msingi wa kutafuta namna ya kuweka wazi maana, dhana, picha au hali fulani kwa mujibu wa ulinganifu wa kipicha.

Katika uchanganuzi wa kauli ya Mtu II tungependa kutathmini maana inayojitokeza kutokana natashbihi tulioidokeza mkolezo. Ufasiri mwafaka wa kauli ya Mtu II ambayo ni tashbihi imetumika kujenga picha ya Mtu I kwa kumfanya kudhihirisha sifa za mtoto ambazo miongoni mwao ni kikojozi. Hebu tutathmini kauli hii.

Mtu II: Nasikia mkeo an’lalamika siku hizi.... Ukilewa chakari unakuwa kikojozi.....unalowesha malazi kama kitoto.(uk 2)

Fasiri ya usemi huu inatoa maana katika muktadha wake wa matumizi. Maana hii ni maana dhahania kwa kuwa msingi wake ni mazungumzo na matendo ya wahuska katika matini hii.

Matumizi ya neno ‘kama’ yanatambulisha tamathali ya usemi ya tashbihi iliyotumika. Tashbihi ni mbinu ya uhusiano na ulinganishi ambapo vitu viwili huhusishwa baina ya neno kama; kama vile, useme, mithili ya, mfano wa, na kadhalika. Katika kauli hii, Mtu I anachorwa kuwa na sifa na tabia zinazosawiriwa na mtoto ambaye bado ni mtegemezi kwa mzazi. Sifa hizi anazo Mtu I kwani anakojoa kitandani alalapo. Haya hutokea baada ya kulewa chakari kwani hali hiyo humpelekea kujiingiza katika kufanya mabaya ama upumbavu. Hali hii inamfanya Mtu I kuwa mzigo kwa jamii yake haswa mkewe ambaye anavumilia madhila ya aina hii. Tashbihi hii inaibua matumizi na athari za dawa za kulevya. Dawa za kulevya zimeharibu maisha ya wengi na hata kuharibu uhusiano uliopo baina ya wazazi na vijana na hata mke na mume. Hali hii inasababisha kutowajibika kwa wanaohusika katika ulevi wa aina hii kwani wamezitelekeza familia zao jinsi alivyo Mtu I. Kulingana na muktadha wa kauli hii tunashuhudia kuwa Mtu I amejisahau kiwango cha kukojoa kitandani. Tunaweza kufikia uamuzi kuwa hata majukumu yake ya kuwa mume kwa mkewe vilevile yamepuuzwa. Bila shaka dhiki hizi ni za mwanamke anayeishi na mume wa aina hii.

Katika mzungumzo baina ya Mtu I na wenzake nyumbani kwa Fiona, kunaibuka ubishi kuhusu tabia za Matari. Wizi wa Matari umekuwa kero hata kwa wafaidi wake. Hali hii inazua wosia kutoka kwa Mtu II ambaye anatumia tashbihi kuwafikisha ujumbe wanaomsikiliza. Hebu tuitathmini kauli hii ya Mtu II tuliyoitambulisha kwa mkolezo hapa chini.

Mtu II: Yule mjaalaana Matari akija hapa tumwambae kama mgonjwa wa ukoma. Hata salamu msimpe. ... (uk 7)

Katia ulimwengu halisi maana ya tashbihi hii haiwezi kumfaa msomaji. Maana kiushi inajitokeza kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya kauli hii tuliyoitambua hapo juu.

Matumizi ya neno ‘kama’ yanaitambulisha tashbihi katika usemi wa Mtu II kuwa tashbihi. Katika ulimwengu halisi ni vigumu kufasili maana ya tashbihi hii. Hatujui ni kwa nini Mtu II angependa wamwambae Matari kama mgonjwa wa ukoma. Hata hivyo, katika ulimwengu dhahania tunajengewa picha ya mgonjwa anayeugua ukoma. Ukoma huwa ni ugojwa hatari wa kuambukiza wa mabatomabato ambao huharibu

mishipa ya fahamu na kukata viungo vya mwili. Hukata sehemu za mwili kama vile vidole na kumwacha mtu bila sehemu hizi za mwili. Kwa hivyo anayeugua ukoma hutisha na kutengwa na wanaoishi naye. Kauli hii bila shaka inatujengea picha ya jinsi Matari alivyo hatari kama ugonjwa wa ukoma. Sifa ya ugonjwa huu ya kukata viungo vya mwili inalinganishwa na sifa hatari ya Matari ya kuwapunja watu mali yao. Hali hii ni hatari na kwa hivyo Mtu II anaonelea kuwa Matari na tabia yake ya wizi hafai kukubalika katika jamii na ni vyema ikiwa jamii itamuepuka kwa kumtenga. Ufasiri huu tunaupata kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya kauli hii ya Mtu II.

Mtu I anasema ‘hakuna dawa kama Matari’. Kauli hii inaonyesha kiwango cha utegemezi alichomo Mtu I kwa Matari. Kukosekana kwake kunamfanya alalamike kwa kuwa hapati kileo. Katika ulimwengu halisi, dawa ni vidonge majimaji au unga anaopewa mgonjwa ili kuponya au kutuliza maumivu mwilini. Ufasiri huu kwa hivyo hautupi maana katika ulimwengu halisi. Kimuktadha ni kuwa Matari ni mkarimu kiwango cha kuweza kuwanunulia walevi kileo bila ubaguzi. Ajapo huwa ni tiba ya wengi kwani yeyote aliyefika hapo ili kupewa kinywaji lazima na cha Matari kiwepo. Kwa hivyo ulevi wao ni wa ubwete, kwani Matari ndiye hugaramia malipo haya.

Hata hivyo Mtu II hakubaliani naye. Hapendezwi na tabia ya wizi ya kuiba kisha kutumia fedha alizopata kunywa pombe. Kwa hivyo Matari ni hatari kwa jamii yake kwani ni chanzo cha kudidimiza maendeleo na vilevile tisho kwa kizazi kijacho kwani akiwaambukiza wadogo wake tabia hiyo jamii nzima imo taabani. Hii ni maana kiushi ya kauli hii kwa kuwa imetokana na muktadha wa matumizi ya kauli unayoirejelea.

Katika usemi ufuatao, Mtu II anatumia tashbihi kuonyesha umuhimu wa Matari kwao. Anataeleza:

Mtu II: Sote twakuenzi kama mboni ya jicho. Usibadili mwendo na mavazi, bado twakupenda.

Matari: Acha kuniuliza maswali ya kijinga kama polisi. (uk 12)

Mboni ni sehemu ya jicho ambayo hufanya kazi ya kuona katika jicho. Kwa hivyo ni kiungo maalum na muhimu cha jicho chenye jukumu kubwa. Kazi hii ya mboni ndiyo inayofanya Matari kulinganishwa na mboni ya jicho kwani bila mboni kutakuwa na

upungufu fulanifulani kwa yule anayeitegemea mboni. Kwa hivyo kauli hii inaonyesha kiwango cha mapenzi waliyonayo Mtu I, Mtu II na Mtu III kwa Matari. Kwa hivyo wana madai kuwa wizi wa Matari bado unawafaa. Tabia ya wizi aliyonayo Matari inawafaidi wanaomtegemea na kwa hivyo kumfanya Matari kuwa rafiki wa thamani kubwa kwao.

Mtu II na wenzake wanamtegemea Matari kukidhi mahitaji yao ya pombe. Bila Matari basi tamaa ya pombe au kiu haitoshelezwi. Hali hii inamfanya Matari kuwa kipenzi chao. Haya yanatokea Matari anapofika kwa Fiona baada ya kulala kwa Vero. Anapoulizwa vipi? Anajibu kuwa hataki maswali ya kijinga kama ya polisi.

Katika jamii nyingi za Afrika uhusiano baina ya raia na polisi huwa si wa kirafiki. Mara nyingi huwa ni uhusiano wa kudhulumu na wenye chuki. Hali hii imetokana na mazoea ya polisi kuwasingizia watu makosa ya uvunjaji sheria pamoja na kudai hongo miongoni mwa dhulma nyinginezo kwa mfano vipigo na mauaji ya kiholela kwa wasiokuwa na hatia. Udhaifu huu umeitenga idara hii na wananchi wanaofaa kuhudumiwa. Matari ni mwizi na kwa hivyo ni mteja wa kitengo cha polisi mara kwa mara. Vilevile kushiriki kwake katika unywaji pombe haramu kumemfanya kuwa mteja wa pekee wa polisi kwani pombe anayotumia ni haramu. Hali hii inamfanya kuchukulia kuwa polisi na mbinu zao za kudadisi uvunjaji wa sheria ni za kukandamiza. Kwa kuzingatia ulimwengu halisi, mjinga ni mtu asiyejua kitu, fala, juha au gulagula. Tamko hili vilevile hutumiwa kuonyesha dharau kwa anayeambiwa. Hali hii inadhihirika katika utambuzi wa Matari kwa polisi.

Tashbihi hii inaibua swala kuhusu utaratibu wa polisi wa kudadisi kesi ya mhalifu anapotiwa mbaroni. Kauli hii inayosemwa na Matari inadhihirisha udhaifu wa mbinu hii na kufahamisha wasomaji kuwa kunapotokea udadisi unaofanywa na polisi kwa kweli hakuna utaratibu unaofuatwa ili kupata chanzo cha uhalifu uliotekelezwa isipokuwa maswali yasiyokuwa na mwelekeo. Ndiposa Matari anayaita maswali haya ya kijinga. Kauli hii yenye tashbihi kwa hivyo inarejelea sifa na tabia za polisi.

Katika kauli tunayoichunguza hapa chini, ni muhimu kupata maana ya neno riziki na bahati katika hali ya ulimwengu halisi na ulimwengu dhahania. Hebu tutathmini kauli hii:

Matari: Riziki kama bahatihuitambui ijapo ati. Nikazichukua bwana. Sikuiba. Ahaah! Hata kidogo.

Mtu II: Ngapi

Matari: Eflu tisini. (uk 14)

Riziki ni baraka na mafanikio anayopewa mtu na Mungu; majaza. Riziki ni mapato yatokanayo na kazi ili kumwezesha mtu kuishi. Kwa upande mwingine bahati ni hali ya mafanikio au tukio zuri au baya. Matari anapotaja kauli hii, anarejelea methali.

Methali hii ni ya kitashbihi. Maana ya methali hii ni kuwa mtu haitambui riziki imujiapo, huweza ikamjia ghafla kama ajali itokeavyo. Katika kauli hii, Matari hatarajii kupata pesa taslimu elfu tisini kwa wakati mmoja imfanyikiavyio siku hii Lila ajapo kumshughulikia mamake. Pesa hizi anazipata kwa njia rahisi kwani hazitolei jasho anaziiba chumbani pa mamake. Methali hii ya kitashbihi katika ulimwengu halisi, ina maana pana. Yaweza kumainisha mtu ambaye anajishughulisha na kazi yake ya kawaida kisha akabahatika kuokota pesa au mtu kumruzuku au hata kuangukia pato kubwa baada ya bidii zake. Hali hii ni kinyume na ya Matari kwani Matari ni mwizi na wizi wake siku hiyo umempa pato kubwa kinyume na matarajio yake. Katika hali kiushi kulingana na muktadha wa kazi hii tunatambua kuwa Matari hapendi kufanya kazi. Anatarajia kuangukiwa na riziki au bahati jinsi Mungu huwaruzuku waja. Aidha, riziki au bahati hutoka kwa Mungu. Hali hii ndiyo anayoirejelea Matari. Katika hali halisi tunajua kuwa riziki yoyote haiji bure. Lazima uitolee jasho. Hatuoni Matari akishughulika kufanya kazi ili kuzipata pesa hizi. Methali hii ya kitashbihi tukimrejelea Matari inaibua maudhui ya upotovu wa vijana. Matari hashughulikii ugonjwa wa mamake jinsi wenzake wanavyoushughulikia. Ila anazua utata zaidi wa kuwahangaisha aila yake na kuwaongezea madhila.

Temba vilevile anatumia tashbihi katika usemi wake tulioutambulisha kwa maneno yaliyokolezwa hapa chini.

Temba: Acha kunizungusha kwa maneno. Wanipeleka huku na huku kama mpira uwanjani kwa nini? (uk 26)

Ufasiri wa tashbihi katika kauli ya Temba katika usemi ulioko hapo juu hauibui maana bila muktadha wa kauli hii katika matini teule.

Neno ‘kama’ linaitambulisha tamathali hii. Katika matumizi ya kawaida Mzee Temba si mpira kwa hivyo Lila hawezi kumpeleka huku na huko kama mpira uwanjani. Ukiushi tunaoupata hapa ni kuwa, Lila hataki kumwambia babake habari alizokumbana nazo asubuhi hiyo kumhusu Matari moja kwa moja. Kumbuka Matari amekuwa mzigo kwa familia yake; ni kikwazo kwa maendeleo ya jamii hii. Mbali na hayo kitendo kilichotokea kimeigusa mali ya nduguye. Hali hii inamfanya Lila kuwa katika hali tata. Inambidi Lila kutokuwa wazi katika habari anazotaka kumpasha babake. Hali hii inamfanya Mzee Temba kupoteza subira na kwa hivyo kuzua usemi huu. Kabla ya haya Lila hakupenda kutumwa kudai kodi wakaazi ambao hawataki kulipa kodi ya nyumba.

Kimuktadha tunaona heshima aliyonayo Lila kwa babake. Hataki kupasua mbarika kwa mkurupuko. Inabidi atafute njia ya kumweleza babake habari hii kwa njia halisi kwani si habari njema na zaidi ya hayo inamhusisha Matari ambaye ni mmoja wao katika jamii hiyo. Babake anapenda mambo yanayoelezwa moja kwa moja. Kauli hii inaibua maudhui ya maadili katika jamii.

Kwa mujibu wa mbinu hii ya tashbihi tunawaona Temba, Mama na Mtu II wakitoa maelezo yao kwa wasomaji au hadhira. Hali hii inaondoa uchapwa katika matini. Hebu tutathmini kauli hizi za wahusika hawa ambazo ni tashbihi:

Temba: Naye mjanja kama nini Jefule! Huwezi kupata ushahidi wowote wa kumtia hatiani; (uk 27)

Mama: Yaani polisi wamemkamata mwanangu nawe umesimama hapa tu kama nguzo ya umeme?Zumbukuku wewe! (uk 33)

Mtu II: Anatokwa na udenda mdomoni kama kondoo anayeelekezwa machinjioni. (uk 35)

Usemi huu wa Temba ni usemi ambao ni tashbihi. Neno ‘kama’ linautambulisha usemi huu. Katika ulimwengu halisi kauli hii kutoka kwa Mzee Temba haina maana yoyote. Hatuwezi kufasili kwa nini Temba amwone Jefule kuwa mjanja kiwango cha hata kukosa kilinganishi. Tunaposoma matini tunagundua kwamba Jefule hushirikiana na Matari katika wizi wa ng’ombe. Katika kipindi hiki chote Jefule ameshirikiana na Matari kuiba ng’ombe wa Temba lakini hakushikwa wala kushukiwa. Siku ya arubaine imfikiapo,

haepuki. Matari aibapo ng'ombe, huwauza kwa Jefule ambaye ana bucha pale kijijini. Kawaida ya sheria ni kuwa mtu apatikanapo na mali ya wizi, yeye vilevile ni mwizi. Tendo hili la wizi wa ng'ombe limefanyika katika kijiji hiki kwa muda mrefu. Mzee Temba amewapoteza ng'ombe wengi ila hajawahi kufikiri kuwahi kichinjioni asubuhi ili kuwapata ng'ombe wake walioibiwa. Wasemavyo wahenga 'siku za mwizi ni arubaini'. Jefule anauziwa ng'ombe na Matari usiku na kwa bahati mbaya anakisahau kichwa cha ng'ombe huyo machinjioni. Vero ni mwanamke mwenye busara na kwa hivyo aamkapo na kumkosa ng'ombe wake zizini, wazo linalomjia mwanzo ni kuwahi machinjioni ambapo anakutana na kichwa cha ng'ombe wake kikiwa kimesahaulika pale. Kauli hii yenye tashbihi inaibua maudhui ya uozo wa wizi miongoni mwa jamii hii.

Kauli 'umesimama hapa tu kama nguzo ya umeme' ni kauli ambayo ni tashbihi. Kauli hii imetambulishwa kwa neno 'kama'. Neno nguzo lina maana ya kipande cha mti au chuma kilichosimamishwa wima ardhini ili kuhimili au kushikilia kitu kingine kama vile paa la nyumba au nyaya za umeme. Maelezo haya katika ulimwengu halisi hayatufaidi. Katika ulimwengu dhahania, ni muhimu kurejelea muktadha wa matumizi ya kauli hii. Kauli hii imetamkwa na mama baada ya kupata ujumbe kuwa Matari ametiwa mbaroni baada ya kupatikana kuwa aliiba ng'ombe na kumuuzia Jefule. Hali hii haimpendezi mama na kwa hivyo anamwona Lila, kutomshughulikia Matari ilhali yumo matatani. Tabia ya Matari ni tabia isiyokubalika katika jamii yoyote ile. Mamake Matari anadhihirisha sifa ya utendekezaji wa mzazi kwa mwana kwani tunamwona akichelea vitendo vya Matari ambavyo bila shaka hata yeye havipendi. Mwanzoni tumemshuhudia akimsomesha Matari Bibilia ili aokoke na kuachana na wizi. Kwa hivyo hali ya Lila kufananishwa kusimama kwake kama nguzo ni ishara ya kuchanganyikiwa na kutokuwa na uamuzi wa kumsaidia Matari. Lila ameonja kiboko cha Matari kwani kabla ya Matari kukamatwa kwa sababu ya wizi wa ng'ombe, alikuwa amemwibia Lila pesa taslimu shilingi elfu tisini. Kauli hii yenye tashbihi inaibua maudhui ya malezi ya mzazi kwa mwana. Mama amemtendekeza Matari na kwa hivyo yeyote ambaye hamshughulikii Matari kutokana na maovu anayoyatekeleza anachukuliwa kuwa kama nguzo ya umeme ambayo hubakia kusimama kuwe na hatari au usalama. Tunashuhudia katika matini mama akimtetea mwanawe ingawa anafahamu kuwa kitendo alichofanya mwana ni cha uhalifu na kinachofaa kurekebishwa kwa kupewa adhabu fulani.

Kauli ‘anatokwa na udenda mdomoni kama kondoo anayeelekezwa machinjioni’ ni tashihisi. Kauli hii inatujengea picha ya uoga alionao Matari baada ya kunaswa na mkono mrefu wa serikali.

3.4 Tashihisi

Msokile (1993) ana maoni kuwa tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu hupewa sifa zote au baadhi ya sifa za binadamu na kuonekana kutenda kama binadamu. Hiki kitu kisicho na tabia ya kibinadamu hupewa sifa, tabia, sura au matendo ya kiuhaiau kiutu na kibinadamu. Mara nyingi tashihisi hutumiwa kumvutia msomaji na kukwepa kuweka wazi maana au wazo. Hebu tutathmini kauli ifuatayo.

Katika ulimwengu halisi viumbe kama binadamu, wanyama na wadudu ndio wana uwezo wa kuuma. Kauli ya Mtu I tuliyoitambulisha kwa kukoleza ni tashihisi. Hebu tuitathmini:

Mtu I: Agh! Linakuumia nini hilo?..... usiyoiramba inakuwashiani? (uk 5)

Katika ulimwengu halisi maneno hayana uwezo wa kuuma. Tunapousoma usemi huu tunafasili kuwa maneno yana uwezo wa kuuma kwani maana tunayopata ni hiyo.

Kwa kurejelea muktadha wa kauli hii, tunatambua kuwa Mtu II ana wasiwasi kuhusu tabia ya Matari ya wizi. Hali hii inamfanya kuwasihi wenzake kuuonea fahari wizi wa Matari. Hata hivyo Mtu I haonekani kutishwa na hali ya hatari inayoweza kumkumba Matari na kwa hivyo anaitumia tashihisi ‘linakuumia nini hilo...’ kumzima Mtu II. Kutokana na kauli hii ya Mtu I tuna ufasiri kwamba vitendo vya wizi anavyotekeleza Matari havimpi wasiwasi Mtu I na kwa hivyo haoni haja ya yeyote katika jamii kuhangaika kwa sababu ya vitendo vya wizi vya Matari. Msimamo huu wa Mtu I ni wa kuiumiza jamii hii. Yeye haangalii upande hasi wa Matari kwa jamii, ila anangalia faida anayopata yeye binafsi ya kununuliwa kileo kila uchao kutokana na fedha za wizi za Matari.

Katika kauli zifuatazo za Matari na Lila kuna tashihisi. Tumezitambulisha kauli hizi kwa kuzikoleza ilivyo hapa chini.

Mtu I: Matari afeje?

Matari: *(kwa furaha kubwa ya ghafla)* Ohoo! Sasa naelewa. Mimi Matari sifi. Kifo hakitawahi kunionja mimi Matari binTemba....kifo? (uk 10)

Lila: Ugonjwa mbaya sana, ugonjwa usiosikia dawa kama kidondandugu.(uk 18)

Kuonja ni kutia kitu kidogo mdomoni ili kujua ladha yake. Kwa hivyo binadamu tu ndiye mwenye uwezo wa kuonja kitu kwa mfano chakula. Katika ulimwengu halisi kauli ‘kifo kumwonja Matari’ ni kauli isiyoleta maana yoyote kwani kifo hakina uwezo wa kufanya hivyo. Miongoni mwa dhiki za kifo ni kuwa kitokeapo, humnyakua kipenzi cha watu. Katika hali hii tunaona kuwa Matari anajaribu kupima kiwango cha mapenzi walichonacho wafaidi wake kutokana na wizi wake kwake. Mtu I, Mtu II na Mtu III wanamtetea na hata kusahau uovu wake kwa jamii hii. Wote wanakiri kuwa Matari hawezi kufa. Kauli hii kwa hivyo inathibitisha unafiki wa watu hawa.

Kauli ya Lila katika ulimwengu halisi inafasiliwa kuwa ugonjwa una uwezo wa kusikia mfano wa kidonda ambacho ni sugu. Katika hali kiushi, imetumika kuwasilisha ujumbe tofauti kabisa. Tunaufahamu kuwa ugonjwa hauna hisi ya kusikia dawa lakini mtu anapougua na kupimwa na daktari bila shaka kinacholeta kasoro katika mwili hugunduliwa. Kisha anapewa maagizo ya matumizi ya dawa na daktari. Kauli hii kwa hivyo inamrejelea Matari ambaye mara kwa mara anapewa ushauri kuachana na tabia ya wizi lakini ametia sikio nta. Tunamwona mama akimsomesha Biblia ili aachane na tabia hii, babake pia amezungumza naye wakiwemo Tonge pamoja na Lila ambaye kaibiwa elfu tisini na yuyu huyu Matari. Kwa hivyo ugonjwa unarejelea tabiaya wizi aliyo nayo Matari. Aidha, dawa ni washauri wake wakiwemo wanajamii wazazi pamoja na nduguze. Kidondandugu ni kilinganishi cha usugu wa tabia hii ambayo Matari ameizoea na kukataa kuiacha. Ujumbe tunaopata ni kuwa aila yake hawapendezwi na hii tabia na kwa hivyo wamejaribu mbinu zote wawezavyo kumwepusha na mazoea haya lakini ni vigumu.

Kauli hii kwa hivyo inaibua maudhui ya swala la malezi ya mtoto. Matari ni kitindamimba na kwa hivyo waliomzingira wana jukumu kubwa la uwezo wa kuathiri maisha yake. Katika hali hii, wazazi ni washauri na wenye ushawishi mkubwa. Ili kujaribu kumkuza mtoto ambaye ana maadili na mwenye kutii amri akiwa chini ya wazazi na hata mbali na wazazi. Tunamwona Matari akikaidi haya , ishara kwamba kumekuwa na pengo la malezi mema.

Mama: Lakini ujue amri ya umri. Wewe si mtoto tena. Utakuja kuchelewa kuolewa. Ubaki unahangaika kama usipotahadhari.

(uk 31)

Katika kauli hii neno ‘amri’ limepewa uwezo wa kuzungumza na hata kutoa maagizo ambayo ni lazima yatekelezwe. Vilevile tunaweza kusema kuwa umri una matakwa ambayo ni maagizo ya lazima. Kauli hii haiwezi kutupa maana kulingana na matumizi ya maneno katika hali halisi. Lakini kulingana na muktadha wa matumizi tunaona maneno anayotamka mama kwa mwana anapotaka kujua aliyekuja kumposa Lila. Lila naye hayuko tayari kuyazungumzia hayo nayotaka mama. Hali hii inamtia mama wasiwasi kwani utamaduni unamtaka Lila awe ameoleka kufikia sasa. Hali hii ya yeye kuwa kimya kuhusu swala la ndoa, inaibua mawaidha haya anayotoa mamake.

Hali inayopelekea usemaji wa kauli hii si muhali. Tunaona udhaifu kwani mzazi mamake Lila anafaa kumwalika bintiye kisha waketi kitako na kushauriana kuhusu swala hili la kutaka aoleke. Kauli hii kwa hivyo ina maudhui mawili inayoibua. Kwanza ni jukumu la mzazi katika malezi, jukumu la mzazi linaanzia wapi na kuishia wapi. Je, mzazi ana uwezo wa kuamua ni wakati au umri gani wa bintiye kuolewa? Vilevile swala la ndoa na uchumba linaibuka. Lila anaogopa dhiki wazipatazo walio katika ndoa. Tunamwona akimwambia mamake haya kuwa hataki kusumbuliwa na mume. Huenda madhila wanayopitia waliooleka yanamsuta na kwa hivyo kumtoa haja ya kutaka kuolewa.

Mtu I: Yote mamoja. Vyovyote vile mali inajila yenyewe kwa yenyewe.

(uk 38)

Hebu tutathmini tashihisi hii. Katika hali halisi mali haina mdomo na kwa hivyo haiwezi kujila. Kwa kawaida mali huwa na mwenyewe na katika muktadha wa matumizi ya tashihisi hii tunaona kuwa Matari ni mwanawe Temba. Temba ni mzee mwenye bidii na kwa hivyo ana mali mengi. Mwanaye Temba ambaye ni Matari ana mkono mrefu: mwizi.

Matari hana adabu anawaibia aila yake na kuwaweka taabani. Katika kauli ya Mtu I tuliyoitambulisha kwa mkolezo hapo juutunafasili maana kuwa Matari ambaye ni mwanaye Temba anaiba mali ya Temba na kwa hivyo ni sawa na kuwa Temba hapotezi kwa kuwa mwanawe ndiye anayechukua mali ile ingawa kwa kuiba. Maudhui yanayoibuka na kuendelezwa hapa ni ya jukumu la mzazi katika malezi chambilecho methali mchelea mwana kulia hulia yeye. Temba hana haja ya kulia kwani kama mzazi hafai kuchoka kumwadhibu mwanawe. Ni kinaya kwa Mtu I na Mtu II wanaojadili haya na ni wafaidi wa wizi wa Matari na vilevile wana udhaifu wa unywaji pombe kupindukia.

Tamko la Temba lililokolezwa hapa chini ni tashihisi. Tunajaribu kuangalia maana inayojitokeza kwa kuyarejelea maneno uamuzi na harara. Hebu tutathmini kauli hii:

Temba: Usije ukamwatuamoyo bure kwa uamuzi wenye harara.

Tonge. Maji nimeyavulia ngua sharti niyaoge. (uk 48)

Kamusi ya Kiswahili Sanifu ina maelezo kuwa harara ni vipete vidogo vidogo vinavyomtoka mtu mwilini kwa sababu ya joto au ni michubuko ya mapaja kwa sababu ya joto. Maelezo haya ni ya ulimwengu halisi. Kauli tunayoisoma katika usemi huu wa Temba ina uhuishi. Neno uamuzi limepewa uwezo wa kushikwa na ugonjwa wa harara. Katika ulimwengu halisi wa matumizi ya maneno haya si rahisi hali hii kuwezekana. Lakini katika ulimwengu dhahania ambao ni ulimwengu wa muktadha wa matumizi ya usemi huu tunapata ukiushi katika maana. Bila shaka sifa moja ya harara ni kuwa mtu anapotokwa na harara mwilini huwa hana utulivu. Kwa hivyo tumechukulia kuwa uamuzi wenye harara ni uamuzi ambao umefanywa bila makini na usio na busara yoyote. Hauna makini. Kwa hivyo ni uamuzi unaomiza upande mmoja. Kimuktadha Temba, ambaye ni babake Tonge anamshauri mwanawe kuyatafakaria maamuzi anayotaka kufikia. Anaona kuwa wao ni ndugu na kwa hivyo haina haja Tonge kumchukulia Matari aliyemwibia ng'ombe hatua kwa kuwa wanatoka katika tumbo moja. Tonge anasisitiza kuwa ni lazima amchukulie nduguye hatua. Kauli hii inazua maudhui ya malezi ya mzazi kwa mwanawe. Temba anamtendekeza Matari na kwa hivyo anaona kuwa ni vyema nduguye kuitupilia mbali kesi hiyo. Anausingizia ugonjwa wa mama yao ingawa hakusudi ni kumwambia Tonge kumsamehe nduguye moja kwa moja. Hali ya

kutetendekezwa kwa Matari kunamfanya afanye mambo bila kukadiria matokeo au athari za vitendo vyake. Hajali ikiwa yatakuwa mabaya au la.

Katika kiwango hiki tungependa kuchanganua usemi wa Askari I ambaye ametumia methali ya kitasihishi.

Tonge: Basi ombi.

Askari I: Kama ni ombi kumbuka mti hauendi ila kwa nyenzo.

Tonge: Naenda zangu na ukitakacho hupati. (uk 49)

Methali ‘Mti hauendi ila kwa nyenzo’ ina uhuishi. Maana ya methali hii ni kuwa haiwezekani kulisukuma gogo au pande la mti bila kuwa na nyenzo a kufanya hilo. Methali hii hutumiwa kwa jambo ambalo haliwezi kufanyika au kufanikiwa bila ya kuwepo kwa vitu fulani au taratibu zifaazo kulifanyia. Katika maelezo haya hatupati maana yoyote kwa kuwa maelezo haya ni ya ulimwengu halisi.

Kauli hii ina uhuishi. Kawaida, katika ulimwengu halisi mti huwa hauna uwezo wa kwenda. Katika ulimwengu dhahania kuna ufasiri tofauti kabisa. Jambo linalozuliwa na kauli hii ni kuwa askari huyu alitaka hongo ili kumtimizia Tonge matakwa yake ya Matari kuwekwa kizuizini. Tonge anakataa lakini baada ya kutafakari kidogo anarudi na kumpa askari mlungula. Kauli hii bila shaka inaibua maudhui ya ufisadi uliokithiri katika idara ya ulinzi inayofaa kuwatumikia wananchi wote bila malipo. Vilevile inatufahamisha kuwa utoji wa hongo ni kosa la anayetoa na anayepoke. Tunaona askari na Tonge wakivunja Sheria hadharani.

Askari I: Sheria hairuhusu.

Mtu III: Sheria kitu gani? Sisi hatuheshimu sheria inayowanyonga wanyonge. (uk 57)

Ukiushi tunaupata katika kauli hii ni kuwa sheria za jamii hiyo hazilengi kutoa haki kwa wanajamii hii. Hali hii inaudhi kiasi kwamba Mtu III anampinga Askari I anayehakikisha kuwa wanajamii hawavunji sheria. Hii ni kejeli kwa kuwa wao wameenda katika kituo cha polisi kudai Matari aachiliwe huru licha ya yeye kuwa mhalifu. Tunajua kuwa polisi ni chombo cha serikali kilichopewa jukumu la kuhakikisha usalama wa raia na mali zao.

Kutokana na ukweli halisi wa ukoloni mkongwe, katika jamii hii kuna baadhi ya watu ambao wanawachukulia polisi kuwa ni maadui wao. Kauli hii inathibitisha haya:

Mtu I: Mpokonyeni bunduki.

Kejeli hii inajidhihirisha wazi kwani wanajamii hii wana machungu ya kutaka Matari aachiliwe. Vilevile shutma zao kwa polisi zinadhihirisha haya.

3.5 Oksimora

Ili kufasili dhana ya oksimora, maelezo ya van Peer (1986), Van Peer na Hakemulder (2006) pamoja na Wamitila (2008) yatatufaa. van Peer na Hakemulder wanasema oksimora ni tamathali ya usemi ambayo huleta ama kuunganisha maneno mawili yenye mgotano ambayo licha ya kuwa na mgongano, huleta maana fulani katika usemi ilimotumika. Wanatoa mfano wa ‘chungu tamu’.

Shen (1987) ameanisha aina mbili za oksimora. Oksimora ya moja kwa moja na oksimora isiyo ya moja kwa moja. Oksimora ya moja kwa moja hutambulika kwa sifa kwamba maneno mawili yaliyo na mgotano huwa na nominokuu na kivumishi. Maneno haya huwakilisha antonimia ambazo ni za moja kwa moja. Antonimia za moja kwa moja ni leksimu mbili za maneno ambazo huwakilisha maneno yenye kinyume katika kipimo cha aina fulani kwa mfano katika oksimora ‘baridi moto’ kipimo tunachozingatia katika hali hii ni ‘joto’ au katika oksimora ‘maji makavu’ kipimo cha kuzingatiwa ni ‘maji’. Kwa hivyo antonimia hizi huwakilisha maneno yaliyo na viwango tofautitofauti vya kinyume.

Katika oksimora isiyo ya moja kwa moja maneno mawili yaliyo na mgotano huwa si antonimia za moja kwa moja ila kinyume hutokana na haiponimia. Haiponimia ni maneno katika lugha yaliyo na maanakuu au tunaweza kuyaita maneno makuu. Kwa mfano haiponimu ‘mnyama’ ina fahiwa mbalimbali kama vile farasi, mbuzi na paka. Neno paka laweza kuwa na fahiwa kwa mfano paka wa kawaida na paka mapepe. Kwa hivyo oksimora isiyo ya moja kwa moja ni oksimora ambayo huwakilisha haiponimu ya antonimia ya kauli au neno jingine. Maoni ya wataalam hawa yanaoana na ya Wamitila anayesema: Katika oksimora vitu viwili huwekwa pamoja ambavyo huwa katika hali ya

kugotana. Kimsingi vitu hivi viwili huwa vinakinzana. Oksimora na kweli-kinzani hufanana isipokuwa oksimora huwa na ubanifu mkubwa. Oksimora huwa na maneno mawili yaliyogotanishwa ilhali kweli kinzani huhusisha sentensi au kauli pana zaidi. Oksimora sanasana huwa maneno mawili yenye kugotana Kwa mfano; *Raha Karaha, Chungu Tamu, Asali Chungu* na kadhalika.

Wamitila (2003:172) ana maoni kuwa oksimora ni dhana inayotumiwa kuelezea aina ya kwelikinzani ambayo ni fupi mno yaani ni kwelikinzani iliyobanwa. Anasema kuwa oksimora hujengwa kwa maneno mawili yaliyowekwa pamoja na ambayo hayapatani au hayaingiliani kwa kawaida. Anwani ya tamthilia tunayoithmini kitamathali ni oksimora. Anwani hii ni: *Mbaya Wetu*. Hii ni oksimora isiyo ya moja kwa moja kwani tunarejelea haiponimu ya neno ‘mtu’. Mtu anaweza kuwa mwizi, mlevi n ahata mkarimu. Matari anadhihirisha kuwa mwizi katika jamii yake ila kwa Vero, Fiona, Mtu I, Mtu II na Mtu III, Matari ni mkarimu. Vero anauona uzuri wake kutokana na ujauzito alionao. Waliobaki ni wafaidi wa pesa alizoiba. Tunadadisi haya kutokana na maneno haya mawili yenye mgotano. Neno ‘mbaya’ lina mofu {m} ya umoja na mofu {baya} ili kuleta muundo wa:

$$\{m\} + \{baya\} \longrightarrow \{mbaya\}$$

Neno ‘mbaya’ lina maana ya mtu muovu, wa kuchukiza au wa kudhuru au wa shari. Hizi ni maana katika ulimwengu halisi. Nalo neno ‘wetu’ ni kivumishi kimilikishi cha nafsi ya kwanza hali ya wingi. Maneno haya mawili yakiwekwa pamoja yana mgotano kwani katika hali halisi binadamu hapendi kujihusisha na kitu chochote kilicho na doa au dosari. Kwa kurejelea muktadha wa matumizi ya kauli hii tunaona kuwa jamii inayozungumziwa katika tamthilia ya *Mbaya Wetu* inamtetea Matari. Matari ni zao la utamaduni wa jamii hii kwani amezaliwa na kukuzwa katika jamii hii. Wanakijiji wakiwemo Mtu I, Mtu II Mtu III, Fiona, Vero, Temba na mkewe wanamtetea Matari akiwa korokoroni na hata anapofikishwa mahakamani. Mtu I, Mtu II na Mtu III wanadai kuwa Matari ni mzuri kwani aibapo huuza alichioa kwa bei ya kutupa na kuwanunulia kinywaji. Matokeo ya matendo haya bila shaka yana ukinzani mkubwa. Jamii yenye maadili haimkubali mtu mwenye tabia kama hii.

Hebu tutathmini kauli zifuatazo:

Mtu III: Eeh! Nchi hii imeangamizwa na tabia hii ya kuhalalisha haramuna kuharamisha halali... Mambo mtayabirua hivi hadi lini? Mnatuza wanaostahili kutwezwa na kuwatweza wanaostahili kutuzwa. (*anatema mate sakafuni*)...Mna uwendawazimu nyie? (uk 5)

Hebu tutathmini oksimora inayojitokeza katika kauli ya Mtu III kama ilivyo hapo juu. Kwa kuzingatia maoni ya Shen (khj), hii ni oksimora ya moja kwa moja kwani antonimia ya halali ni haramu. Vilevile kwa kuzingatia maoni ya Wamitila, oksimora ni maneno mawili yaliyowekwa pamoja na ambayo hayapatani au hayaingiliani, tunapata oksimora katika kauli ya Mtu III. Maneno ambayo yana mgotano ni ‘kuhalalisha haramu’ na ‘kuharamisha halali’. Kwa kuyagawa maneno haya katika makundi haya mawili tunaibuka na oksimora hizi. Neno ‘kuhalalisha’ ni kitenzi cha kufanya jambo likubalike kulingana na sheria au kanuni, idhinisha au ruhusu. Nalo neno ‘haramu’ ni kivumishi ambacho huwa na maana ya kwenda kinyume na kanuni za dini, batili au hali isiyo halali au isiyotii sheria. Kauli hii kwa hivyo ina mgotano kwani halali na haramu ni antonimia. Mgotano huu unaifanya kuwa oksimora ya moja kwa moja. Maelezo haya vilevile yanaweza kutumika katika maneno mawili yaliounganishwa ambayo ni ‘kuharamisha halali’ Katika muktadha wa matumizi ya oksimora hizi katika kazi hii, usemi huu unatamkwa na Mtu III.

Katika harakati za Mtu I na Mtu II kunywa pombe, wanajadiliana kuhusu uovu wa wizi wa Matari. Ubishi wao unazuka baada ya Mtu I kumsifu Matari kuwa mtu mkarimu na asiye mkono birika. Hali hii, Mtu II anaiona kuwa mbaya kwani anaonelea kwamba anachojaribu kufanya Mtu I ni kuhalalisha tabia ya wizi ya Matari. Mtu I anafanya hivi kwa sababu yeye ni mfaidi wa pesa haramu anazonunuliwa nazo pombe na Matari. Huku ndiko ‘kuhalalisha haramu’. Kauli hii haimhusu tu Matari ila kuna wengine kama vile majaji, mawakili, maaskari polisi, wanasiyasa, wahubiri, wahadhiri ambao ni wezi na hata Mtu I na Mtu II ambao wamekubali kununuliwa pombe na pesa hizo haramu. Licha ya hayo, wao pia wanajihusisha na unywaji wa pombe haramu na kwa hivyo ‘kuhalalisha haramu’.

Kuna kugotanishwa kwa maneno mawili katika kauli ‘kuhalalisha haramu na kuharamisha halali’. Katika ilimwengu halisi tunaposema kuhalalisha haramu na kuharamisha halali tunaona maana kuwa tunageuza kitu ambacho hakifai au ni kinyume na sheria na kukifanya kukubalika kisheria. Vilevile ni kuchukua kile kinachofaa na kukidunisha ili kionekani kuwa hakifai kisheria. Ufasiri huu wa hali halisi ya matumizi ya maneno haya hautoi maana jinsi mhusika katika matini anavyokusudia. Katika hali dhahania ya matini hii tumerejelea tabia walizo nazo Mtu I na Mtu II. Wanajua kuwa Matari hafanyi kazi yoyote inayompa ujira. Kwa hivyo wana ufahamu kuwa Matari ni mwizi na ingawa wanamtegemea kwa kinywaji, si sawa kwani hali hiyo ni sawa na wao kuwa wezi vilevile.

La pili ni kuwa kileo wanachokunywa kwa Fiona ni haramu na wanatetea kuwa ndicho kinachofaa. Kwa kawaida nchi huwa na taratibu zinazofuatwa ili kukifanya kitu fulani kukubalika ili kitumike na umma kwa sababu za kiusalama. Mwanzoni mwa tamthilia hii tunaona kuwa walevi hawa wanafahamu kuwa vileo haramu vya aina hii hupofusha watu na hata kuhatarisha hali zao za kiafya. Kauli zao zinaunga mkono uamuzi kuwa jamii inapinga vileo ambavyo havijahalalishwa kwa sababu ya madhara yavyo. Kwa hivyo oksimora hii katika maana yake kiushi tunapata fasili kuwa taratibu za nchi ndizo zinazochangia katika hali ya uvunjaji wa sheria. Ukosefu wa pato katika jamii ili kujikidhi kimaisha unaifanya jamii kujihusisha na bishara ya aina hii ambayo huleta bidhaa isiyo halali katika masoko. Mara nyingi bidhaa hii huwa haijakaguliwa na kuidhinishwa kwa matumizi ya watu pamoja na usalama wake kwa wenye kuitumia. Bidhaa hii bandia ambayo haikubaliki kisheria inapopenya na kuingia katika masoko na inapopata watumizi ambao hununua na kutumia basi inakuwa imehalalishwa kiharamu, ile iliyokaguluwa na kukubakliwa kisheria inapoachwa basi huwa imeharamishwa kihalali na watumizi. Katika hali ya kawaida, ikiwa bidhaa ni nzuri basi huwa na wanunuzi. Ikiwa haina wanunuzi, basi bidhaa hiyo hutwezwa. Pombe haramu ya Fiona haifai kutuzwa kwani ina madhara si haba kwa jamii hiyo.

Kwanza imewafanya Mtu I, Mtu II na Mtu III kushinda kwa Fiona mchana kutwa. Vilevile imewafanya wanaume hawa kutowajibika au kuzitelekeza familia zao, mbali na

hayo, pombe hii imekuwa chanzo cha upotovu wa vijana kwani kule kuna uzinzi na umbeya pamoja na wizi. Haya yote si mambo halali.

Hali hii inazua oksimora nyingine. Fiona kama mgema , hafai kutuzwa anafaa kutwezwa kutokana na athari ya biashara yake katika jamii. Hali ya umasikini ya Mtu II inamfanya kuwa na uamuzi huu kwani bado anasema:

Mtu II: 'Haramu tamu' (uk 6),

Huu ni usemi wenye mgotano. Katika ulimwengu halisi neno 'haramu' ni kivumishi kilicho na maana ya kwenda kinyume na kanuni za dini au hali isiyo haki, halali, isiyotii sheria au batili. Nalo neno 'tamu' ni kivumishi chenye maana ya kitu chenye ladha ya kupendeza kinywani au kitu kilicho na mwonjo mzuri. Vilevile ni kitu chenye kuleta furaha. Maana ya maneno haya katika usemi huu yana mgotano. Katika ulimwengu halisi sheria huruhusu jambo kutendeka na kwa hivyo kulifanya halali ambapo kinyume chake ni haramu. Jambo lililowekewa vikwazo bila shaka huwa na athari kwa jamii. Katika hali halisi ya jamii kitu kilicho haramu hakiwezi kuleta furaha ila dhiki tupu. Mtu II anatamka kauli hii katika mazungumzo yake na Mtu III. Hapendezwi na tabia aliyonayo ya kununuliwa kileo na Matari ambaye anatumia pesa zinazotokana na wizi. Hali hii anaiona kumfanya kuwa sawa na mwizi. Ufasili huu tunaupata katika ulimwengu dhahania. Mtu II anaona kuwa ni makosa kula kitu ambacho hujakitolea jasho. Oksomora hizi zilizotumika katika kauli tulizotambua zinazua maudhui ya sheria na maadili katika jamii. Nchi yoyote huwa na sheria ili kuwalinda watu wake. Sheria hizi zikizingatiwa na taasisi za kitawala kwa mfano polisi kutakuwa na msimamo thabiti wa kutekeleza sheria hizi. Jamii nayo huwa thabiti na yenye watu wenye malengo na kuheshimu sheria. Ikiwa kuna ulegevu fulani, basi unyanyasaji hutokea kwani wenye kutumia wasaa au fursa hiyo kufanya mambo haramu hawachelei.

Mtu II: Nauliza tena , ukarimu wa mwizi tuufanyeje?

Wote: Tuususie. (uk 7)

Kauli ya Mtu II katika mazungumzo yake ulevini ni yenye mgotano. Hii ni oksimora isiyo ya moja kwa moja tunapofuata mtazamo wa Shen (khj). Katika kauli hii kuna mgongano wa maneno. Neno 'mwizi' ni haiponimia ya mtu na ni nomino yenye maana ya mtu mwenye mazoea ya kuchukua mali ya watu bila idhini yao. Nalo neno 'ukarimu'

ni nomino yenye maana ya tendo la kukaribisha watu chakula au kutoa vitu au pesa au kuwasaidia wenye kuhitaji msaada. Bila shaka kitendo cha wizi hakiwezi kuambatana na ukarimu. Mwizi hutumia mabavu ilhali mkarimu hutoa kwa hiari. Katika ulimwengu halisi wizi huwa pigo kwa mwenye kuibiwa na humfanya afadhaike kwa kupoteza alichokienzi. Aliyeiba bila shaka huwa hajui juhudi alizopitia mwenye kuibiwa katika kufanikisha kuwepo kwa mali hiyo. Mtu II anajaribu kukejeli tabia ya wizi ya Matari na vilevile tabia ya mazoea ya wanaomtegemea Matari katika ununuzi wa kileo. Hakuna ukarimu wowote hapa kwani Matari anawadhulumu wenye mali kwa kuwaibia ili kufanikisha ukarimu wake. Huu ni uozo katika jamii hii. Kauli hii kwa hivyo inaendeleza maudhui ya utovu wa vijana wanaojihusisha na uozo wa wizi na kisha kula raha kwa kutumia pesa ambazo hawakuzitolea jasho kiholela anavyofanya Matari.

3.6 Tanakuzi

Tanakuzi ni tamathali ya usemi ambayo hutumia dhana ya kukinzana ili kuleta msisitizo wa wazo bila kutengua dhana ya msingi.

Wamitila (2008:405) ana maoni kuwa dhana hii hutumiwa kama mbinu ya kiusemaji au kibaalagha kurejelea msembo ambao unaonyesha ukinzani wa mawazo na aghalabu katika muundo wa kisambamba. Hii ni mbinu ambayo imetumiwa kwa kiwango kikubwa katika methali za semi.

- *Kupanda mchongoma, kushuka ndio ngoma*
- *Kukopa harusi, kulipa matanga*
- *Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi*

Msokile (1993:100) anasema tanakuzi ni usemi/uneni unaoonyesha kupingana kwa mawazo. Anatoa mfano wa

*Ilikua ajabu siku za utumwa kuona wapagazi wadogo na wanyonge
kubebeshwa mizigo mikubwa na mizito na wale wenye nguvu wakichukua
mizigo miepesi.*

Wamitila (2008:508) anasema kweli-kinzani ni aina ya tanakuzi ambapo kauli au maneno yanayotumiwa huweza kuonyesha kupingana fulani katika kiwango cha juujuu ingawa katika kiwango cha ndani yana maana wazi.

Katika usemi unaosemwa na Tonge kuna tanakuzi. Ukinzani unaibuka katika maneno ‘hawezi hata akiwezesha’. Neno ‘weza’ lina maana ya kuwa na maarifa, ari na msisimko wa kufanya jambo. Kwa hivyo mfasiri wa kauli hii anakumbana na ukinzani anapokabiliana na maneno ‘hawezi’ na ‘akiwezesha’. Hebu tutathmini kauli hii ya Tonge na Vero wakiwa mahakamani:

Tonge: Asemavyo huyu bibi ni kweli mheshimiwa. Mumewe huyu bibi hawezi hata akiwezesha. Hana *network*, amekatika waya.

Vero: Tafadhali utazame wema wa mbaya wetu.(uk 78)

Tonge anapotamka kauli ya mume kutoweza hata akiwezesha anajirejelea bila kujua. Kulingana na muktadha wa mazungumzo, ni yeye ambaye hana uwezo wa kumpa mke uja uzito. Kauli hii ina maana mfichamo ambayo haisemi au kutoa waziwazi matatizo ya ndoa yanayomsibu Tonge. Hali ya kutoweza anayoizungumzia Tonge ni ukosefu wake yeye wa kuwa na uwezo wa kumpachika Vero mimba. Katika utamaduni wa Kiafrika swala la ugumba huwa halizungumziwi waziwazi. Muktadha huu kwa hivyo unamfanya Tonge kutaja yanayomsibu katika ndoa yake na kwa hivyo kujenga taswira ya kujiondoa katika miiko ya kuzungumzia utasa, jambo ambalo halikubaliki kulingana na utamaduni wa mwafrika. Tonge na mkewe wamekuwa katika ndoa na hawakufanikiwa kupata mtoto hadi Matari alipoingilia maisha yao ya ndoa na kufanikiwa kumpa Vero mimba. Kwa hivyo usemi huu umeficha ulemavu alionao Tonge na hauzungumziwi moja kwa moja ila kwa tasfida. Tunaweza kusema kuwa Tonge anaonea aibu hali hii aliyomo. Jambo zuri ni kuwa anafahamu hali hii. Kwa hivyo ufasili wa tanakuzi hii unaibua maana katika muktadha wa matumizi yake. Mbeleni tuna habari kutokana na mazungumzo ya Mtu I, Mtu II na Mtu III wakiwa kwa Fiona na kuzungumzia tabia ya Matari ya kujihusisha kimapenzi na Vero ambaye ni shemejiye.

Vero kwa upande wake anatetea vikali aliyempa mimba na kwa hivyo kuzua tanakuzi nyingine. Kauli ‘utazame wema wa mbaya wetu’ ni tanakuzi anayoitamka Vero. Vero anamuenzi Matari kutokana na ukarimu wake wa kumwezesha kuwa na mimba. Kwa hivyo uamuzi wa mahakama wa kumweka Matari kizuizini utamnyima mwana atakayezaliwa nafasi ya kuingiliana naye. Kwa hivyo katika kufasiri kauli hii, tunaangalia ubaya wa Matari ambao ni tabia ya wizi. Vero ameshuhudia hali hizi zote za ubaya na wema wa Matari. Matari amemfaa Vero kwa kumpa mimba na vilevile amemdhulumu

Vero kwa kumwibia ng'ombe. Ufasili huu ni wa dhahania kwani unapatikana tu kwa muktadha kurejelewa.

Kwa hivyo usemi ambao ni tanakuzi hutokea katika sentensi na huwa ni sawa na kweli kinzani. Kumbuka Vero ni mkewe Tonge na Tonge ndiye anayesema kuwa mumewe Vero hawezi hata akiwezesha. Hali ya kuweza kiukiushi, ni uwezo wa mwanamume kumtia mke mimba. Kwa hakika mimba aliyonayo Vera si ya Tonge ila ni ya kakake Tonge ambaye ni Matari. Kauli hii inaibua maudhui ya uzinzi au uasherati katika jamii, mbali na hilo, tanakuzi tulizozirejelea hapa zinaibua maudhui ya utamaduni na jinsi unavyomkandamiza na kumshushia mtu hadhi. Hali hii tunaiona kwa Tonge ambaye licha ya kufahamu ulemavu wake, anauzungumzia tu awapo kortini. Tonge anajua kuwa hana uwezo wa kumpachika mkewe mimba lakini ni jambo la kushangaza kuwa mkewe ni mjamzito. Bila shaka huu ni wema wa mbaya wetu.

3.7 Kejeli

Mbatiah (2001:27) anasema kejeli ni maneno yanayotumika katika matamshi na ambayo huwa ni maneno ya kuchoma, kukata na kutia chungu. Mbatiah anaendelea kusema kuwa ingawa kejeli huchukuliwa kisawe cha kinaya, inafaa kusisitiza kuwa kejeli ni aina ya kinaya yenye ukali wa kipekee. Kwa hivyo kinaya huwa na jukumu la kutoa maana, kinyume na kinachosemwa kwa ajili ya kuonya, kushutumu au kumtweza mtu.

Kuhenga (1977) anakubaliana na Mbatiah. Naye anasema kejeli ni usemi wa kimafumbo ambao humuudhi mtu kwa nia ya kumuonya kichinichini bila ya bughudha. Katika mazungumzo yafuatayo kuna kejeli. Hebu tuyatathmini:

Mtu II: Kwani wewe kubwabwajika ni siri tangu lini?...*(anaimbaimba kwa kejeli)* kindumbwendumbe chalia, kikojozi kakojoa, na nguo kazitia moto.

Mtu I: *(Kwa hamaki)* mimi kikojozi nabwabwajika?...
Nitakutandika mpaka mkeo akose kukutambua.

Mhusika Mtu II ametumia kejeli katika usemi wake. Kitendo hiki cha kuwa kikojozi si kitendo cha kuonewa fahari. Mtu I anapoambiwa haya anakasirika na kumfokea Mtu II maneno makali. Kitendo cha kuandamiza usemi wake na wimbo ndicho kinaufanya

usemi huu kuwa kejeli kwani wimbo huo unajenga picha ya mzaha katika kuuwasilisha ujumbe huu wa kujaribu kuzungumzia kitendo hiki cha aibu anachotekeleza Mtu I baada ya kulewa chakari. Kwa kufanya hivi, Mtu II anamshutumu na kumtweza Mtu I.

Mazungumzo ya Mtu II, Mtu I na Vero vilevile yana kejeli. Mukstadha wanayoyasema maneno haya unawahusisha Mtu I, Mtu II, Vero na Lila. Kuwepo kwa Lila hakutambuliki kwani amejibanza ili kusikiza udaku wa Mtu I na Mtu II. Vero haudhiki kwa maneno ya Mtu I na Mtu II ingawa maneno haya ni ya kuudhi kwa kuwa yanagusia mienendo ya wanajamii ya Temba akiwemo yeye. Kwa mfano Mtu II anamwambia Vero: ‘Bila shaka kwema tu... tena nyumba ya Bwana Temba njema tu tangu hapo... Nyumba ya amani na muamana na itifaki. Haijui mawimbi yanayosukasuka watu wengine hapa kijijini.’

Anayeyafanya maneno haya kuwa kejeli ni mhusika Lila kwani kulingana na mukstadha, Lila ameusikia udaku wote Mtu I na Mtu II waliousema kuhusiana na jamii ya Temba. Lila ni mmoja wa waliozungumziwa kwa njia hasi ambayo hailingani na tabia zake. Mengine waliyosema kuwahusu Matari, Vero na Tonge ni ya ukweli. Hali hii inamkasirisha Lila na kwa hivyo kutupa nafasi ya kuamua kuwa kauli hizi zina kejeli. Lila na Vero katika mazungumzo yao baadaye wanajadiliana kuhusu mazungumzo aliyoyasikia Lila. Hali hii bila shaka ni ya kushtumu baadhi ya vitendo vya Matari, Vero na hata Lila. Kejeli hizi bila shaka zinaibua maudhui ya maadili katika jamii kwani licha ya Mtu I na Mtu II kuwa walevi, wan uwezo wa kutambua uozo ulioko katika jamii n ahata kuuzungumzia.

3.7 Hitimisho

Katika sura hii tumeangalia jinsi tamathali za usemi tulizoteua zimeibua maudhui na kuyandeleza katika tamthilia hii. Miongoni mwa maudhui yaliyoibuka ni: upotovu wa vijana, malezi ya mzazi kwa mtoto wa kiume na wa kike, madhara ya dawa za kulevya miongoni mwa mengineyo. Tumeona kuwa ukiushi wa kisemantiki katika kauli tulizoteua na kuzichanganua zimechangia pakubwa katika uelewaji wa tamthilia nzima zinapochanganuliwa kimukstadha kwa jumla.

SURA YA NNE

HITIMISHO

4.0 Utangulizi

Katika sura hii tunatoa hitimisho la utafiti huu. Sura hii ina sehemu zinazoshughulikia matokeo ya utafiti huu, umuhimu wa utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi juu ya *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu*. Tunatoa muhtasari wa yale tuliyotekeleza na kuyaibua katika uchanganuzi huu.

4.1 Kuhusu Madhumuni ya Utafiti.

Katika kazi hii, tulidhamiria kutekeleza mambo matatu makuu: kwanza kabisa, tulidhamiria kutambua na kuchanganua tamathali za usemi za sitiari, chuku, tashihisi au uhuishi, tashbihi, kejeli, tanakuzi na oksimora katika tamthilia za *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu*. Tumeitekeleza dhamira hii katika sura ya pili na sura ya tatu mtawalia. Katika sura ya pili, utafiti ulionyesha uhusiano wa karibu uliopo baina ya sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora. Kimsingi tuligundua kuwa tamathali hizi zina mchango mkubwa katika kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui katika tamthilia tulizoteua. Uchunguzi ulibainisha kuwa tamathali hizi zinatumia maneno ya lugha ya Kiswahili ambayo kisemantiki yana maana tofauti lakini zikitazamwa kimuktadha katika matini zilimotumika maana kiushi ilijitokeza na kwa hivyo kuwasilisha ujumbe kwa hadhira au msomaji. Kwa jumla tuligundua kuwa ni vugumu kuchanganua tamathali yoyote ile bila kuzingatia muktadha kwani maana zina ibuka na kudhihirika kwa kurejelea muktadha wa matini.

Pamoja na hayo, uchunguzi ulilenga kutathmini mchango wa tamathali hizi katika kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui katika tamthilia tulizochagua. Lengo hili limetekelezwa katika sura ya pili na ya tatu ya tasnifu hii. Uchanganuzi wa tamathali hizi za usemi katika *Mbaya Wetu* na *Zinguo la Mzuka* ulibainisha kuwepo kwa mchango wao mkubwa wa kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui katika ufasili wa ukiushi wa kisemantiki. Tunashikilia hoja hii kwa kuwa uchanganuzi lazima uwe na uwezo wa kushawishi na hata kukubalika na wachanganuzi wengine. Kwa hivyo kutokana na tamathali hizi, tuligundua kuwa ukiushi wa kisemantiki umeibua maudhui yakiwemo:

ukoloni mamboleo, maana ya uhuru, uongozi mbaya, ufisadi, utegemezi, siasa, umasikini na maridhiano katika tamthilia ya *Zinguo la Mzuka*. Katika tamthilia ya *Mbaya Wetu*, kuliibuka maudhui kama vile malezi ya mzazi kwa mtoto wa kiume na wa kike, upotovu wa vijana, ufisadi, madhara ya dawa za kulevya, umasikini, swala la ndoa na uchumba, mapenzi, uajibikaji na maridhiano. Kwa hivyo tuligundua kuwa kila sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora iliyojitokeza katika tamthilia hizi tulizoteua imesheheni mojawapo au zaidi ya maudhui haya. Kwa hivyo tamathali tulizoteua zimekuwa na mchango mkubwa sana katika ukiushi wazo wa kisemantiki kuibua na kuwasilisha maudhui. Tamathali hizi zilikuwa nguzo muhimu za mwonoulimwengu wa waandishi hawa katika kutunga kazi zao za sanaa wakijikita katika jamii. Kupitia tamathali hizi kazi hizi za sanaa zimeibua madhila yaliyopo katika jamii, visababishi vya madhila haya na suluhu kwa matatizo haya yaliyomo katika jamii tunamoishi.

Katika uchunguzi wetu, tumeangazia mtindo katika kiwango kimoja ambacho ni kiwango cha ukiushi wa kisemantiki. Uchunguzi huu umegundua kuwa waandishi Leonard Sanja na Ken Walibora wametumia lugha kwa upekee fulani tukirejelea tamathali za usemi ili kujadili maswala mbalimbali yanayoikumba jamii. Tumegundua kwamba matini hizi zimetumia ukiushi wa kisemantiki kueleza mawazo yao. Tumeona kwamba kuna ukiushi wa kimaana kwa kutumia tamathali za usemi ili kuzua maana mbalimbali. Tamathali hizi za usemi zimechangia thamani ya kiujumi katika tamthilia hizi. Tumbainisha kuwa tamathali za usemi zina umuhimu mkubwa kwa kuwa zimetumiwa kufafanua maana, kutoa mifano mwafaka, kuibua hisia, kuzua ucheshi na kuongeza ujumi wa kisanaa. Aidha tuligundua kuwa kuna uwezekano wa kufanya uchanganuzi kuwa wenye kukubalika ikiwa mchanganuzi ataanza kwa kuichunguza kauli husika kiisimu. Kwanza kauli hii kiushi hutambuliwa na kisha kuchanganuliwa kiisimu ambapo maana katika ulimwengu halisi huibuka na kisha jinsi ukiushi unavyojitokeza. Hatua inayofuata huwa kujaribu kugundua umuhimu wa kauli hiyo kiushi ilivyojitokeza kimuktadha na kwa hivyo kuibua udhahania katika kauli hiyo.

Nadharia ya elimumitindo imetufaa sana katika kuhakiki mtindo katika *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu*. Tuligundua kuwa usemi wenye ukiushi si wa kiajali ila hutumika kwa kusudi fulani na kwa kiwango kikubwa huwa na maana unapotathminiwa na msomaji au msikilizaji unapohusishwa na muktadha wa matumizi yake. Haya yote hutokea katika tamathali yoyote ya usemi iliyotumika katika matini.

Kuhusu umuhimu wa utafiti wetu, tumethibitisha kwamba mtindo katika tamthilia hasa ukiushi wa kisemantiki ukilinganishwa na ukiushi wa kiwango kingine kama vile ukiushi wa kisintaksia na ukiushi wa kimsamiati; ukiushi wa kisemantiki una mchango mkubwa sana katika kuibua maudhui, kuyaendeleza na kuyawasilisha vilevile.

Uelewa wa ukiushi wa kisemantiki kwa kuzingatia nadharia ya elimumitindo ni muhimu kwa msomaji pamoja na mwandishi wa utanzu wa tamthilia ili aweze kufikia dhamira yake ya kuelewa na vilevile kuwasilisha ujumbe. Hivyo basi, utafiti huu utatoa mwanga wa kuhakiki tamathali za usemi kiukiushi kwa kuirejelea kazi hii kimtindo. Kazi hii itawafaa wachanganuzi wa fasihikimtindo kwa kuzingatia ukiushi wa kisemantiki.

4.2 Kuhusu Nadharia Tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete tatu kuu. Kwanza tamthilia za *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu* zina ukwasi wa sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora. Tulizitambua na kuzichanganua. Kwa hivyo nadharia tete ya kwanza ni kweli kuwa tamathali tulizoteua zimetumika kuanzia mwanzo hadi mwisho katika matini tulizoteua. Tamathali hizi zilitambulika kwa kuyarejelea maelezo ya wataalam mbalimbali kuzihusu na kisha tukazieleza katika kuzichanganua kwa kuhakiki maana katika hali halisi na maana inayojitokeza katika hali dhahania. Maana dhahania ilionekana kutegemea muktadha wa matumizi ili kuwepo na ufasiri unaokubalika. Tamathali hizi zimetumiwa kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui na kwa hivyo kuwa kiungo kikubwa mno na kuyafanya matendo ya tamthilia hizi kunata katika akili za hadhira na hata msomaji na kuwa msingi muhimu wa kuyakumbuka matukio haya.

Katika nadharia tete ya pili, tulidai kuwa vipengele vya tamathali vya sitiari, chuku, tashbihi, tashihisi, kejeli, tanakuzi na oksimora vimechangia pakubwa katika kuibua, kuendeleza na kuwasilisha maudhui katika tamthilia tulizoteua. Uchunguzi ulithibitisha ukweli wa dai hili kupitia ukiushi wa kisemantiki uliotokana na tamathali za usemi tulizoteua. Uchunguzi ulibainisha kuwa tamathali tulizoteua ndizo mihimili ya maudhui kwa kuzingatia muktadha wa matumizi yazo. Kwa maoni yetu, tamthilia hizi hazingefikia dhamira yake kwa kiwango fulani ikiwa tamathali za usemi hazingetumika. Tamathali za usemi zilitumika katika kuziboresha kazi hizi za Sanaa. Tamathali hizi kwa hivyo zimesheheni maudhui mbalimbali. Maudhui yaliyoibuka ni kama vile swala la ndoa na uchumba, umaskini, ufisadi, uajibikaji, uongozi mbaya, athari za dawa za kulevyo, maana ya uhuru, ukoloni mamboleo, siasa na kadhalika. Nadharia tete hii vilevile tumeiona kuwa ya kweli.

Katika nadharia tete ya tatu tuliona kuwa tamathali za usemi tulizoteua zilikuwa na upekee wa kimatumizi na mwandishi katika ukiushi wa kisemantiki na hivyo kuibua maudhui yaliyo na upekee fulani kimuktadha. Kauli hizi zenye tamathali za usemi zilipatikana kusheheni maana iliyokuwa na ujumbe wa usemi. Nadharia ya elimumitindo ilitumika kwa njia mwafaka na kuwezesha kubaini upekee wa maudhui katika matini tulizoteua kutokana na tamathali hizi.

4.3 Changamoto za utafiti

Katika kipindi hiki cha utafiti tulishuhudia matatizo mawili makuu. Kwanza kabisa, matini tuliyoteua kutumia ya *Zinguo la Mzuka* ilikuwa na mfano mmoja tu wa tamathali ya usemi ya oksimora. Hali hii ilikuwa ya kuvunja moyo kwani miongoni mwa tamathali tulizoteua kuzitambua na kuzichanganua ni oksimora. Hata hivyo, uteuzi wa matini ya *Mbaya Wetu* uliokoa jahazi kwani tulifanikiwa kupata mifano ya kuridhisha. Tatizo jingine lilikuwa wakati. Kipindi cha miezi minne hakikuwa cha kutosha kwani ilikuwa vigumu kushughulikia kazi hii pamoja na majukumu ya nyumbani na ajira ya ualimu.

4.4 Mapendekezo

Utafiti wetu umejikita katika kipengele cha fani cha mtindo hasa tamathali za usemi. Hatukushughulikia vipengele vingine vya fani kama vile muundo, wahusika na mandhari. Kwa hivyo mtafiti yeyote atakayevutiwa na kutafiti kuhusu tamthilia hizi za *Zinguo la Mzuka* na *Mbaya Wetu* ana nafasi ya kufanya tahakiki hiyo. Mbali na hayo tulijifunga katika ukiushi wa kisemantiki na kuacha ukiushi wa kisintaksia na ukiushi wa matumizi ya msamiati.

Pia, tunapendekeza kuwa uhakiki zaidi ufanywe kuhusu tamthilia hizi kwa kutumia nadharia tofauti na tuliyoitumia ya elimumitindo ambapo tumechunguza tamathali za usemi.

MAREJELEO

- Bally C. (1909) *Saussurean Linguistics*. The Hague. Manton de Gryter.
- Barry P. (2002) *Structuralism: Beginning Theory. An introduction to Literary and Cultural Theory*. Manchester. Manchester University Press.
- Burke K. (1952) *Psychology and Form katika Criticism: The major Statemements*. Kaplan C. Mhariri. St. Martins Press. New York.
- Chatman S. (1967) *Literal Style. A Symposium*. New York. Oxford University Press.
- Combes G. (1953) *Structuralism*. Boston. Ronald Press.
- Crystal D. na Davy D. (1969) *Investigating English Style*. Longman Publishers
- Gibbs, W. R. and Kearney, L. R. (1994) 'When Parting is such Sweet Sorrow: The Comprehension and Appreciation of Oxymora', *Journal of Psycholinguistic Research* 23:75–89.
- Habwe J. na Karanja P. (2005) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi. Phoenix Publishers.
- Indangasi H. (1988) *Stylistics*. Nairobi University Press.
- Kitsao J. (1975) A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts. Tasnifu ya M.A. Kiswahili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kuhenga C. (1977) *Tamathali za Usemi*. Dar es Salaam. East African Literature Bureau.
- Leech G. na Short M. (1981) *A Style in Fiction: An Introduction to English Fictional Prose*. London. Longman
- Lodge D. (1988) *Structuralism and Literary Criticism*. London. Longman Publishers.
- Lugwiri (2011) Sitiari, Taashira na Tashbiha katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*: uhakiki wa kimtindo. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Magare (2002) Uhakiki wa Tamthilia ya *Amezidi* kama kazi ya Kibwege. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mbatiah M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Text Books Group and Publishing.
- Mohamed S.A. (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili. Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi*. Nairobi. East African Education Publishers.
- Msokile M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. East African Educational Publishers Limited

- Mulokozi (1989) *Tanzu za Fasihi*. Mulika 21 Dar es Salaam.
- Murumba (2013) *Mtindo Katika Watu wa Gehenna*. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ngara E. (1990) *Ideology and Form in African Poetry*. James Carry. London.
- Njogu K. na Chimera R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.
- Sanja, L. (2011) *Zinguo la Mzuka*. Nairobi. Focus Publishers.
- Senkoro F. (1982) *Fasihi*. Press and Publicity Center, Dar es Salaam.
- Senkoro F.M.E.K. (1988): *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam University Press.
- Shen, Y. and Balaban, N. (2005) 'Cognition and Oxymoron', Paper presented at International Workshop: Text and Cognition, 15–18 May, Tel Aviv University.
- Simpson P. (2004) *Stylistics: A Resource Book for Students*. London. Routledge.
- Swift J. amenukuliwa na Crystal D. (1987) katika The Cambridge University Press. New York.
- van Peer, W. (1986) *Stylistics and Psychology: Investigations of Foregrounding*. London: Croom Helm.
- van Peer, W. and Hakemulder, J. (2006) 'Foregrounding', in Keith Brown (ed.) *The Pergamon Encyclopaedia of Language and Linguistics*, Vol. 4, pp. 546–51. Oxford: Elsevier.
- Wales K. (2001) *Dictionary of Stylistics*. Toleo la Pili. Harikow person Education.
- Walibora, K. (2014) *Mbaya Wetu*. Nairobi. Moran Publishers.
- Wamitila K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers.
- Wamitila K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publishers.
- Wamitila K.W. (2003) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Focus Publication Limited. Nairobi.
- Wamitila K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide~Muwa Publishers Limited.